Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 25 Juni, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 100

**Kukabiliana na Hali ya Njaa**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mvua za Vuli zilipungua sana msimu huu na mavuno ya chakula nchini msimu uliopita si ya kuridhisha ingawa Waziri wa Kilimo na Chakula alisema ndani ya Bunge hili kuwa hakutakuwa na njaa nchini, lakini hali hivi sasa ni ngumu hasa maeneo ya baadhi ya Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki:-

(a) Je, hadi hivi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu imejiandaaje katika kukabili hali hiyo ya njaa nchini?

(b) Je, hadi leo unapojibu swali hili ni Wakuu wa Wilaya wangapi walioleta taarifa ya njaa katika Wilaya zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maandalizi yafuatayo:- Hivi sasa *SGR* inayo mahindi tani 51,971 kama akiba ya Serikali. Akiba hiyo itaongezeka hadi kufikia

tani 75,523 kama inavyoelezwa katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vile vile wafanyabiashara binafsi wana kiasi cha tani 114,899. Zaidi ya hapo kuna msaada toka Serikali ya Japan na India ambao jumla yake ni tani 51,000.

Aidha, napenda ieleweke pia kuwa kulingana na takwimu za kilimo inakadiriwa wananchi wenyewe wanayo akiba ya tani 333,740. Kwa hali hiyo upungufu uliopo ni tani 300,000 ambazo wafanyabiashara wanaruhusiwa hivi sasa kuagiza kutoka nchi za nje.

Aidha, hivi sasa Hazina imeruhusu tani 7,215 kutoka *SGR* ambazo zitauzwa katika maeneo yatakayokuwa yanajitokeza kuwa na upungufu mkubwa wa chakula. Vile vile kuanzia wiki ijayo tathmini ya kina inafanyika nchi nzima na hii itaainisha maeneo yote yanayohitaji msaada. Tunategemea kuweka mkakati zaidi baada ya kupata taarifa ya tathmini ya kina.

(b) Hadi leo Wilaya 52 zimekwishaleta taarifa za kuwepo kwa upungufu wa chakula na njaa sehemu fulani fulani ikiwemo Wilaya ya Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa tathmini ambayo ilifanywa na Waziri, nina swali moja tu dogo la nyongeza.

Kwa kuwa chakula nilichokiomba hapa sio cha kuuza ni cha biashara kwa sababu hawa wana njaa kwa hiyo, wanahitaji chakula cha bure, chakula cha kazi na chakula cha bei nafuu. Kwa hiyo, Waziri tathmini aliyoifanya alikuwa hajatangaza utaratibu wa kusaidia jimbo hilo la Morogoro Kusini Mashariki na maeneo mengine ya Tanzania.

Je, hatua zinaweza zikachukuliwa za haraka zaidi kwa ajili ya wananchi wa Tarafa ya Ngerengere na Mikese, ambayo mimi nimeshaweka maji ndugu kwa ajili ya kusaidia hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, nimesoma vile vile maelezo ya Mheshimiwa Pawa akichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maandishi aliandika haya na itatusaidia sana katika tathmini. Lakini ndani ya maandishi yake anasema ameshatoa kiasi fulani cha chakula kwa Shule za Msingi na baadhi ya vijiji ameviorodhesha. Nampongeza sana kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Lakini haya aliyosema utaratibu wa kugawa chakula cha bure, cha kazi na chakula ambacho kitauzwa kwa bei nafuu naomba anipe muda kidogo tusubiri hii tathmini itahusisha wataalamu wengi sana na tutaifanya kwa haraka.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadi sasa ni Wilaya 52 ndio zilizopeleka taarifa na kwa kuwa Mkurugenzi wa Wilaya ndiye mwenye vikao vyote vya kisheria na wataalamu

wote kutoka kwenye vijiji ambao wana uwezo wa kufanya tathmini ya kina na kwa kuwa wote hao wanawajibika kwake; je, ni lini sasa Serikali itaanza kutumia mtiririko wa Ofisi ya Mkurugenzi pamoja na vikao vyake kuanzia *ODC* kupeleka taarifa hizi ili wawe na uhakika wa kupata taarifa zilizopitia kwenye vyombo vya kisheria katika ngazi zote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa habari ya maafa *authority* ni Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Kamati wa Maafa ya Wilaya ni Mkuu wa Wilaya.

Najua swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, anazungumzia habari ya Halmashauri na kwa sababu maalum ya Wilaya ya Karatu. Lakini kwa kweli kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na Serikali masuala ya maafa yanasimamiwa na Kamati iliyo chini ya Mkuu wa Wilaya. Wakuu wa Wilaya hawa ndio waliokwishaleta tathmini katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo na Chakula ni Wilaya 52 lakini wengi wameelezea juu ya upungufu wa chakula.

Tunapeleka timu za wataalamu kwa sababu tunahisi utaratibu wa namna ya kutathmini wazi wazi ili takwimu hizi ziweze kuonekana sehemu nyingine katika Wilaya haupo. Si kweli kwamba wataalamu wote wa kilimo wanajua kufanya tathmini ya jambo hili.

Kwa hiyo, tunapeleka timu ya wataalamu kuthibitisha na pengine kuweza kuzungumza nao na kuainisha utaratibu mzuri zaidi wa kuweza kukabiliana na tatizo hili. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakurugenzi ni sehemu tu ya Kamati za Maafa ambayo itakuwa iko chini ya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mbali na ukame uliojitokeza mwaka huu sababu nyingine zinazosababisha upungufu wa chakula kila mwaka ni wananchi kutopatiwa huduma ya utaalamu wa kilimo bora. Je, Serikali ina mikakati gani ya kupeleka utaalamu wa kilimo shambani na sio wa kukaa ofisini na kukusanya takwimu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wanahitaji utaalamu mashambani na Serikali imejitahidi sana kusambaza watalamu Mabwana Shamba na Mabibi Shamba sehemu nyingine wakafika mpaka kwenye ngazi za vijiji. Hata hivyo ni muda mrefu tangu Serikali imetufundisha hata wananchi kwa sababu wananchi wengi wamekuwa wanalima kilimo cha aina hiyo hiyo kwa miaka mingi. Kwa hiyo, wananchi nao sasa wamekuwa watalamu wa kilimo. Lakini namshauri Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu wataalamu hawa tunaowasema wako Wilayani pale wasukumeni hao waende vijijini. *(Makofi)*

Na. 101

**Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali huwapa mkopo wa ada wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini; na kwa kuwa Serikali haina utaratibu wa kuwaajiri wakati wanapomaliza mafunzo ya Digrii zao:-

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inarejeshwa Serikalini?

(b) Je, kwa nini Serikali isiite fedha hizo msaada badala ya mkopo usioweza kurejeshwa?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haitoi mkopo wa ada kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu bali hutoa mkopo wa kujikimu chakula na malazi kwa wanafunzi hao wawapo mafunzoni kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu. Ili kuhakikisha kuwa mikopo ya chakula na malazi iliyotolewa kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu inarejeshwa, Wizara yangu inaandaa utaratibu wa kisheria wa kuunda chombo cha kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Wizara yangu kuwa Muswada wa kuunda chombo hicho utawasilishwa kwenye kikao cha Bunge lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2003/04. Chombo cha kusimamia mikopo kitakapokamilika urejeshwaji mikopo utawezekana kwa kuwa chombo hicho kitakuwa na sheria ya usimamizi pamoja na mtandao wa kuwafikia wakopaji.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa fedha iliyokopeshwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wakati utaratibu huu ulipoanza itarejeshwa. Wizara yangu imeendeleza kutunza kumbukumbu za wakopaji kwa kipindi chote na kinachosubiriwa ni kukamilika kwa uundaji wa chombo tajwa ili kisimamie urejeshaji. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa takwimu za wanafunzi wanaopata nafasi za kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu hasa katika Afrika Mashariki inaonekana Tanzania ina namba ya chini kabisa; na kwa kuwa sasa hivi kasi yetu ni uhakika kwamba tunawezesha wanafunzi wanaomaliza darasa la saba kujiunga na Sekondari ili baadaye tuweze kupata wanafunzi safi wa kujiunga na Elimu ya Juu.

Je, Waziri anaweza kunisaidia kufahamu ni wanafunzi wangapi na kiasi gani cha fedha ambacho kimekwishatolewa kwa ajili ya wanafunzi hawa ambao wamepewa mkopo wa chakula na malezi kujikimu hapo vyuoni?

La pili, kwa kuwa tunatarajia kwamba elimu itolewe kwa wanawake na wanaume, je, anaweza kunisaidia ni mkakati gani unaothibitisha kwamba fedha hizo zinazotolewa wanafunzi wa kike nao wanafaidika sawa sawa na wanafunzi wa kiume? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, fedha ambayo tayari imekwishakopeshwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ni kiasi cha shilingi 26,722,926,450. Fedha hiyo imekopeshwa kwa wanafunzi ambao bado wako chuoni na ambao tayari wamekwishahitimu 16,402.

Kuhusu swali la pili Serikali inahakikisha vipi kwamba wanafunzi wanawake nao wanapata mikopo hiyo. Mikopo tunayotoa ni kwa wanafunzi wote wanawake na wanaume. Katika kutoa mikopo hatubagui wanawake wala wanaume. Lakini hata hivyo kwa nyongeza tayari Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina mpango maalum kusaidia wanafunzi wanawake 50 ambao wanasomeshwa bure. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Suala lililoulizwa na Mheshimiwa pale ni kwamba wanafunzi wanaokopeshwa, wakishamaliza masomo yao huwa hawapati kazi. Je, watu hawa wanalipa vipi mikopo yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba mkopo unapoombwa unaombwa kwa hiari, hakuna mtu anayelazimishwa kuchukua mkopo.

Pili, wanapoomba wanaonyesha jinsi watakavyolipa na wana wadhamini. Sasa awe amepata kazi ya kuajiriwa au amejiajiri mwenyewe wajibu wa kulipa mkopo upo pale pale kama utakavyokopa kwenye Benki. Sasa tutawafuata wadhamini hao na watalipa. *(Makofi)*

Na. 102

**Wanafunzi wa Chuo Kikuu Kubadilishiwa Masomo ya Fani Yao**

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH** aliuliza:

Kwa kuwa yapo malalamiko ya wanafunzi wa Chuo Kikuu kubadilishiwa masomo ya fani wanazochagua wanapoingia chuoni na hivyo kusababisha usumbufu wa kimasomo kwa upande wao:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba mtindo huo unaweza kuwa ni matokeo ya kufeli kwa wanafunzi wengi katika masomo yao?

(b) Je, kuna ubaya gani kuwaacha wanafunzi hao kuendelea na masomo waliyochagua kulingana na fani zao?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba mwombaji ambaye hakupata nafasi katika fani ambayo ni chaguo lake la kwanza hufanya vibaya katika masomo yake kwa vile mwanafunzi huyo kwanza, huwa na sifa ya kujiunga na Chuo Kikuu na hutakiwa kuikubali fani hiyo kwa kufanya usajili.

Pili, uamuzi wa kumpatia mwombaji fani nyingine yenye nafasi huwa umezingatia uwezo wake kitaaluma hususan jinsi alivyofaulu katika masomo yake katika ngazi ya Kidato cha Nne na cha Sita. Tatu, hakuna uthibitisho wa kitaalamu kuwa wanafunzi ambao wamebadilishiwa fani wanafanya vibaya katika masomo yao.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubaya mwanafunzi kuendelea na masomo katika fani aliyoichagua. Tatizo kubwa ni kutokuwepo kwa nafasi za kutosha katika fani hiyo ikilinganishwa na mahitaji. Ni nia ya Wizara yangu kuona kuwa raslimali mbalimbali zilizopo vyuoni zinatumika kikamilifu na kwa ufanisi mkubwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, je, ni fani gani ambayo wanafunzi wanawake wanaipendelea zaidi na ni utafiti gani uliofanyika kuona hiyo fani wanayoipendelea zaidi wanafunzi wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kusema kweli wanafunzi wanawake wanapendelea masomo yote. Lakini pamoja na kupendelea masomo yote uchaguzi unategemea sana kufaulu kwa yule mwombaji. Lakini hata hivyo wanafunzi wanawake wako katika fani zote ukianza Uhandisi, Udaktari, Sayansi, Sheria na masomo yote. *(Makofi)*

Na. 103

**Mafunzo kwa Wafanyabiashara wa Bukoba**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (k.n.y. MHE. WILFRED M. LWAKATARE)** aliuliza:-

Kwa kuwa uboreshaji wa miundombinu kati ya Wilaya za Mkoa wa Kagera na nchi jirani inaendelea kuboreshwa na hivyo kuwavutia wafanyabiashara mbalimbali toka nchi hizo kuleta bidhaa zao na wengine kununua mazao yetu ya Kilimo:-

(a) Je, ni hatua gani za makusudi zinachukuliwa au zinategemea kuchukuliwa na Serikali kuwapa mbinu na mafunzo wafanyabiashara walioko kwenye Wilaya za Mkoa wa Kagera zitakazowawezesha na wao kupanua masoko ya biashara katika nchi jirani badala ya kubaki watazamaji kama ilivyoanza kujitokeza hivi sasa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kuanzisha kituo cha utoaji habari za masoko na biashara katika Mji wa Bukoba ili kiweze kuwasaidia na kuwashauri wakulima na wafanyabiashara wetu na kama ni sawa, ni lini jambo hili litafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa katika kutoa mafunzo na mbinu kwa wafanyabiashara nchini, ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wa Mkoa wa Kagera. Moja ya hatua hizi ni mafunzo rasmi kwa njia ya semina, warsha na kongamano zilizofanyika mwaka 2000. Serikali, kwa kupitia Wizara na Taasisi nyingine nchini, iliendesha semina ya kuhamasisha biashara ya Samaki na kubainisha mahitaji ya soko la nje iliyofanyika Mjini Mwanza kwa Kanda ya Ziwa.

Pili, Serikali imekwisha pitisha sera ya viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ambazo zitazingatia umuhimu wa kuwafundisha wananchi mijini na vijijini mbinu za kufanya biashara. Mnamo mwaka 2002, Serikali ikishirikiana na *SIDO* ilifanya mafunzo ya walimu kutoka *SIDO* mikoa 20 kwa Tanzania Bara kwa kufundisha wananchi na wafanyabiashara kwa ujumla mbinu mbalimbali za biashara.

Wananchi na wafanyabiashara wakiwemo wa Mkoa wa Kagera watafundishwa jinsi ya kuanzisha biashara, ubora wa bidhaa zao, jinsi ya kufanya biashara kwa faida na hata jinsi ya kuandika michanganuo ya biashara. Tatu, ningependa kusisitiza pia umuhimu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara kuwahamasisha wanachama wao kushiriki katika maonyesho ya ndani na nje ili wajifunze kutoka kwa wenzao kuhusu mbinu za kisasa za kufanya biashara na nchi za nje.

(b) Serikali inaona umuhimu wa upatikanaji wa habari Mjini Bukoba hasa zinazolenga masoko ya nchi za jirani ndio maana katika sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo, Serikali kwa makusudi kabisa imeweka kwanza, mikakati maalum itakayowezesha wafanyabiashara kuzielewa kwa ufasaha sheria, taratibu na mbinu mbalimbali zinazotumika katika kuwawezesha kufikia masomo ya nje ya nchi kwa njia ya mafunzo. Pindi utekelezaji rasmi utakapoanza wadau mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara wa Bukoba watapewa mafunzo husika ili waweze kufanya biashara si na nchi jirani tu bali na nchi nyingine kwa ufanisi zaidi. Aidha, sera hii inategemea kuimarisha upatikanaji wa huduma za kuendesha biashara *(Business Development Services).*

Pili sera hiyo, ina mkakati maalum utakaowezesha kuanzisha vituo vya mawasiliano na biashara *(Business Centers)* katika sehemu mbalimbali nchini. Pindi maandalizi yatakapokamilika, utekelezaji kamili utawahusisha wadau husika pamoja na wadau kutoka Mkoa wa Kagera kuishauri sehemu za kuweka vituo hivyo na namna nzuri ya kuvianzisha.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake. Lakini kwa kuwa majibu yalikuwa ni kwa ujumla jumla na kwa kuwa Mkoa wa Kagera ndio uko pale kabisa unapambana na Mganda. Sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwatembelea wafanyabiashara wa Mkoa Kagera waweze kuzungumza nao waweze kumwambia hasa nini wanachokitaka? La kwanza.

La pili, je, Mheshimiwa Waziri anapozungumza kwamba waliwapa ushauri kuhusu Samaki lakini imetajwa kwamba wakulima ndio wanauza mazao yao. Yuko tayari vile vile kwenda kuona kwamba wananchi wana mazao mengi wanataka kuyauza kule lakini wanakataliwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza niko tayari kutembelea Mkoa Kagera na katika ratiba yangu niliyoipanga Mkoa wa Kagera ulikuwa mmojawapo ambao nitatembelea kushirikiana na uongozi wa *SIDO* kutazama ni mazao gani, biashara gani ambazo tutaweza kuwasaidia kuwahamasisha ili waweze kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, ningependa uniruhusu nitoe hili tangazo sasa hivi katika kujibu hili swali kwamba, Serikali imejiandaa mwaka 2003 na imepitishwa kwenye Bajeti, *Credit Guarantee Scheme* ambayo itasimamiwa na Benki Kuu kupitia Benki za Biashara kwa ajili ya biashara ndogo ndogo. Tutatazama na tutatembea nchi nzima kuhakikisha kwamba wananchi wameujua mfumo huu ili waweze kuzitumia hizo fedha kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ningependa kumjibu kuwa pamoja na kwamba tumeshughulika sana na mazao ya samaki lakini tunaelewa kwamba kuna mazao mengine ambayo yanahitaji msukumo, mafunzo na pia maelekezo jinsi ya kuuza pamoja na masoko. Jukumu mojawapo la kutembelea katika Mikoa hii ni kuhakikisha kuwa pia tunaweza kuwaeleza wananchi kama nilivyosema kuwaandikia michanganuo na kutazama ugumu wanaoupata katika kufanya biashara zao za maeneo yao na nchi za nje au na mikoa mingine. *(Makofi)*

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Waziri kuwa Mkoa wa Kagera umepata shida ya maafa, vita na Wakimbizi. Je, katika sera zako na kutembelea katika nchi nzima kuna Serikali inakubali kuweka umuhimu wa upendeleo maalum kwa Mkoa wa Kagera kwa sababu ya shida ambazo wamezipata kwa niaba ya nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkoa wa Kagera umepata tunaita *National Disasters* nyingi na Serikali imeanza kufuatilia na upendeleo maalum kutolewa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara tuko tayari kabisa kama nyie mko tayari kushirikiana na nanyi kuwapa upendeleo maalum. *(Makofi)*

Na. 104

**Wasimamizi wa Mirathi Kuhodhi Mali za Yatima**

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wasimamizi wa mirathi huhodhi mali za yatima kwa kisingizio kwamba wao ndio wakuu wa familia na mali zao na wakati mwingine baadhi yao hasa wanaume huwalazimisha wawaoe wajane hao kwa kisingizio kuwa wanataka kulea watoto taratibu zinazotokana na mila; na kwa kuwa wajane walio wengi huwa hawakubaliani na utaratibu huo na matokeo yake hupelekana Mahakamani ambako wakati mwingine baadhi ya Mahakimu hushirikiana na hao wasimamizi.

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo au tatizo hilo na kama inalifahamu inachukua hatua gani hasa za kisheria?

(b) Kwa kuwa baadhi ya Mahakama kutokana na sababu moja au nyingine huchelewesha kutoa hukumu za kesi za aina hiyo na hivyo walengwa yaani wajane na watoto kuendelea kusumbuka; je, ni Mahakimu wangapi ambao wamewajibishwa kwa tuhuma hizo na ni Wilaya na Mikoa ipi?

(c) Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuweka kiwango cha muda wa kuendesha kesi kama hizo ili zisiendelee kuwatia uchungu wafiwa na gharama mbalimbali za kwenda na kurudi Mahakamani na hatimaye kukata tamaa?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kupitia taarifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na taarifa ya utafiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Serikali inalifahamu tatizo la wasimamizi wa mirathi na ndugu wengine wa marehemu kuhodhi mali ya marehemu na hivyo kuwanyima yatima stahili zao. Tume ya Kurekebisha Sheria ilitoa mapendekezo ya kukabili tatizo hilo likiwemo la kukifanya kuwa kosa la jinai, kitendo cha mtu yeyote kunyang'anya au kuhodhi mali ya marehemu. Tume na tunarajia katika muda muafaka itaweza kuwasilisha Bungeni hapa Muswada wa kuzifanyia marekebisho ya sheria kuhusu masuala ya mirathi. Hata hivyo, kama Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, anayo taarifa ya tukio mahsusi, naomba anipatie ili ziweze kuyafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria.

(b) Baada ya shauri la mirathi kufunguliwa Mahakamani, hutolewa matangazo katika mbao za matangazo na magazetini. Iwapo hakuna pingamizi lolote, msimamizi huteuliwa mara moja. Katika mazingira hayo hauwezi kuwepo ucheleweshaji wowote. Ucheleweshaji hujitokeza pale panapokuwepo pingamizi kwa kuwa hulazimu kuwepo usikilizaji wa pingamizi hizo. Muda wa usikilizaji hutofautiana kuzingatia pingamizi zinazotolewa. Kwa mujibu wa Mkataba baina ya Mahakama na Wateja, hukumu inatakiwa kutolewa ndani ya siku 60 tangu kumalizika usikilizaji. Hazipo kumbukumbu za Mahakimu waliowajibishwa kwa tuhuma za aina iliyozungumziwa na Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi.

(c) Kama nilivyoeleza, ucheleweshaji wowote hutokea pale panapokuwepo pingamizi kutoka kwa wanandugu. Kwa kuwa ni haki ya Kikatiba na Kisheria kwa mtu kuwasilisha Mahakamani pingamizi au lalamiko lake lolote kwa nia ya kutolewa uamuzi wa Mahakama, Serikali haina uwezo wowote wa kuzuia pingamizi hizo zisiwasilishwe. Hivyo, ni vigumu kuweka muda maalum wa kusikiliza Mashauri ya mirathi au Mashauri mengine yoyote.

**MHE. HADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya Mahakimu, Wasimamizi wa Mirathi na familia husika wanaendelea kutowatendea haki wanawake na watoto wajane; je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka ofisi za kushughulikia kesi za mirathi katika kila Wilaya?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, matatizo haya tunayo, ni mengi na makubwa ndiyo maana tukaiomba Tume ya Kurekebisha Sheria kuliangalia suala hili na kwa sasa hivi tuko katika hatua ya kuandaa Muswada baada ya Serikali kukubali mapendekezo kuhusu matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kusema kwamba, utaratibu wa kimahakama upo, kwa hiyo, sioni kama utakuwa umetatua tatizo hili kama utaweka Maofisa ambao watakuwa wanashughulikia masuala haya. Zipo Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama za Mikoa mpaka Mahakama ya Rufaa kuweza kushughulikia matatizo hayo. Kwa hiyo, tutumie utaratibu tulionao sasa hivi. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala la mirathi limekuwa ni tatizo kubwa na ni la muda mrefu; je, ni lini Serikali italeta marekebisho hayo Bungeni ili Sheria ianze kutumika na Wananchi waanze kuneemeka na Sheria hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, suala hili tumelifanyia kazi sana na kwa karibu sana na akinamama kwa kupitia Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Waoto; Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na sasa hivi tunangoja kwenda Serikalini na mapendekezo yako tayari. Ni mategemeo yetu kwamba tukifanikiwa katika hatua hizo zote tunaweza kuusoma Muswada huo kwa Mara ya Kwanza katika kipindi hiki cha Bunge. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika swali mama lililoulizwa na Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, lilizungumzia kuhusu wanaume kulazimisha kuwaoa wajane; Mheshimiwa Waziri katika jibu lake hakueleza suala hilo na wakati huo huo Mheshimiwa Waziri alimwambia Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, kama anayo kesi mahsusi ampelekee; je, Mheshimiwa Waziri ataweza kuwatenganisha hao wajane ambao wamekwishaolewa na wanaume hao? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza swali la msingi lilihusu wasimamizi wa mirathi kuhodhi mali za yatima. Pamoja na kuwa suala hili liliongezwa humo, lakini halikuhusu suala la wanaume kuwalazimisha wawaoe wajane, lakini napenda kusema kwamba, hii imekuwa ni mila katika baadhi ya makabila yetu hapa nchini kwa wajane hao kuolewa na shemeji zao. Hii ni mila potofu na ni lazima tuondokane nayo.

Niliwahi kusema hapa Bungeni kwamba, sitegemei mdogo wangu Balozi Juma Mwapachu, ambaye anasubiri subiri nife amuoe Shilla. Kwa kweli hizi ni mila potofu na ni lazima tuondokane nazo. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 106

**Ushirikiano wa Nguzo Tatu za Dola katika kutatua Kero za Wananchi**

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, ameomba swali lake namba 105 lisijibiwe leo, naheshimu uamuzi wake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba unaweza kwenda kupumzika. Sasa tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 106

**Mikataba ya Mkampuni ya Uchimbaji Madini**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD (k. n. y. MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHANI)** aliuliza: -

Kwa kuwa wananchi wamekuwa hawaridhishwi na kipato cha Serikali kinachotokana na madini yanayochimbwa na Makampuni mbalimbali hapa nchini kinyume na ilivyotarajiwa:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuangalia upya mikataba iliyowekeana na Makampuni yanayochimba madini kwa lengo la kuangalia upya kiasi ambacho Serikali inapata na kuona uwezekano wa kukiongeza?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakati sasa umefika wa kuandaa mapendekezo mapya ya mikataba ya kuileta Bungeni ili Wabunge wapate nafasi ya kutoa maoni yao kwa uwazi na ukweli kabla ya kuwakaribisha wawekezaji wapya, hali ambayo siyo tu itaondoa manung'uniko bali kuwaweka Wabunge na Serikali yao karibu zaidi na jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abrahman Ramadhani; Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, mikataba kati ya Serikali na Makampuni ya Madini inaweza kuangaliwa upya kwa ridhaa ya pande zote zinazohusika na mikataba hiyo na kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa chini ya mikataba hiyo.

Hata hivyo, naomba kulieleza Bunge kuwa, mikataba hiyo haihusu moja kwa moja viwango vya kodi, bali inalenga zaidi katika kuyakinga Makampuni ya Madini na athari ambazo zinaweza kujitokeza iwapo kodi zinabadilishwa mara kwa mara wakati wa uhai wa mikataba hiyo. Makampuni ya Madini yanalipa kodi kwa kuzingatia mfumo wa kodi ulioko kwenye Sheria. Sheria kuu inayohusika ni *The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Act. No. 27 of 1997* ambayo ndiyo inaweza kuangaliwa upya na Bunge hili kwa madhumuni ya kujiridhisha kama kuna haja ya kurekebisha viwango vya kodi vilivyopo. Madhumuni ya viwango vya kodi vilivyopo ni kuweka uwiano mzuri kati ya maslahi ya Taifa letu na mahitaji muhimu ya wawekezaji katika Sekta ya Madini.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 63(3)(e) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge linaweza kujadili na kuridhia mikataba yote kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi zingine ambayo, kwa masharti yake, inahitaji kuridhiwa. Mikataba kati ya Serikali na Makampuni ya Madini ni tofauti. Kikatiba, kulingana na mgawanyo wa madaraka kati ya Bunge, Serikali na Mahakama, Mikataba ya Madini ni ya kiutendaji *(Executive actions of the Government)*. *(Makofi)*

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Katika Mikataba kuna baadhi ya ahadi ambazo zinatolewa na wawekezaji ili kusaidia maeneo husika na katika Mkataba wa *Geita Gold Mine* inasemekana kuna dola 200,000 ambazo zinatakiwa zitolewe kwa ajili ya kusaidia Halmashauri ya Geita.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Serikali kutokuwa wazi na kutoonyesha kilichomo kwenye Mikataba ni kuendelea kuwanyima haki wale wananchi wanaozunguka maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna kinachofichwa na Serikali kuhusu Mikataba kwa maana ya maslahi ya mtu yeyote yule au kikundi chochote kile.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, taarifa aliyoitoa kuwa katika mkataba huo kuna kipengele kinachotakiwa Kampuni ya Madini ya Geita ilipe Halmashauri si taarifa ya kweli.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kampuni hizi za Madini ikiwemo hii ya Geita zimekuwa zikifanya kazi kubwa ya kusaidia maeneo ambamo hizi Kampuni zipo katika miradi ya maendeleo ya jamii na tumewahi kutoa takwimu hapa Bungeni ya miradi mbalimbali ambayo imekuwa ikitolewa misaada ama kupitia kwa Halmashauri au moja kwa moja kwa Makampuni haya ambayo yamekuwa yakifanya kazi katika maeneo haya na tuko tayari kutoa tena takwimu hizo kwa Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa inaonyesha wazi kwamba Serikali imekuwa ikipata kigugumizi kusema ukweli kuhusu haya madini. Ni kwa nini sasa Serikali isikae pamoja na Wabunge wazungumze jambo hili kuliko kila siku kupata tabu ya kujibu maswali hayo hapa ndani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali haijawa na kigugumizi na haina kigugumizi kwenye suala hili. Sisi kama Serikali na kama Wizara inayohusika tunajua tunawajibika kwenye Kamati ya Bunge

inayohusika na tumekuwa tukitoa na tunaweza tukatoa taarifa kwenye Kamati ya Bunge kuhusu masuala mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge watapenda kuyafahamu.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kama tunavyofahamu, uwekezaji huu wa katika migodi ya madini ni uwekezaji wenye gharama kubwa. Kwa mfano, Mgodi wa Nzega peke yake ni shilingi bilioni 68. Mradi wa Geita ni shilingi bilioni 165 na mgodi wa Bulyanhulu ni shilingi bilioni 280 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika migodi hii ni sera yetu ya ndani na pia ni sera yetu ya nje kwa maana ya kuwaita wawekezaji na unatawaliwa na Sheria zetu na pia matarajio ya Kimataifa kuhusu suala zima la uwekezaji. Lakini uwekezaji ambao unatokea wakati huu wa dunia ya utandawazi ambapo wawekezaji hawa kwanza wanashindana wenyewe kwa wenyewe, lakini pia na nchi zinashindana katika kuhakikisha kwamba tunavutia wawekezaji. Uwekezaji huu unahusu kuvutia vitega uchumi katika dunia hii ya utandawazi na hao wenye mitaji mikubwa wanaangalia mambo mbalimbali katika nchi ambazo wanakwenda kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati tunayo haki ya kujua na kujiuliza kama Taifa letu linafaidika vya kutosha kuhusu raslimali zetu, lakini pia tunawajibika kuendelea kuihakikishia dunia kuwa Tanzania inakaribisha wawekezaji, ni tulivu, ina sera tulivu na inaheshimu Mikataba inayoingia na wawekezaji. *(Makofi)*

Na. 107

**Fidia kwa Wananchi wa Maeneo ya Mgodi wa *Geita Gold Mining***

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza: -

Kwa kuwa baadhi ya wananchi waliokuwa wakikaa kwenye maeneo ya Mgodi wa *Geita Gold Mining Ltd* hawajalipwa fidia ya mazao yao na kwa kuwa Wananchi hao wamekuwa wakifuatilia kupata ufumbuzi wa madai yao bila mafanikio na kwa kuwa Serikali katika kutaka kuwaridhisha Wananchi hao imeunda Tume ambazo zimeshindwa kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu fidia ya wananchi hao wasiokuwa na makosa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati wa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliokuwa wanakaa katika maeneo ambayo yalichukuliwa na Kampuni ya *Geita Gold*

*Mining Ltd* kwa ajili ya kufungua mgodi, baadhi ya wananchi hawakulipwa fidia hiyo na waliwasilisha malalamiko yao Serikalini.

Kufuatia malalamiko hayo Serikali iliunda Tume ambayo iliongozwa na Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* Mwanza kwa ajili ya kuchunguza malalamiko hayo. Tume ilifanya uchunguzi na kuwasilisha taarifa yake Serikalini na taarifa hiyo ilipitiwa na Viongozi wa Serikali pamoja na uongozi wa Mgodi wa Geita.

Katika taarifa yake, Tume ilibainisha kuwa ni kweli kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa fidia pamoja na kwamba Mgodi wa Geita ulikwishatoa fedha yote iliyotakiwa ambayo ni Shilingi bilioni 3.8. Tume ilitoa taarifa kwamba kilichosababisha baadhi ya wananchi kutokulipwa fidia ni baadhi ya Watumishi wa Serikali, Watumishi wa Mgodi wa Geita na baadhi ya wananchi na Viongozi wao wa Vijiji kukiuka taratibu za utoaji fidia ama kwa uzembe au kwa makusudi.

Uongozi wa Mgodi wa Geita ulikwishawafukuza kazi watumishi wake ambao walibainika kutokuwa waaminifu wakati wa ulipaji fidia. Kwa upande wa Serikali, baada ya kupokea taarifa ya Tume, Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* ilianza uchunguzi ambao bado unaendelea. Uchunguzi huo ukikamilika watakaothibitika kuwa walijihusisha na vitendo vya rushwa au wizi watachukuliwa hatua za kisheria.

Baada ya uchunguzi Serikali itahakikisha kwamba wananchi wote ambao wana madai halali watalipwa. Kwa sasa Wananchi wenye madai halali wanaombwa wawe na subira kidogo wakati *PCB* inakamilisha kazi hii ya uchunguzi.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inakubali kwamba hawa wananchi ambao hawajalipwa wanazidi kuteseka na kutokuwa na imani na Serikali yao na kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba angeweza kushughulikia masuala haya na wananchi wale wakalipwa.

(a) Je, kati ya Wizara na Mheshimiwa Rais, mkubwa ni nani?

(b) Kwa kuwa wakati tunakuja huku wananchi waliandamana wakitaka kurudi katika maeneo yao na wakataka mgodi usitishe shughuli za uchimbaji ili warudi huko. Je, Serikali itaniruhusu ili nami nikawaruhusu waingie katika eneo lile? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ahadi ya Serikali kwamba wananchi ambao wana haki halali watalipwa bado iko pale pale.

Mheshimiwa Spika, pili, kama tutamruhusu Mheshimiwa Mbunge aende akawaambie wananchi warudi pale pale, nadhani kazi ya Mheshimiwa Mbunge siyo kufanya fujo au kupeleka watu waende wakafanye fujo! Napenda kumshauri

Mheshimiwa Mbunge kwamba, hiyo siyo kazi ambayo tungemtegemea yeye kama Kiongozi wa Umma aende akafanye shughuli kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu uzito wa suala hili na tunafahamu pia kwamba kuna baadhi ya wanasiasa wanalitumia suala hili katika kuwakandamiza Waheshimiwa Wabunge wa maeneo yale, lakini napenda nichukue nafasi hii kuwafahamisha wananchi wa Geita wanaohusika na suala hili, kwa kweli hili ni suala ambalo liko mikononi mwa Serikali na wasidanganywe na watu wachache wanaokwenda kule kwa mintaarafu ya kuwakandamiza Waheshimiwa Wabunge halali waliowachagua kwamba eti wao ndiyo wanaohusika na suala hili. Hili ni suala ambalo liko ndani ya mikono ya Serikali na tutalishughulikia kwa juhudi zote. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna wananchi wenye madai halali ambao hawajalipwa na sasa ni zaidi ya miaka minne na kwa kuwa wananchi hao wanaishi kwa shida sana wakiomba omba na kukopa.

Je, sasa Serikali itakuwa tayari kuwalipa wananchi hao pamoja na fidia za kujikimu, usumbufu na riba kwa miaka yote ambayo imekuwa ikishikiliwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi nilieleza kwamba, Serikali inafahamu umuhimu wa wananchi hawa kulipwa na taabu ambayo wananchi hawa wamekuwa wakiipata na ndiyo maana nimesema kwamba, tunalishughulikia suala hili ili kuhakikisha kwamba matatizo yalijitokeza wakati huu ambayo mengi kama nilivyosema katika jibu la awali, yalisababishwa na baadhi ya Viongozi wao katika maeneo yao ya Vijiji na baadhi ya wananchi wasiokuwa waaminifu hayajitokezi tena.

Na. 108

**Upungufu Mkubwa wa Maji Nchini**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza: -

Kwa kuwa mvua zimepungua sana katika maeneo mengi ya nchi yetu na kusababisha upungufu mkubwa wa maji kwa wananchi na mifugo na kwa kuwa suala la upungufu wa maji lilijadiliwa katika Mkutano wa Johannesburg na kuwekewa mkakati wa Kidunia na kukabiliana na tatizo hilo.

(a) Je, Serikali ya Tanzania imeandaa mikakati gani ya kukabiliana na tatizo hilo la Kitaifa?

(b) Je, Serikali imebaini maeneo gani ambayo *rate* ya kupungua kwa maji ni kubwa sana na kuwa na mikakati ya kusaidia maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) k. n. y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imejipangia mikakati mbalimbali inayolenga kukabiliana na upungufu wa maji ili kupunguza idadi ya watu wasiopata huduma za maji kufikia nusu ifikapo mwaka 2015. Mikakati hiyo inalenga kuweka mfumo na uwiano mzuri wa usimamizi wa raslimali ya maji nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na: -

(i) Kutambua maeneo yenye matatizo ya maji na kupanga mbinu na mikakati ya kukabiliana nayo.

(ii) Kuendeleza na kutekeleza mipango ya kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji.

(iii) Kuandaa mikakati na programu za Kitaifa kwa ajili ya kusimamia kwa pamoja matumizi endelevu ya raslimali za maji.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Serikali inayo mikakati ya kujenga miradi mipya na kukarabati ile isiyofanya kazi ili kuwapatia wananchi majisafi katika maeneo yasiyokuwa na maji; kuimarisha mitandao ya kupima ubora wa maji ili kuhakikisha kwamba wananchi na mifugo wanapata maji yenye ubora unaofaa; kuanzisha miradi maalum ya maji katika maeneo kame na kufanya mapitio ya Sheria za maji na kuimarisha miundo ya utekelezaji na usimamizi wa Vyombo vya usambazaji maji.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imebaini maeneo ambayo kasi ya kupungua kwa maji ni kubwa. Maeneo hayo kame ambayo hupata mvua kidogo na kwa vipindi vifupi ni pamoja na Mikoa ya Singida, Dodoma, Shinyanga na sehemu ya Mkoa wa Manyara. Maeneo mengine ni Mikoa ya Tabora, Pwani, Lindi sehemu ya Arusha na Kilimanjaro.

Ili kupunguza makali ya tatizo hili, Serikali inayo mikakati ya kujenga mabwawa, malambo na visima vya maji Vijijini, kuwahamasisha na kutoa elimu kwa Wananchi na wadau mbalimbali waishio katika maeneo kame, kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua na kujumuisha mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo kwenye usanifu wa miradi ya maji.

Aidha, baada ya Serikali kupitisha Sera ya Maji, Julai 2002, Wizara yangu inaandaa mikakati na programu ya Kitaifa kwa ajili ya kusimamia kwa pamoja matumizi endelevu ya raslimali za maji na pia itaendeleza na kutekeleza mipango ya kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na uharibifu wa mazingira.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa hakutaja Wilaya ya Chunya, wakati najua kwamba Wilaya hiyo ni moja katika maeneo ambayo maji yake yanapungua kwa haraka sana kutokana na mito na vijito kukauka maji mapema kuliko ilivyokuwa siku za nyuma; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari au Serikali ina mkakati gani wa kusaidia Wilaya ya Chunya kujipatia malambo ya maji ili kujikinga na tatizo la upungufu wa maji ambao unatarajiwa kutokea?

(b) Kwa sababu hali ya ukame haiwezi kutusubiri; je, huo mkakati wa Kitaifa ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumzia unatarajiwa kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k. n. y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Chunya ni mojawapo ya Wilaya zenye upungufu mkubwa wa maji, lakini sikuwa nataja Wilaya bali nilikuwa nataja Mikoa. Nimesema kwamba, baadhi ya maeneo ambayo yana upungufu ni pamoja na niliyoyataja, lakini binafsi nilitembelea Wilaya ya Chunya wakati nikiwa katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na kweli tatizo ni kubwa. Nilishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuandaa mikakati ambayo bado inaendelezwa katika Wizara na baadhi yake iko kwenye Bajeti na tumeishatekeleza baadhi ya mambo ambayo tuliyafanyia kazi wakati nilipofanya ziara ikiwa ni pamoja na kuchimba malambo kwa ajili ya mifugo.

Pia, kuna timu ambayo ilikwenda kule kufanya tathmini na kufanya usanifu wa maeneo ambayo yatachimbwa mabwawa hayo na ninaamini kwamba Halmashauri itakuwa imeingiza kwenye Bajeti ya mwaka 2003 kwa kushirikiana na Mkoa pamoja na Wizara. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuwasiliana ili kuona kipi kifanyike sasa hivi kama *priority* na vitu gani vifanyike katika miaka inayofuata.

(b) Mikakati ya Kitaifa ya kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji ilizungumziwa katika Mkutano wa Johannesburg na ikawekwa mikakati ya kushughulika na suala hilo. Kimataifa mikutano mbalimbali ngazi ya Mawaziri wa Maji imefanyika huko Marrakech, Morocco mwaka 1997, The Hague, Uholanzi mwaka 2000 na mwaka 2003 huko Kyoto - Japan. Mkutano huu wa Kyoto - Japan ambao umefanyika mwaka huu ulikuwa unafuatilia utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Johannesburg.

Katika sura ya 18 ya *agenda* ya 21 ya Mkutano wa Johannesburg ulitambua wazi umuhimu wa maji kama msingi madhubuti wa maendeleo endelevu. Tanzania imeshiriki katika mikutano yote hiyo na kuahidi kutekeleza na kufanikisha malengo ya mikakati iliyowekwa na Jumuiya ya Kimataifa katika kukabiliana na matatizo ya maji. Mwaka 2002 Wizara au Serikali ilipitisha Sera ya Maji ambayo ndiyo hasa inatekelezwa hadi hivi sasa.

Na. 109

**Mradi wa Maji - Mwamashele na Mwamanota**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza: -

Kwa kuwa Mradi wa Maji wa Mwamashele na Mwamanota uliharibika kwa kipindi kirefu na sasa hautoi huduma ya maji kwa Wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuufufua mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k. n. y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo: -

Mradi wa Maji wa Mwamashele/Mwamanota ulijengwa na kukamilika mwaka 1972/1973. Mradi unahudumia Vijiji vya Mwamashele, Busongo na Mwamanota ukiwa na matanki matatu ya maji (tanki moja kwa kila Kijiji).

Mheshimiwa Spika, mradi huo ulisimama kufanya kazi miaka 10 iliyopita baada ya Serikali kuwa na uwezo mdogo wa kugharamia uendeshaji wake.

Kwa kuwa wananchi hawakushirikishwa kikamilifu tangu awali katika kuendesha, kulinda na kutunza mradi huo matokeo yake yalikuwa ni kuibiwa kwa mashine ya kusukuma maji, madirisha na paa za nyumba ya mashine *(Pump House).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1980 Halmashauri ya Wilaya na Serikali ya Uholanzi ilikuwa tayari kufufua mradi huu kama wananchi wangechangia fedha au nguvu kwa ajili ya ukarabati. Kwa bahati mbaya wananchi hao hawakuhamasishwa kuweza kupata mchango huo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Shinyanga, Serikali inatekeleza mpango wa usambazaji wa maji Vijijini kwa msaada wa jumla ya shilingi bilioni 8.3 kutoka Serikali ya Uholanzi. Mpango huu unagharamia miradi ambayo Wananchi wenyewe wako tayari kushiriki kuchangia na kumiliki.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huu, kila Halmashauri ya Wilaya au Manispaa inatekeleza miradi yenye thamani ya wastani wa shilingi milioni 155 kila mwaka. Kiasi hiki kinaweza kuongezeka kama wananchi wengi zaidi wataandaa miradi na kuiwasilisha Wilayani.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Mwamashele/Mwamanota ambao ukarabati wake umekadiriwa kugharimu shilingi milioni 42, unaweza ukafufuliwa chini ya mpango huu kama Wananchi wa maeneo hayo watatimiza taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na uongozi wa Wilaya ili waweke utaratibu wa kufufua mradi huu chini ya mpango unaotekelezwa hivi sasa.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, katika maelezo yake amesema kwamba mradi huu ulikwama kufufuliwa kwa sababu ya wananchi kutokuhamasishwa ili waweze kuchangia gharama za mradi huu. Kwa kuwa sasa wananchi hao tumeshawahamasisha na wako tayari kugharamia nusu ya gharama ya mradi, je, Serikali itakuwa tayari kuwaunga mkono kuchangia ili kukumilisha mradi huu uweze kufanya kazi zake kama inavyotazamiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k. n. y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, kama ifuatavyo:-

Programu ya maji vijijini na usafi wa mazingira Mkoani Shinyanga kutaka jamii ichangie kiasi cha asilimia 5, Halmashauri kuchangia asilimia 5 na mradi wenyewe utachangia asilimia 90 kwa mradi wa maji na matumizi ya nyumba. Lengo la programu ni kufufua angalau mradi mmoja wa maji ya bomba kila mwaka. Programu hii itakuwepo Mkoani Shinyanga hadi mwaka 2006, kama nilivyosema zimetengwa shilingi bilioni 8.3 kwa ajili ya shughuli hii. Kwa sasa timu ya wahamasishaji iko vijijini kuitangaza programu hii, Mwamashele na Mwamanota ni moja ya vijiji vilivyoko katika Wilaya ya Shinyanga Vijijini, ambako programu inatoa huduma zake.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Mwamanota na Mwamashele, ikiwa sehemu ya Wilaya hiyo kwamba kama wao watachangia hizo asilimia 5 na Halmashauri ichangie asilimia 5, uhakika wa kutekelezwa mradi upo. Ni juu yao kuonyesha kwamba wana tatizo la maji na kwamba wanataka wapatiwe maji basi watoe mchango wao wa asilimia 5 na nguvu ambayo inatakiwa na Halmashauri nayo ichangie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali vile vile umekwisha. Kuna tangazo moja tu la Kikao cha Kamati, Mheshimiwa Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wakutane leo saa tano asubuhi hii katika chumba namba 54.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004
### Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo. Ninachowashauri ili muweze kufanya vizuri Bungeni, angalau someni mara moja kwa mwezi Kanuni za Bunge, la pili, angalau kwa miezi miwili someni mara moja Katiba ya Nchi na tatu ninawashauri kila karatasi, kitabu au matangazo yanatolewa katika Bunge muwe mnayosama msiache pale kwenye *pigeon holes,* mtakuwa wachangiaji wazuri na hamtasumbuliwa na sheria.

Baada ya kusema hayo naomba pia niipongeze Serikali kwani nimetumwa na baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Pwani kuipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo na wanasema wanaishauri Serikali kero yoyote ya wananchi inapotokea basi Serikali iweze kulishughulikia haraka haraka. Kodi ilikuwa ni kero kwao na walichokiona katika Bajeti hii kikubwa kabisa kilichofanyiwa kazi na Serikali ni kufuta kodi ya maendeleo. Wanashauri kwamba wanaomba Wizara ya Fedha itazame aina zote za Kodi izioanishe kisha iseme hizi ni za Serikali Kuu na hizi ni za Halmashauri ili Halmashauri zitatazama katika kodi zilizoonyesha kama zinawafaa katika Halmashauri zao na zisizowafaa wanaweza kuacha na pale wanapoona wanahitaji kodi nyingine basi wanaomba wapeleke ushauri ule kwa Wizara ya Fedha ili waone kodi zile zinafaa au hazifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ni maombi kwa sababu imewahi kujitokeza linatangazwa jambo kwenye Bunge, lakini kuna baadhi ya Halmashauri zinasema kwa sababu imezungumzwa ndani ya Bunge na hatujapewa barua hatutekelezi. Natoa mfano niliuliza swali la nyongeza humu Bungeni nilimwuliza Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu 10% na akazungumzia, 10% iko pale pale alipunguza tu kwa wale ambao walikamilisha 10% ndiyo watoe 5%. Nilipokwenda kwenye Halmashauri yangu ambayo ni Mji Mdogo Kibaha walisema hivi, sisi hatuwezi kusikiliza jambo linalotangazwa ndani ya Bunge. Tunaomba Waziri aandike barua. Sasa Waziri utaamua kuandika barua au kutangaza hapa Bungeni. Kwa hiyo na mimi nina wasiwasi kufutwa kodi ya maendeleo iliyotangazwa ndani ya Bajeti. Halmashauri zinaweza kukataa kama hii ya kwangu Mji Mdogo Kibaha naomba muwaandikie barua haraka la sivyo wataendelea kuwatoza hiyo kodi. Huo ulikuwa ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Maili Moja. Kanuni ya 49 (vii) inaniambia kwamba kama una *vested interest* lazima utangaze. Naomba kusema hili suala la Maili Moja ninatangaza kwa sababu nahusika, hili ninalozungumza hapa linanihusu mwenyewe na mimi nina biashara pale Maili Moja ambayo nimedhalilika pia.

Mheshimiwa Spika, si kawaida yangu suala linalohusu Mkoa wangu kuja kulisema Bungeni. Lakini baada ya kuwasiliana na wakubwa wao wenyewe wakaniambia nenda kaseme Bungeni. Kwa hiyo, nakuja kulisema baada ya wao kunishauri.

Mheshimiwa Spika, *stand* ya Maili Moja ilianza miaka ya themanini wakati Kijiji cha Maili Moja ambayo ni *shunt town* walipoona wananchi wamepata *accident* baada ya basi kusimama barabarani na kupata ajali kwa sababu kulikuwa hakuna *stand,* halafu likaja *semi trailer* likalisukuma basi na robo tatu ya abiria wakafariki dunia. Wakati huo

nyoyo za watu zilikuwa nzuri wakiona majeruhi wanashughulikia vizuri, walipomaliza kushughulikia majeruhi wale wakapiga mbiu ya mgambo na kuomba wananchi wa Kijiji cha Maili Moja ambacho ni *shunt town* wakasema jamani tutafute *stand* ama sivyo tutamalizika. Wananchi wale wa Kijiji cha Maili Moja walikubaliana, katika kukubaliana wakaona eneo la Maili Moja linafaa wakaamua kusambaza kichuguu kwa sababu lilikuwa na kichuguu na *stand* ile ikaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, *stand* ile ilianza kwa nia kwamba mabasi yakitaka kusimama basi yasimame kwa kuingia kule ndani ili watu wasije wakafa kama ilivyotokea ajali hiyo. Lakini jinsi siku zilivyokuwa zinakwenda Halmashauri ikasema kuna haja ya kusaidia kutengeneza *stand* hii vizuri ili iwe *stand* yenye hadhi, Halmashauri ikashughulikia hilo. Shida ikaanzia hapo, Halmashauri iliposhughulikia hela zilizotumika sehemu fulani ya hela zililiwa na Halmashauri wakasema *contractor* amefanya kazi kumbe hakufanya kazi. Nina ushahidi na nikipewa nafasi nitatoa *minutes* zote za kikao cha Halmashauri ambacho nilisema kitu fulani hakikufanyika na wakakubaliana wakasema hilo suala tutalizungumza baadaye mpaka leo halijazungumzwa.

Baada ya hapo kukatokea ugomvi kati ya Halmashauri na Mji Mdogo kila mtu anaitaka ile *stand* kwa sababu ina pesa. Ukatokea mvutano mkubwa. Mimi ni mmoja wa Madiwani walioshawishika kuomba Mji Mdogo uwe na *stand* yake kwa sababu iko ndani ya Mji Mdogo. *Stand* ile ikachukuliwa na Mji Mdogo kwa nia nzuri tu kwamba sasa angalau tupate kipato.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi Stendi ya Maili Moja imekuwa ni kero kwa wananchi, imefika wakati *stand* ya Maili Moja inawanyima haki za binadamu wananchi.

Mheshimiwa Spika, niliambiwa na madreva wa teksi juu ya manyanyaso wanayopata. Nimesema nina *vested interest* kwa sababu na mimi pia nina teksi. Madreva wakanifuata wakaniambia tananyanyaswa (Mheshimiwa Mbunge), nikawauliza mnanyanyaswa namna gani? Wakasema tunatakiwa kulipia kila tukipata na abiria tunatoa shilingi 200. Kwa siku tunatoa kati ya shilingi 2000 mpaka shilingi 3000, sasa zidisha kwa mwezi na wenye daladala kwa *trip* zao kwa siku kama ile ya mia mbili mbili kwa *taxi* wanatakiwa kutoa shilingi 1600 kila siku. Lakini inapotokea kama siku hiyo una matatizo hukufanya kazi unaambiwa lazima ulipe na usipolipa kasheshe inatokea kwako.

Eneo lile limepewa *agent,* mtu atakayekusanya mapato ya *stand* ya Maili Moja. Kampuni inaitwa *Salu Investment. Salu investment* alichofanya kashawishi askari polisi wengi kati yao wanashinda *stand* ya Maili Moja. Pale dreva yeyote asipotoa chochote kwa hawa askari kinachofanyika ni kumkamata na kumtia ndani bila kumfungulia kesi na wakimweka ndani wanasema una mawili ya kuchagua umpe askari chochote, ukishindwa kumpa askari chochote wanakwenda kuzungumza na Salu na kumwambia kuwa sema kuwa hajalipa kodi ya *stand.* Matokeo yake utalazimika kutoa shilingi 10,000/=, kama hutaki kukaa ndani. Salu anakupa risiti kwamba wewe ulishindwa kulipa unapewa risiti. Shilingi 10,000/= wanagawana askari na *agent* wao. Sasa hivi askari wengi wanashinda *stand* ya Maili Moja.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba kuuliza, najua askari si wengi nchini. Nimeona *City Council Dar es Salaam* wao wanachofanya wana askari wao, lakini kwa Wilaya ya Kibaha kwa maana ya Mji Mdogo huyu Salu ameweza kuwachukua askari polisi kuwa wao ndiyo walinde pale. Sasa naomba niulize ikiwa Mkuu wa Wilaya tu hana askari polisi wa kumlinda, je, huyu Salu ni nani?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaambiwa na madreva siamini, sasa Mungu siku moja akasema litakutokea wewe mwenyewe. Mimi nilisafiri kwenda nje ya nchi, nikamwomba dreva wangu, kwamba chukua teksi hii kamchukue mtoto wangu anakuja kwa ndege kesho kwenye saa moja asubuhi, kwa bahati mbaya ile ndege ilikuwa *cancelled* ikaja usiku, dreva akalazimika kubaki Dar es Salaam kwa sababu hana mafuta ya kutosha. Siku ya pili amefika *stand* akafuatwa na askari, akaambiwa wewe jana hukulipa na leo hujalipa. Akasema leo hii ni saa mbili risiti hii nimetoka mara moja nimelipa na jana sikuweko nilikwenda kumchukua mtoto wa mama. Wakasema una mawili utoe chochote ama sivyo utakwenda ndani.

Mheshimiwa Spika, dreva akasema sitaki kutoa rushwa, matokeo yake akachukuliwa akatiwa ndani. Mtoto wangu ametoka nyumbani alipofika Maili Moja alikuwa anamtaka huyo dreva waende Dar es Salaam kulikuwa na harusi, matokeo yake akaambiwa dreva wako ametiwa ndani. Akaenda kituo cha polisi, akauliza imekuwaje dreva ametiwa ndani? Wakasema hajalipa ushuru wa teksi jana, akasema mbona jana alikuwa ananishughulikia mimi nilikuwa nimetoka safari, wakamkatalia. Wakasema msubiri afande aliyemweka ndani maana hata kesi haijafunguliwa, akamsubiri mpaka saa sita kuanzia saa tatu. Ilipofika saa sita mchana ndiyo afande kaja akasema twende kwa Salu, wakaenda ofisini kwa Salu, akasema wewe itabidi ulipe, akasema nilipe kwa nini na dreva hakuwepo jana?

Wakambishia wakaanza kumtukana matusi na kumwambia mtoto wangu malaya. Huyu mtoto anasoma, muda wake wote amesoma shule za *Mission,* Tosamaganga na watu wengine wanamjua, kaambiwa malaya na usilinge na hicho kimama chako malaya kinajidai daktari kilifanya kazi ya udaktari wapi? Mtoto alinyanyaswa aliaanza kulia, wakasema lete shilingi 10,000/= au siyo na wewe tutakutia ndani. Alichofanya akatoa shilingi 10,000/= akawapa, wakapokea. Yeye karudi polisi akasema nataka nifungue kesi nimedhalilishwa kijinsia, polisi wakasema hatukufungulii kesi.

Huyo mtoto hakuamini kwa sababu hajasikia hata siku moja mama yake anatukanwa hadharani ilimu-*affect mentally.* Niliporudi kutoka safari ya *South Korea* akaniambia yaliyowatokea, sikuamini, nilichoamua ni kwenda kumwona askari mhusika, akasema ndiyo tumemtia ndani, nimekwenda kwenye kituo cha polisi akasema ndiyo tulimtia ndani bila kufunguliwa kesi. Nimekwenda kwa Salu akasema ndiyo tumemtia ndani nenda Mahakamani.

Niliamua kwenda kwa wakubwa kwa sababu huwa sipendi kuja kusema Bungeni, wakubwa wakasema wewe si Mbunge, nenda Bungeni kawaambie wakubwa, nikawauliza wakubwa gani? Wakasema utamwambia Waziri mhusika au Naibu.

Nikasema mimi niende Bungeni huoni kuwa nimedhalilishwa na askari ambao wananipenda.

Mimi nilikuwa kocha wao wa *netball,* mimi ni kipenzi chao, nilipokuwa nafanya kazi askari wengi walikuwa wananifuata kwenye *postmortem* na shughuli za kawaida, askari walikuwa wananifuata hata saa 8 za usiku. Akasema wewe nenda.

Sasa mimi naomba kusema kwamba Polisi wa *stand* Maili Moja wanadhalilisha na nasema Halmashauri imemng'ang'ania huyu Salu ambaye alidhalilisha Tawi la Maili Moja kusababisha watu wakawa *corrupt,* watu wakaamua kuoa, watu wakaamua kuwa walevi mpaka mimi na Mheshimiwa Ibrahim Msabaha, tuligombana kwa sababu ya Salu.

Naomba niwe mkweli kwenye hili kwa ajili ya Salu, tumefikia mahali nimesema asiruhusiwe, lakini anaruhusiwa, sasa hivi ni kero na ninasema Mheshimiwa Waziri hata sasa hivi tukitoka hapa twende na mimi nikupeleke *stand* ya Maili Moja, kasikilize kero ya polisi na *agent* Salu. Sikuwa na nia ya kulisema hili, lakini nimeamua kulisema. Hii inadhalilisha, watu wanachukua nafasi ya sheria kama zipo za kumweka mtu ndani tu kwa sababu zao wenyewe. Sasa hicho ni kitendo kibaya. Nilisema nina *vested interest* na nime-*declare. (Makofi)*

Naomba *Salu Investment* ifutwe kwenye u-*agent* wa kukusanya kodi ya *stand* ya Maili Moja. La mwisho naomba kuhusu Mafia waangaliwe, anapozungumza Mbunge wa Mafia kuhusu gati, anazungumza Mbunge kuhusu kituo naomba jamani mumwelewe. Sasa hivi Mafia imekuwa kero, kuna viongozi wasiowatakia heri wala mema katika suala la maendeleo wananchi wa Mafia wanataka ibaki ilivyo bila maendeleo. Nashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba na mimi niunge mkono hoja iliyotolewa na Waziri Mkuu na niwapongeze kwa kutoa hotuba ambayo ni nzuri. Leo nimeamua nizungumzie suala moja tu linalohusu Ofisi ya Waziri Mkuu na lenyewe ni la Makao Makuu, Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbele ya safari nitaomba kwamba wakati umefika wa mtu kusema ukweli kwamba tuhame turudi Dar es Salaam, tusiendelee kukaa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *master plan* iligawanyika katika sehemu kubwa nne. Sehemu ya kwanza ilitaka Jiji hili liwe na *Man Centered City,* liwe na barabara za magari, liwe na barabara za wapita kwa miguu, liwe na barabara za waendesha baiskeli, Jiji hili lilitaka Ofisi ya Serikali yaani Rais na Wizara zake zote ziwe Dodoma, lilitaka Spika na Bunge lote liwe Dodoma, lilitaka Jaji Mkuu na Mahakama zote ziwe Dodoma na lilitaka ofisi zote za Balozi zilizoko Tanzania ziwe Dodoma. *(Makofi)*

Katika kipindi cha miaka 30 iliyopita tulitegemea Serikali itekeleze *master plan* iwe na sehemu ya pili ambayo ni miundombinu. Tulitegemea utekelezaji wa *master plan*

uwe na shule za kusomesha watoto wetu, tuwe na hospitali, tuwe na umeme, tuwe na maji, tuwe na mabenki na tuwe na *airport* ya kuwa-*accommodate* wageni na mahoteli ya kuwa-*accommodate* wageni wanaotembelea hapa Dodoma. *(Makofi)*

Miaka 30 baadaye hatuna Ofisi za Ubalozi hata moja. Miaka 30 baadaye Rais na Wizara karibu zote hazipo hapa, miaka 30 baadaye, Jaji Mkuu na Mahakama yake hawapo Dodoma, lakini miaka 30 baadaye Spika na Bunge lake tu ndiyo wako Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 wakati wa Bajeti kama hii alikuja rafiki yangu Balozi mmoja simtaji jina lake, akanipigia simu na kunieleza kwamba atakuja Dodoma kwenye Bajeti na kwa sababu ni mgeni alikuwa *exited* sana kuja Dodoma na akaniambia amekuja kuangalia Makao Makuu mapya ya Tanzania kwa sababu alipopata *briefing* aliambiwa Dodoma ni *Capital City.* Alipowasili moja kwa moja waliingia kwenye *galley* tukashindwa kuongea, lakini tulipotoka akaniambia inabidi mabalozi tuondoke kabla ya jua kuzama turudi Dar es Salaam kwa sababu kiwanja cha ndege cha hapa hakina umeme na hakina vifaa vya kuongozea usiku. Lakini *of interest* akaniuliza tunaweza tukapata dakika fulani au saa ya kwenda kwenye Makao Makuu nikatembelee? Nikamwuliza unataka kufanya *shopping?*

Akasema hapana nataka kuangalia *master plan* ya Jiji mnavyo-*design the modern 21st Century City* ili tuone namna ya kusaidia. Nikamwambia nadhani hamtakuwa na muda. Akaniambia kimji kinaitwaje? Nikamwambia hii ndiyo Dodoma na *Capital City.* Ni maili ngapi kutoka hapa? Nikamwambia ndiyo hii hii! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilishukuru sana *Dean* wa *Diplomatic Cope* alipowaambia Mabalozi sasa ni muda wa kuondoka, waondoke waende kule. Lakini baadaye kiliniuma sana. Nikasema hivi kweli ile *master plan* inafuatwa?, Zile *open space* zilizokuwa zimetengwa na akina Mheshimiwa *Sir* George Kahama, mwaka 1974 mpaka 1979 zinafuatwa kweli? Mbona hazijengwi? Ule mpango wa kupanda miti milioni moja kwa mwaka na *survival rate* ilikuwa 98% miti ile inaendelea kupandwa Dodoma? Maana hatuhitaji hela za kigeni pale? Lakini nikauliza Mabalozi wa *EU* hivi mpo pamoja na sisi katika kuhamia Dodoma? Wakasema hatupo pamoja. *Donors are not with us* katika masuala haya ya kuhamia Dodoma na ndiyo maana nadhani hata ubalozi mmoja haujajengwa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua Serikali itajibu kwamba hii ni Sera ya Chama chetu cha Mapinduzi. Mimi sina wasiwasi lakini sera hubadilika, tulishabadilisha Azimio la Arusha. Najua Serikali itajibu kwamba azma ya Serikali iko pale pale, lakini azma ni Katiba? Hii azma itaendelea miaka mingapi? Najua tutaambiwa mipango mingine iko mbioni au mipango hii inashughulikiwa. Inashughulikiwa vizazi kwa vizazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti wa karibu, ukiachia mbali Mji wa Lilongwe ambao ulihama kutoka Blantire na ambako walitumia fedha ya wakati ule walipohamia Lilongwe mwaka 1984/85, fedha zilizotumika, linganisha pia mabilioni ya fedha yalitumika Abuja, walipokuwa wanahama kutoka Lagos kwenda Abuja gharama za

uhamishaji wa Makao Makuu ni mabilioni ya dola. Sisi katika *Budget* hii 1/3 ya *Budget* nzima ndiyo inatumika kwa *development.* Katika hiyo 1/3, 3/4 tunategemea misaada ya nje na misaada hiyo ya nje iwapo na sisi katika suala hili. Kwa hiyo, *we have more 300 years* kujenga Mji wa Dodoma kama tunataka huu Mji wa Dodoma uwe katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *history* inataka mtu mmoja atamke tu siku moja aseme tuhame Dodoma. Jamani mimi sijaona katika *research* niliyofanya ukiachia mbali Pretoria, kidogo hakuna Bunge ambalo liko *isolated* katika nchi yake yaani lililotengwa na Serikali na Mahakama Kuu yenyewe ikajipachika mahali peke yake na ikategemea kufanya kazi zake kwa makini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Tanzania ni Mbunge peke yake katika Bara la Afrika, ambaye anapotoka kwenye Jimbo lake inabidi aende kwanza Mkoa mmoja unaitwa Dodoma, akajadili Bajeti ya Serikali, halafu afunge safari kuifuata Serikali Mkoa mwingine ambao unaitwa Dar es Salaam akafuatilie utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Jimbo lake. Ni adhabu kubwa na kwa kweli inabidi tujijue kwamba kwa kweli tunaumia zaidi kuliko Wabunge wengine wa sehemu zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa kuhusu Makao Makuu, lakini mimi naomba kabisa kwa vichwa vya kutulizana na naomba hili kwa sababu tumepata shilingi bilioni tano mwaka 2003/04 kwa ajili ya kujengea Ukumbi mpya wa Bunge mwaka na huu ni mwanzo kama alivyosema Mheshimiwa Basil Mramba kuwa tutakazana usiku na mchana kuhakikisha kwamba hizi fedha zitakuwepo. Tumepata shilingi bilioni tano za ujenzi wa Jengo la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua kuna *master plan* ya ujenzi wa Jengo la Bunge. Lakini hata kabla sijasema kitu hapo Waziri Mkuu mwaka 2002 alitueleza nadhani hata mwaka 2003/04 kwamba yeye atahamia Dodoma na atachukua Ofisi ya Chimwaga kule juu porini, ikawe ndiyo ofisi yake yaani mbali ya kutengwa Dodoma, aende porini kule akakae kule. Najua anafuata nyayo za Mawaziri Wakuu waliopita kwa mfano Mzee Rashid Kawawa, aliishi hapa, Mzee Cleopa David Msuya, alikuwa hapa, Mheshimiwa Samwel Malecela, alikaa hapa na Marehemu Edward Sokoine alikaa hapa, nadhani anafuata nyayo za Mawaziri Wakuu.

Lakini Makao Makuu haina maana ya Serikali kuhama kuja hapa. Hata mkihamisha Wizara nane au tisa zikaja hapa kama nguzo zote tatu hazijakaa pamoja na dunia nzima haijakaa pamoja hatujahamisha Serikali. Sasa tufanye nini? Naomba kutoa mapendekezo ingawa siyo mazuri lakini mimi nataka niyaseme tu haya yafuatayo:-

Moja, ujenzi wa jengo la Ofisi Kuu mpya ya Bunge la Jamhuri ya Muungano lijengwe Dar es Salaam. Tusikae wenyewe, najua wenzetu wachache wataumia, lakini nasema hivi ni vyema kutokuwapa matumaini wananchi wa Dodoma ambao wamekaa kwa miaka 30 kwa kutumaini ya Makao Makuu kuhamia Dodoma mpaka watazeeka, watapata watoto wengine, huku tumaini hilo liko pale pale, Makao Makuu kuhamia

Dodoma, nadhani hatupo sahihi, hatupo *fair* kuwaambia wananchi namna hiyo. Mimi natoa pole kabisa. Lakini mji huu unajengwa na fedha za nje na hazipo! *(Makofi)*

La pili, majengo yaliyopo Dodoma hayawezi kukaa kama *white elephant* yaliyopo, kingeweza kuwa Chuo Kikuu kimoja cha madini na jengo kama hili likawa ndiyo *Conference Hall* moja nzuri na *complex* ikawa *Univesity* safi kabisa na nyumba zile zikatumiwa na Maprofesa, bado uchumi wa nchi ukapanuka pale pale badala ya kuwa hivi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokitaka mimi ni kuwafanya Wabunge wawe na Serikali yao, badala ya sisi kuisubiri Serikali itufuate Dodoma, kwa muda wa miaka 30 imeshindikana ni vema sisi tukaifuata Serikali Dar es Salaam kwa sababu dalili zote zilizopo ni kwamba Serikali haiwezi kuhamia Dodoma na kwa kweli wala huhitaji kwenda shule kujua kwamba Makao Makuu yatahamia Dodoma hii itakuwa ni hadithi ya kudumu lakini ni azma ya Serikali najua, ni sera ya Chama cha Mapinduzi najua na kwamba mambo mengine yanashughulikiwa au hatua zingine ziko mbioni najua. Lakini lazima mtu aamke aseme Makao Makuu haya hayapo na zile mbio hazipo na shughuli zile ni chache na azma ile inaweza kubadilika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kusema ninaunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, lakini natoa changamoto kwa Waheshimiwa Wabunge, wenzetu kukaa na kutulia, jambo linalowezekana tulitekeleze.

Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti na hali ngumu ya uchumi, magonjwa yaliyopo ya ukimwi, magonjwa yaliyopo mengine ya kuambukiza, umaskini unaoikumba nchi hii, balaa la njaa lililoingia katika nchi hii na matatizo mengi ya utengenezaji wa miundombinu Kitaifa, hatuna nafasi ya kutenga shilingi milioni 71 kama zilizotengwa mwaka huu, milioni 71 kuweza kujenga jiji jipya la karne ya 21 la Dodoma na kutegemea Serikali, Mahakama Kuu na vyombo vingine vije Dodoma, hiyo itakuwa ni kujidanganya na ni ndoto ya mchana. Twende turudi Dar es Salaam tuungane na viongozi wenzetu na Dodoma igeuzwe iwe Chuo Kikuu tena *Mining Universty* nzuri kabisa na nina hakika tukienda hivyo tutakuwa tunasema ukweli. Chama cha Mapinduzi kimejaliwa kujikosoa chenyewe tunaangalia mbele lakini pia tunaangalia nyuma.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Upinzani wanaleta mihadhara ya siasa ndani ya Bunge, sisi tunachambua sera na tunaangalia tulikotoka, lakini kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, gharama zilizojificha za hatua yetu ya kuendelea kuwa Dodoma, achia mbali kwamba zingine zimeondoa maisha ya binadamu akiwemo aliyekuwa Waziri Mkuu mmoja, ajali zinazotokea za barabarani, gharama za mafuta na watu kukaa kwenye nyumba huku na kule sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Umetumia dakika zako vizuri kwa kuzungumzia jambo moja tu nadhani Waheshimiwa Wabunge, mkijaribu kuzungumza mambo mengi kiasi cha dakika kumi na tano hazitoshi. Lakini kwa njia hii zinatosha sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pia nimshukuru Waziri Mkuu na kumpongeza kwa hotuba yake nzuri yenye sura ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze katika eneo la barabara ya Kibiti - Lindi - Mingoyo. Kwanza, niishukuru Serikali kwa azma ya kujenga barabara ya Kibiti - Lindi - Mingoyo. Kwa hilo naishukuru sana. Hivi sasa sisi watu wa Mikoa ya Kusini tunaanza kupumua. Barabara hii ilikuwa ni donda ndugu lakini leo limepata dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mashaka tu kidogo nataka niyaseme. Kuna eneo la kipande kutoka Mbwemkulu - Mingoyo kuna mjenzi aliyepewa ambaye nina mashaka naye kwa sababu mpaka sasa hakuna kifaa chochote kilichopo *site.* Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwa Waziri Mkuu aende akaone hili kwa sababu sasa ni muda mrefu toka tumefanya mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningeiomba Serikali itakapofikia ujenzi wa barabara hii kutakuwa na kitu kinaitwa bomoa bomoa. Naamini kitakuwepo kwa sababu kuna nyumba zilizojengwa karibu na barabarani lakini wananchi hawa hawakufanya makosa kujenga majumba haya kwa sababu hawakuelezwa mapema. Tunajua kuna *road reserve* lakini hawakuelezwa kwa sababu hilo wananchi wa kawaida hawalijui. Kwa hiyo, naomba hilo lisifanyike kama ilivyokuwa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba wamebomolewa wasilipwe. Naomba ndani ya Jimbo langu walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wananchi hawa ni maskini mno, wengi wamejenga nyumba hizo kwa muda mrefu, kwa hiyo, leo wakibomolewa hawataweza tena kuzijenga kama hizo. Naomba walipwe.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niende katika maeneo ya mawasiliano ya simu ndani ya Jimbo langu. Ndani ya Jimbo la Kilwa Kusini, Wilaya ya Kilwa kuna simu zile zile za asili alizoacha mzee yule tusiyemtaka sisi Mkoloni. Simu zile mimi ninapoziona napata kichefuchefu, tena nashindwa hata katika Ofisi yangu kuweka simu zile za kukoroga kwa sababu zimepitwa na wakati na ndani ya Bunge hili naahidiwa mara nyingi kwamba simu zile zitabadilishwa kuwekwa simu za kisasa, lakini hilo jambo halifanyiki.

Naomba kupitia kwa Waziri Mkuu kumwomba Waziri mhusika, anibadilishie ili aniondoe kichefuchefu na mimi nipate kuweka simu ndani ya Ofisi yangu. Maana bila hivyo, basi nitadumu mimi kukaa bila simu, kwa sababu kila ninapoona simu ile namkumbuka Mkoloni, mtu ambaye tumemfukuza. Jambo hili linanitia uchungu sana! Katika mambo kama yapo yanayonitia uchungu, hili zaidi.

Mheshimiwa Spika, niende katika eneo la gesi ya Songosongo. Hii gesi ya Songosongo iko ndani ya Jimbo langu. Kama ni mzazi mimi ndiye niliyezaa. Lakini

niliposoma kitabu cha Waziri Mkuu nimeona gesi hii mimi mzazi sinufaiki, wananufaika watu wengine. Ndio, najua unaweza kumzaa binti akaja akanufaika mtu mwingine. Lakini si unapata mahari? Unapomwoza mtu mwingine wewe si unapewa mahari? Leo hata mahari mimi mwenyewe mwenye binti yangu sipewi, maana yake nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo linasikitisha sana na lina maonevu makubwa. Hakuna mahali popote nilipotajwa kama mimi ndani ya Jimbo langu kutakuwa na umeme unaotokana na gesi hii, hakuna. Yametajwa maeneo mengine tu. Lakini dalili ya kuwa Kilwa imedharaulika kiasi kikubwa, hata ile kambi ya wakandarasi ile iliyoambiwa kwamba itajengwa pale Somanga, basi imeondolewa imepelekwa Muhoro. Maana ingejengwa pale wangefaidika wananchi wa Somanga, lakini leo inajengwa Muhoro. Sasa hilo nalo ni ushahidi tosha kama Kilwa imenyang'anywa haki zake zote. Sasa ni vyema hili tukapata majibu yake ni nini hasa.

Mheshimiwa Spika, pia hakuna mpango wowote wa kuonyesha kwamba suala la gesi itakapofika Somanga kutakuwepo na mpango wa kupelekwa Kilwa Masoko, hakuna kwa sababu sikuona. Ningeomba Waziri Mkuu yeye kwa kuwa ni Kiranja anaelewa yote, anijulishe kama bwana ninyi hamna haki, pamoja na kumzaa mtoto huyu, lakini hampati mahari, sisi tunamchukua kwa kuwa mtoto huyu ni mali ya Taifa, basi sina jinsi. Kama ni mali ya Taifa, basi ichukue lakini mimi nimemlea kwa muda mrefu na nitaendelea kumlea. Kwa sababu pamoja na walinzi wanaolinda lakini pamoja na wananchi wa Kilwa wana jukumu la kuilinda gesi hii. Sasa kama wanailinda gesi hii; Je, malindo yao wanapata nini? Manufaa yao yakoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie katika eneo la kilimo. Tumeelezwa hapa katika hotuba ya Waziri wa Fedha kwamba kutakuwepo na kilimo cha zao la chakula kila Wilaya. Mimi hili nimelifurahia sana. Lakini nataka nimjulishe Waziri wa Fedha kupitia kwa Waziri Mkuu kwamba wananchi wengi maeneo mengi katika Wilaya nyingi wanajitahidi kulima mazao ya chakula lakini hawafanikiwi kwa sababu ya wanyama waharibifu. Sasa hili ameweka mikakati gani katika kuondoa wanyama waharibifu? Kwa sababu kama kulima watu wanalima, wanajitahidi. Kama Kilwa sisi hatuna tatizo la kulima, lakini tatizo letu ni wanyama waharibifu. Sasa mikakati yake ikoje ya kuondoa wanyama waharibifu? Kwa sababu huwezi kuweka mipango ya kuzaa tu kwanza.

Mheshimiwa Spika, unaweka mipango ya kulea kwamba nitakapozaa watoto kumi nitawaleaje? Sasa tunaomba kwanza utuwekee mikakati ya kuondoa wanyama waharibifu, sio ya kulima tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niende eneo la uvuvi wa meli za kigeni. Kilwa mategemeo yetu makubwa ni bahari na kilimo. Hivi sasa tumeingiliwa na uvuvi wa kutumia nyavu ndogo zile ambazo zimekatazwa zinazoitwa kokoro na wanazitumia watu wa meli kubwa. Meli hizi hutumia nyavu hizi kuvua samaki wakubwa na wadogo na wale wadogo huwatupa baharini baada ya kufa na wakawa hawafai tena. Sasa baada ya muda mfupi tunaamini Kilwa kutakuwa hakuna samaki wakati katika eneo letu lililobaki lina samaki ni Kilwa na Mafia tu.

Ningemwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, hili suala alishughulikie. Mwaka 2002 nilipiga kelele hapa katika Bunge lakini hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna uvuvi mwingine mbaya zaidi ya huo wa kutumia gesi. Wanazama ndani ya bahari wakivaa vyombo vya gesi, wakifika chini ya bahari wanakwenda kuvunja matumbau, wanaharibu mazalia ya samaki yote. Hii nayo ni mbaya, hatimaye hata vijana wetu wanaotumiwa kwa uvuvi huu wanapoteza maisha yao. Nalo hili ningemwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, aliangalie kwa sababu linaharibu samaki, lakini pia linapoteza maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, uvuvi huu wote wanafanya watu wa kigeni, sisi wenyewe wa Kilwa hatufanyi, tumekatazwa kutumia kokoro na kokoro tunazo. Sasa kama wageni wanaruhusiwa, basi na sisi wananchi wa Kilwa turuhusiwe. Inaonyesha dhahiri kwamba kuna ubaguzi kati ya wazawa na wale wasio wazawa ingawa jana hapa kulikuwa kumepigwa kelele ya uzawa, lakini wakati mwingine lazima tuuseme huu. Tuna haki ya kuusema huu sana, kwa nini tusiuseme? Mzawa ndio mtu mwenye haki na apewe kipaumbele kwanza.

Sasa kama mzawa hapewi kipaumbele anapewa mtu sio mzawa kwa nini tusiseme? Hata kama mtu mwenyewe namchukia, sisi tuna haki tuseme wazawa, ndio!! Wewe si ulifuata matunda yetu sisi wazawa? Unakuja kujaje? Sisi tunajua ulikuja kwa kufuata matunda ya wazawa. Kwa hiyo, hii tuchukie, kama ina kuchukia ondoka. Wewe si sio mzawa, ondoka tuachie wenyewe wazawa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba uniruhusu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba hii nzuri na kuipongeza Ofisi yake nzima kwa maandalizi mazuri yaliyofanyika. Naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni na kuwakaribisha wajiunge nasi katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ili nisipoteze muda naomba nizungumzie umeme wa Ngara, kaika Ibara ya 43 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Umeme huu unatokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais wa nchi hii mwaka 1995 na umekuwa ukisuasua toka mwaka jana ulipoanza kujengwa. Mapema mwaka 2003 kimetoka kisingizio kizito cha kwamba umeme huu hauwezi kusambazwa mpaka Miji ya Rurenge na Kabanga kwa hofu ya kutoa fidia ya wenye mashamba.

Nilipofika Mkoani nikamwona Meneja wa Mkoa nilimwambia kwamba aende Ngara akatazame. Hakuna mahali popote ambapo patahitaji fidia yoyote hasa kwa safari ya kwenda Rurenge. Nimekuja Wizarani, nimezungumza habari hii nikafikiri kwamba nimeeleweka. Lakini cha ajabu leo tena ninapoingia kwenye kitabu hiki cha nne,

maendeleo ya Wizara na Mikoa nakuta kwamba hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa mradi huu ambao sasa hivi unajengwa.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unajengwa pamoja na umeme wa Biharamulo. Umeme wa Biharamulo umepewa shilingi 5,309,620,000/= na umeme wa Ngara unapewa shilingi milioni 400. Ahadi ya Wizara ni kwamba umeme wa Ngara na umeme wa Biharamulo utawashwa mwezi Septemba, 2003. Sasa mimi sielewi, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati kwa kuijua vizuri sana hali ya Wilaya ya Ngara, matatizo yake kiulinzi, kiusalama, kiuchumi na kiutamaduni, kusudi wananchi wa Ngara wapate umeme huu. *(Makofi)*

Umeme wa Ngara kwenda Rurenge ni muhimu kwa sababu ya Taasisi nyingi zilizopo ikiwa ni pamoja na machimbo ya *Nickel,* Kabanga. Mji wa Kabanga upo mpakani mwa Burundi, ni maingilio mazuri sana ya biashara nzuri ya nchi yetu kwa sababu ndio kuna forodha na kila kitu. Kunyimwa umeme huu mimi nakuita ni kuwadhalilisha viongozi wakuu wa Taifa hili kutoa ahadi zao zisiweze kutekelezwa. Kusema kweli nimesumbuka sana na umeme huu na inawezekana pengine hapa kuna kitu ambacho si cha wazi katika kupitisha mradi huu. Sidhani kama umeme huu unaweza ukawashwa Ngara kwa shilingi milioni 400.

Mapema ilikubalika kwamba wataleta *Kilovolt* 35. Leo sasa wamebadili wamesema wataleta *Kilovolt* 11. *Kilovolt* 11 hazitoshelezi hata Mji wa Ngara peke yake, haitoshelezi hata kidogo. Mimi nafikiri nimwombe tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, kila Kiongozi Mkuu anayekuja Wilayani Ngara au Mkoani Kagera, umeme wa Ngara unasomwa katika risala. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati aweze kuwasaidia watu wa Ngara, wameteseka kwa kuilinda nchi hii kwa muda mrefu, sasa umefika wakati kwa vitu kama hivi vya maendeleo Wilaya ya Ngara ipewe tuzo. Naomba sana, wananchi wa Ngara wanisikie kwamba mimi sauti yao nimeifikisha Bungeni na nimeikabidhi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na wawe na hakika kwamba nina hakika Waziri Mkuu atasaidia kuokoa hali hii katika Wilaya ya Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Wizara ya Afya, Ibara ya 47 katika hotuba hiyo. Nilipenda Serikali ijue kwamba Watanzania wengi ni wagonjwa. Watanzania wengi ni wagonjwa, tumekabiliwa na magonjwa ya aina yote. Kuna kipindupindu, kichaa cha mbwa, uti wa mgongo, tuna kila tatizo huko Vijijini, wakulima wetu ni wanyonge, wakulima wetu hawana madawa ya kutosha, wakulima wetu hawana usafiri, wakulima wetu hawana waganga ambao wana ujuzi wa kutosha kuwasaidia, matatizo ni makubwa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inafahamu. Lakini la msingi sasa hivi ni kwamba katika Bajeti hii hakuna kitu kinachofikiriwa cha kuona kwamba Vituo vya Afya, Zahanati vilivyoko huko Vijijini vitapewa usafiri kwa nchi nzima katika Bajeti hii.

Nimepitia katika vitabu hivi, hotuba ya Mheshimiwa Basil Mramba, imesema hakuna kitu kama hicho. Tunasema tuzalishe, tunasema tuondoe umaskini, tutawezaje kutimiza hayo? Ilani ya Uchaguzi haiwezi kutimilizwa na watu wanyonge wanaokwenda kwa kujikongoja, wasioweza kufanya kazi kwa muda wa saa nyingi.

Wilaya ya Ngara ina Vituo vya Afya vitatu vya Mabawe, Bukiriro na Murusagamba, Kituo cha mbali kabisa kiko kilometa 135 hivi. Kituo cha karibu kiko kilometa karibu 30. Vituo vitatu hivi kwa miaka zaidi ya 20 havina usafiri hata kidogo. Mwaka 2002 peke yake tumepoteza akinamama na watoto wao watatu. Mmoja alikufa na mtoto wake tumboni wakati nikiwa hapa Bungeni wakati kama huu. Mwaka 2003 Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ameona, ametoka kuzunguka Wilaya ile hivi karibuni, namshukuru sana. Ameona Kata za Bugarama, Murusagamba, Kata ya Bukiriro ilikokaa. Sasa hivi watu wanauawa ovyo ovyo na wakimbizi, maeneo hayo na wala majeruhi hawapati usafiri hadi hospitali ya Wilaya kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, taarifa zipo, Serikali inazijua, hawana hata pikipiki ya kusafiria. Ni juzi tu Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi imeweza kuokoa Polisi wa Murusagamba kuwapa pikipiki angalau waweze kutembelea kidogo kuwaona wananchi na ninaipongeza sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Lakini nimehangaika. Ninapofika katika Wizara ambayo inahusika Wizara ya TAMISEMI hakuna kitu cha kuweza kuwasaidia wananchi wa Ngara. Wakimbizi wanatupa shida, tuko mpakani, hali ya usalama kutokana na Wakongo, Wanyarwanda, Warundi wote tunaifahamu. Utekaji tunaufahamu. Wananchi wanauwawa kila asubuhi na jioni, mapadri wengi wanakufa, watumishi wanakufa, baadhi ya shule zinafungwa kwa sababu ya kushambuliwa na hakuna usafiri kwa vituo hivyo kusaidia wananchi, zahanati ili kutoa huduma za mwanzo, kabla ya hizo muhimu.

Naomba Wizara ya Fedha, iweke fungu kwa kununua magari kwa sababu ya Vituo vya Afya kwa nchi hii. Naomba Waziri Mkuu alione hili, nchi haiwezi kuendelezwa na watu wanyonge, watu ambao wanakufa, wasioweza kutibiwa. Naomba nisaidiwe Wilaya ya Ngara kwa hii miaka zaidi ya 20 bila kuwa na magari kwa Vituo vya Afya, vipewe magari ili kusudi wagonjwa waweze kusafirishwa. Watu wamechoka, wanaijua CCM yao, wanaijua Serikali yao ya CCM.

Hivi vipi watu hawa wasiweze kusaidiwa hata katika dimbwi la matatizo haya kukosa usalama, kukosa amani ya kushindwa kuzalisha na kushindwa hata kutembea? Kila kiongozi anayekuja katika Mkoa wa Kagera lazima asindikizwe. Mkuu wa Mkoa atasindikizwa, Waziri Mkuu akija atasindikizwa, Rais akija atasindikizwa, tutafika wapi? Naomba nipate msaada huo ili tuweze kuendelea kuwapa wakazi wa Ngara imani kwamba CCM na Serikali yake inawajali, inawahurumia na hivyo inawalinda na maradhi kwa kuwapa usafiri kama sehemu nyingine za Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo mawili tu, yanatosha. Naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii iliyo mbele yetu. Kwanza, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya wa CCM kwa kufanikisha uchaguzi wao katika Majimbo yao na kuingia katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nina wajibu wa kuwapa pole wananchi wa Pemba kwa kuwachagua wenzetu kwa kutojua hasa dhamira na sababu ya kuingia katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanataka siku zote kufanyiwa haki na kutetewa kwa yale ambayo yanawajibika kwa maendeleo ya nchi yao. Lakini kinyume na wenzetu hawana mawazo hayo! Wao dhamira yao ni kukomoa. Kama wamekuja hapa waache dhana ya Vyama vya *CUF* na CCM. Hapa tumekuja kuwatafutia wananchi maendeleo na wahakikishe kwamba hapa wameiwakilisha Zanzibar. Kwa sababu waungane na wenzao watafute mantiki nzuri ya kufanikisha na yale ambayo wanahisi kwamba si mazuri ni wajibu wao kutetea na kukaa pamoja ili kufanikisha ili kuwa pamoja na kufanikiwa kuleta maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia inajirudia. Sisi tuliotoka Visiwani tunaelewa vizuri sana, si wageni. Ndio nashangaa mimi hata mtu wa Tanzania Bara kujiunga na Chama cha *CUF,* mimi nashangaa sana! Historia ya Vyama kwa kule kwetu ni tofauti sana na Tanzania Bara. Mtanzania Bara anadai maendeleo bila ya kujali Chama cha CHADEMA wala Chama kingine chochote. Lakini kinyume na wenzetu, lazima tujirekebishe tuwe pamoja tujenge nchi yetu. Ni ajabu tuliyonayo katika nchi hii kwamba leo kiongozi unataja kuingia sehemu ambazo hata hazistahiki. Ni ajabu sana! Sababu wenzetu tumewaarifu tu kwamba chakula tayari mje mle, hawakujua kilivyopatikana, hili ndilo tatizo lililotukuta. Lakini kwa sisi tuliokichuma na leo tukafika hapa na tukachukua historia ya wazazi wetu, *wallah* hatuwezi kusema kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee katika hotuba yetu. Katika hotuba hii ukurasa wa tano na sita, kwanza nawapongeza viongozi kutokana na mshikamano katika kuimarisha Muungano katika Serikali zetu mbili pamoja na kubadilishana mawazo ya Muungano. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kipengele napenda kunukuu. Tumefikia pia makubaliano kuhusu gawio litokanalo la faida ya Benki Kuu ya Tanzania. Ningependa tuweke wazi mambo yetu na mara nyingi tunapata matatizo kwa sababu ya kuyabana mambo yetu, kutoyaweka wazi. Sasa kama tunazungumza gawio katika nyanja hizi mbili au sehemu hizi mbili lazima tujue ni kiwango gani kwa sehemu fulani inaweza kufanikiwa na kiwango gani sehemu fulani inaweza kufanikiwa kabla ya kupatikana hii lakini tukajua tu kwamba tunapata, wale wanapata *percentage, one percent or two percent,* basi kwa chochote kinaweza kufanya gawio lile. Lakini hapa imekuwa kitu hiki kama valuvalu, hakuna undani uliotolewa kwamba katika mafanikio haya tunaweza au katika kile kitakachopatikana kwamba kwa upande wa Zanzibar kitapatikana kiasi gani.

Suala hili ningependa tuweze kupata maelezo sahihi kabisa kwa sababu tunapata taabu sana hususan kwa hawa wenzetu ambao walikuwa hawaelewi haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine vile vile ningeliomba katika hotuba ya Waziri wa Fedha, siku zote historia inajiridia na kitabu hiki unaweza kukiona kwamba ndio kitabu

tu, lakini kizazi chetu, hivi wengine tunatunza. Tukiondoka hapa tunachukua tunavitunza vizuri sana. Sasa hata ikiwa miaka 20, kihistoria, hiki mtoto atakuja kusoma hata ikiwa mjukuu. Kuna gawio lile la 4.5 yatokanayo na hapa imezungumzwa misaada kutokana na *Programme Assistance,* ile ilizungumza kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mimi ningeomba hili suala la kusaidia liondolewe. Ukisema unamsaidia mtu ni ridhaa, hana haki, una hiari yako na leo tunasema kusaidia. Hatujui mbele watawala watakuwa nani. Ndio! Mbele wanaweza kuja vijana wapya kabisa wakaweza kubadilisha mantiki. Sasa ningependa hiki kitu kusaidia kiondolewe kama kweli ipo haki kwa Wazanzibar. Sikilizeni *CUF,* ninavyochangia ili na ninyi mfuate huo mfano, natetea Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Wazanzibar, iwekwe bayana hapa kwamba hawa wananchi wa Zanzibar wana haki sio kusaidia, ina maana kusaidia ni ridhaa. Naweza kukusaidia au nisiweze ni ridhaa yangu mwenyewe. Kwa hiyo, ningependa hapa vile vile pafanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, lingine alizungumza kijana hapa kuhusu Dodoma. Chama cha Mapinduzi hapa kinakwenda na sera zake. Mara nyingi hata kama wazee wetu wamefariki lakini tunawakumbuka na kwa sisi wengine huwapigia *Fat-ha* ili kuwaombea dua kule waliko. Nasema ili kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere, Makao Makuu lazima tuendeleze Dodoma. Kusema kwamba tuondoke kuhamia Dar es Salaam, hatumtendei haki Baba wa Taifa. Leo nazungumza Dar es Salaam. Wewe ulipozaliwa tu kweli ulitembea? Wewe ilikuwa mzee kachukua mimba miezi tisa ukazaliwa ukatambaa ukaenda dede, wakati unakwenda tata, wakati unakwenda unafanyiwa mazoezi ya kutembea ndipo leo ukafika hapa ukasota, leo ndio ikafika hapa na leo ndio ikawa unazungumza katika Bunge hili Tukufu. Wewe unataka Dodoma ijengeke kwa miujiza!

Mimi nakumbuka Dar es Salaam, mji ulikuwa Kariakoo tu, karibu kwingine kote kulikuwa na simba tu. Lakini yamekuja maendeleo *step by step,* ndivyo tunavyokwenda, hatua kwa hatua. Hatuwezi kufanya miujiza. Leo tukumbuke kwamba, Dodoma isiwepo wananchi tumewaweka mahali pa baya. Wananchi wamefanya mengi sana ili kuisaidia Serikali kwa ajili kwamba kujenga matumaini kuwa Makao Makuu yatakuwa Dodoma. Kwa hiyo, tunawajibika kuyaendeleza Makao Makuu yawe Dodoma. *(Makofi)*

Mara nyingi tunaambiwa vijana tuna haraka sana ya maendeleo na hatuna ustahimilivu na ndiyo tunafika wakati mwingine mahali pabaya kabisa vijana, ndiyo tatizo letu hilo. Mtu mzima hasimami akasema vile. Kama mimi hapa siwezi kusema kama vile. Siwezi kusema na vile mimi ni mtu mzima na akili zangu, nikaseme vile. Haiyumkiniki, kwa hiyo, nasisitiza kwamba Makao Makuu lazima yawe Dodoma. Kama kawaida yangu katika Bunge hili Tukufu, nikisimama bila kukumbusha habari ya Ukimwi itakuwa dhambi. Wazee nasema kama viongozi tuna jukumu kubwa sana. Ni kawaida yangu lazima, hii ni sera yangu na mimi natoa katika Bunge hili. Ikiwa kwa Ukimwi nitachukua kama dakika mbili nizungumzie. *(Makofi)*

Wazee tuna kazi kama vile viongozi, katika kuwaelimisha vijana wetu. Lakini pia dini zetu hazituruhusu kufanya maasi. Sasa pigo kubwa kusema kwamba sisi tunasaidiwa, tusaidiwe bilioni ngapi? Hii si dawa, nakwenda kunywa dawa kana kwamba umerefusha maisha, maisha hayaji kama hivyo. Kuacha mambo ya zinaa ndiyo yatatusaidia kuondoa maradhi ya Ukimwi. Si dawa, si kusaidiwa misaada au kitu kingine chochote, kuacha zinaa, hii itatusaidia. Kuondoa maradhi haya na tuwaelimishe watu wetu, vijana wetu. Kwa sababu leo ukisema kwamba kuna mambo wenzetu wa Magharibi kusema kweli wanatughilibu. Leo wanakuja wanasema kwamba utumie *condom.* Ina maana unaambiwa wewe nenda kafanye hiki kitendo. Fanya kitendo, kwa sababu una kinga, una kinga gani? Jibu hapa ni kuacha zinaa, ndiyo kuondoa mambo ya Ukimwi, hakuna suala lingine. Tubadilishe tabia zetu na tufanye taratibu ambazo zitatusaidia kuepukana na mambo haya ya zinaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu wale waliokuwa wamepata nafasi kama mimi kukushukuru kwa kuwapatia nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kabla ya kuendelea, nampongeza Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kwa kutambika kidogo. Kwa sababu sisi wa Visiwani tuna mila zetu. Tuna mila ukitaka kufanya jambo unatakiwa utambike kidogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, hongera sana kwa kutambika na kuonyesha njia iliyotuleta hapa na kwa nini tuko hapa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Bajeti aliyotuletea. Lakini vile vile kupitia kwake nawapongeza Wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, pamoja na Watendaji wa Wizara ambayo anaiongoza. Wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mama Rose Lugembe.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikuwashukuru vile vile Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyosaidia kuielekeza Wizara hii hadi kufika kuweza kuandaa ama kuletewa hotuba iliyokamilika au Bajeti iliyokamilika katika Bunge lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile sikupata nafasi ya kuchangia katika hotuba mbili zilizotangulia ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Kwa kupitia kisimamo hiki nilichosimama, ilikuwa vile vile nao niwapongeze kwa hotuba nzuri waliotuletea na mipango iliyo yakinifu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau, niruhusu niwakaribishe ndugu zetu Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika chaguzi ndogo ya mwaka 2003, karibuni sana. Nadhani kazi iliyotuleta hapa ni kusimama pamoja kama Taifa moja na kuwatetea na siyo kugeuza hadhara hii kuwa ni Ukumbi wa mapambano ya vyama vyetu vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake Ibara ya kwanza, alisema kwamba, aliomba tumwunge mkono yaani tupitishe Bajeti yake. Mimi binafsi naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tukubali Bajeti hii kuipitisha kwa moyo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya nne katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nanukuu alipokuwa akizungumzia hali ya kisiasa na chaguzi zilizokuwa zimefanyika Zanzibar. Aliwapongeza, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kazi nzuri iliyokuwa imefanywa na mimi naomba kuungana naye kupongeza Tume hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla wake chaguzi zilizokuwa zimefanyika Zanzibar zilikuwa zina mapungufu mengi. Najua na naheshimu kauli ya CCM, viongozi wa CCM na naheshimu kauli ya Waziri Mkuu. Lakini nataka kuzungumza tu kwamba naelewa kwa sababu kama ni viongozi wakuu, waliyasema hayo kwa upeo ambao wanaujua wao. Lakini kwa sisi ambao tumeyajua yaliyotokea Zanzibar, nasema uchaguzi ulikuwa na mapungufu mengi sana. Sitaki kuyaeleza hapa kwa sababu mwanzo wa maelezo yangu nimezungumza hapa haikuwa uwanja wa kisiasa. Lakini ninachozungumza kwamba yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya sita ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, anasema Mheshimiwa Spika, nanukuu: “Kwa kutambua umuhimu wa kuendeleza na kuimarisha Muungano, Serikali zetu mbili zimeendelea kuimarisha mazingira na mashirikiano na kuondoa kero mbali mbali za Muungano.” Bado kero ziko nyingi na kwa kweli hizi wakati mwingine hawa wapinzani wetu au ndugu zetu ndiyo wanaozivalia njuga kuzipigia bomba na kuzieleza kana kwamba ni mapungufu kwa upande wa CCM. Ningeomba CCM na ningeomba Serikali ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar wakae kitako wajitahidi kupunguza kero hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kuna gawio linalotokana na faida ya Benki ambayo ni moja ya kero ambayo ilikuwa imeondoshwa. Tunashukuru kwa hilo. Kuundwa Tume ya pamoja ya Fedha. Tunashukuru kwa hilo. Ingawaje Tume ya pamoja imechelewa mno kuundwa. Lakini hata hivyo, tunashukuru kuundwa kwa Tume hizo, ambayo ilikuwa ni utekelezaji Kifungu 134 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Ibara ya tisa anazungumza, nanukuu: “Kuna taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni ya mwaka 2000/ 2003 itatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge katika mkutano huu.” Katika mwaka 2002/2003 ujenzi wa kumbi mpya za kisasa kwa ajili ya mikutano ya Bunge Dodoma, ujenzi wa Ofisi ya Zanzibar na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nina swali katika hili na ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atujibu hili wazi wazi, anatuambia nini kuhusu suala la Ofisi za Wabunge Zanzibar? Hapa panaonekana pana kigugumizi. *(Makofi)*

Suala la Ofisi za Wabunge, Wabunge wote wa Tanzania ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama Ofisi zinajengwa upande mmoja wa Muungano hakuna sababu kwa nini isijengwe upande wa pili wa Muungano. Kuna tetesi ambazo hizi siwezi mimi kuzithibitisha. Inasemekana kwamba kuna wakubwa fulani kule wamesema kwamba tusubiri mpaka wawakilishi nao wapatiwe nafasi za kujenga Ofisi zao za wawakilishi kwani ile Ofisi itakapojengwa, ni Ofisi ya Mbunge fulani kwamba ni Ofisi yake au ni Ofisi ya Mbunge ambayo ingeweza kutumiwa na Mwakilishi. Kama kuna uwezekano wa kwamba Ofisi ile inajengwa leo hutumiwa na Mbunge huyu, kesho na keshokutwa akiondoka atatumia mwingine. Tatizo ni kitu gani, kwamba tusubiri mpaka labda kutoke upande wa pili au Zanzibar nao waweze kutolewa kuchangia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi hili niliona kwa upana wake halina mantiki ya kuweza kuelezea. Lakini nije haraka haraka kuna suala hili la MMEM. MMEM kwa ufahamu wangu ni kwamba ni msaada ama ni pesa ambazo zinatoka kupelekwa kwa Halmashauri kusaidia kujenga mashule na ni mkopo huu. Ni mkopo ambao leo uko pamoja, kesho na keshokutwa tutalipa pamoja kama ni Watanzania sote. Kwa nini pesa hizi hazipelekwi Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu alipaswa labda nalo hili kama kule kuna Serikali na huku kuna Serikali kwa namna moja au nyingine suala la elimu *at the end of the day* unakuta kwamba tunaunganika katika elimu ya Chuo Kikuu au la siyo hivyo, tutajikuta kwamba Zanzibar tuko kisiwani kama tulivyo kisiwani na hakuna ambacho kitachoweza kufanyika. Kwa sababu suala la elimu, uendelezaji wa elimu ni gharama kubwa. Hilo limejitokeza katika taarifa zilizokuwa zimetolewa siku za nyuma inasemekana kwamba watoto wa Zanzibar kuingia *Form Five* walio-*pass* ni 13.4% lakini ukija katika Bara imekuja *more than 44%.* Sasa hiyo inaonekana ni mwanya ama ni ufa mkubwa ambao umejitokeza.

Mimi ningeomba kwa hili nalo Serikali ya Muungano, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania. Ina maana kwamba makucha yake na mkono wake mmoja uko kule. Kwa nini yeye asisaidie. Lakini kama hili halitoshi kuna suala la pesa, wanaita *Capitation* dola 10 kwa kila mwanafunzi, nazo ziwe zinakwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo nalo lizingatiwe na tulione kwamba linapatiwa muafaka. Mwisho, ningekuja katika suala la Ukimwi. Suala la Ukimwi kama alivyozungumza ndugu yangu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, nadhani hili siyo suala kubwa kama vile ambavyo tunaliona. Suala la Ukimwi ni suala ambalo linakamatana na maadili ya kidini ni masuala ambayo yanakamatana na maadili ya Muumba. Dini zote zinakataza kuzini. Tuacheni kuzini. *(Makofi)*

Dini zote zinakataza kuzini, tunasema tena, dini zote zinakataza kulawiti. Tuacheni, gharama kubwa tunatumia ya misaada tunayopata upande mmoja zinaitwa *condom. Condom* tunanunua nadhani, zinanunuliwa. Mie simo. *(Kicheko/Makofi)*

*Condom* nadhani zinanunuliwa, hazitolewi bure. Sasa wale wanaozalisha ndio wale wale wanatuambia fanyeni. Lakini upande wa pili tununulieni biashara hizi. Kwa hiyo, tunachokifanya upande huu wanatoa msaada, lakini upande wa pili wanatuambia nunueni, upande wa pili wanafanya biashara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kama nilivyotangulia kusema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na hivyo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, Waingereza husema *charity begins at home.* Nafikiri ni vema, ni sahihi na ni haki ya asili, *the natural justice.* Watu wa Lindi kufaidi umeme wa Songo Songo kwanza kabla ya watu wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, natumaini Serikali imesikia kilio chao na itawasaidia kupata umeme. Natumaini wakipata umeme, mashine zile ambazo *TANESCO* wataziondoa pale Lindi na Mtwara naomba wazipeleke Loliondo ili mji wa Loliondo nao ufaidi umeme kwa njia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi naipongeza sana kwa dhati kabisa Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa mafanikio makubwa ya kiuchumi kwa muda mfupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikijaribu tu kuangalia mafanikio hayo, fanikio moja ni kukua kwa Pato la Taifa kwa kufikia asilimia 6.3. Pili ni kushuka kwa mfumko wa bei kutoka asilimia 4.5 kwenda asilimia 4.3. Tatu, kuongezeka kwa akiba ya fedha ya kigeni kutoka *US dollar* 1.3 hadi 1.5 bilioni. Nne, kuongezeka kwa ukusanyaji wa kodi ya ndani kufikia asilimia 12.3 na tano, ni kutoa msamaha wa madeni kwa mabilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona haya ni mafanikio makubwa sana. Lakini najiuliza pamoja na mafanikio haya ambayo ni makubwa kwa nini maisha ya wananchi wetu wa kawaida vijijini bado ni duni na yanaendelea kuwa duni pamoja na mafanikio hayo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya makubwa ya kiuchumi bado hayajapunguza ukali na ugumu wa maisha kwa wananchi wetu wa kawaida vijijini. Kwa mfano, wananchi wa kijiji cha Masusu Wilayani Ngorongoro, bado wanatembea kilomita 10 na zaidi kupata maji ya kunywa. Aidha, mwananchi wa kawaida wa kijiji cha Pinyingi, Wilayani Ngorongoro atatembea zaidi ya kilomita 10 kupata huduma za afya. Kwa nini, wakati ambapo tumepata mafanikio makubwa kiasi hiki kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ya kiuchumi makubwa hivi nasema bado hayajamfikia mwananchi wa kawaida kijijini, mafanikio haya yameongeza tofauti kati ya

wachache walio nacho na wengi wasio nacho, kati ya maskini na tajiri, kati ya watu wa mjini na watu wa vijijini. Tuna ongezeko kubwa tofauti au tabaka kati ya vikundi hivi vya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali iangalie hili kwa makini kwa sababu tukiendelea na tofauti hizo bila kutafuta namna yoyote ya kudhibiti usalama wa Taifa utakuwa mashakani. Kwa hiyo, naomba sana Serikali hili iliangalie kwa makini jambo hili. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia Mheshimiwa Spika, ni suala la msongamano wa wafungwa gerezani na naomba kunukuu hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 12. Naomba kunukuu: "Takwimu zinaonyesha kwamba idadi ya wafungwa na mahabusu kwa sasa inazidi uwezo wa magereza yaliyopo. Kwa mfano, hadi tarehe 31 Mei, 2003 kulikuwa na wahalifu 44,667 katika magereza yote nchini ambapo uwezo uliopo ni wa kuhifadhi wahalifu 22,699." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, msongamano huo mkubwa wa magereza yetu au kutokana na msongamano huo magereza yetu yamekuwa ni *death place,* mahala pa kwenda kufia tu. Kwa sababu huko magerezani ni mahali pa kupata magonjwa mengi ya kuambukiza kama vile Ukimwi, kama vile kipindupindu. Hali ya magereza yetu sio nzuri na inatisha. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali ijaribu kuangalia kwa upya namna ya kukabiliana na tatizo hili la msongamano mkubwa wa magereza na ikiwezekana kama tumebinafsisha Reli, tumebinafsisha *TTCL,* tumebinafsisha Bandari, sioni ni kwa nini tusianze kuangalia uwezekano wa kubinafsisha magereza ili wananchi wanaofungwa pale wapate hali nzuri zaidi kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu hoja ya Waziri Mkuu. Lakini kabla sijashika kasi ya kutoa mchango wangu naomba nifanye yafuatayo:-

Kwanza, kuwashukuru Wabunge wote kabisa waliochaguliwa hivi karibuni, bila kujali itikadi zao. Nawashukuru sana karibuni sana, tujenge nchi yetu. Lakini pia niishukuru sana Serikali kwa ujumla kwa maana ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa Bajeti waliyoleta mwaka 2003/2004. Bajeti safi kabisa. Imepunguza migogoro, imepunguza hata watu kuchangia vibaya. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali katika hilo. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hoja yake nzuri haina matatizo na mimi nachukua nafasi ya kuiunga mkono kabisa ili niweze kuchangia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi nimechagua kuchangia kwa mtindo ufuatao. Kwanza, nitabainisha baadhi ya maeneo na nitataja zile kero za msingi katika maeneo hayo. Shabaha yangu ni kutaka Serikali ijue haya matatizo na iweze kuchukua hatua za kutatua matatizo. Ndiyo shabaha yangu na ndiyo maana ya kuboresha katika

kuchangia. Lakini vile vile, kero hizo ndiyo kikwazo kikubwa kinachotuchelewesha katika kujenga uchumi. Uchumi ndiyo nyenzo ya kuleta maendeleo zaidi. Kwa hiyo, vikwazo hivyo tusipoviondoa uchumi wetu utabaki pale pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndiyo shabaha yangu katika mchango huo. Nianze na eneo hili la Kilimo. Mimi nimechagua kilimo kwa sababu kilimo ndiyo kinachangia kwa asilimia 50 ya Pato la nchi yetu. Kwa hiyo, usipozungumzia hilo kwa kweli wananchi hawatanielewa. Nasema kwamba kilimo huchangia Pato la Taifa kwa asilimia 50. Kwa hiyo, ni kitu muhimu sana ni jambo la msingi na Serikali inatakiwa lazima ifanye kazi isicheze na kilimo. Lakini vile vile kilimo ndiyo kinachangia mauzo ya nje kwa asilimia 75. Kwa maana basi kilimo bado kinashika nafasi ya kwanza sana katika kujenga uchumi. Kama hatutasimamia kilimo vizuri, uchumi wetu lazima utabomoka na utaanguka chini. Hivyo basi, mimi nasema kwamba fagio la kufagia umaskini, ni kilimo. *(Makofi)*

Kama ni hivyo, lazima hii mfagio tuisuke vizuri ili iweze kufagia vizuri. Kwa hiyo, lazima tupeleke fedha za kutosha katika Sekta ya Kilimo huko vijijini. Sasa nibainishe matatizo basi yanayogusa katika sekta hii ya kilimo na ndiyo maana hatupigi hatua ya kwenda mbele. Bado wakulima wanatumia teknolojia duni katika shughuli za kilimo nchini. Serikali inatakiwa lazima iwaondoe pale, wamekaa kwa muda mrefu sana katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipowaondoa katika eneo hilo, kilimo hakiwezi kufanikiwa hata kidogo, tuwaondoe pale. Lakini vile vile wakulima hawana nyenzo za msingi katika majukumu yao ya kilimo bado kilimo chetu kina misingi ya ujima, sio kilimo cha kisasa. Lazima Serikali iwatoe wakulima katika kilimo hicho chenye misingi ya ujima twende katika misingi ya kisasa. Serikali ndiyo inatakiwa iwezeshe na kuwezesha ni kupeleka nyenzo, fedha, na uwezo ili wananchi waweze kuleta mapinduzi katika nchi hii. Lakini tusipofanya hivyo, tutaendelea kulalamika uchumi unashuka, lakini wanaowezesha uchumi ili uweze kupanda kule kwa wakulima, wataendelea kulima katika hali iliyo duni zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kilimo cha umwagiliaji mashamba hakijapewa mchango wa kujenga uchumi vizuri. Hii ni kwa sababu hatujawawezesha wananchi wetu kutumia haya mabonde, kutumia uwezo wa kisasa na kadhalika ili kilimo hiki cha umwagiliaji kiweze kuzaa matunda. Kwa hiyo, Serikali vile vile inatakiwa tutoke pale ili tuweze kuleta manufaa kwa kupitia kilimo hiki cha mabondeni, cha umwagiliaji. Labda nitoe mfano. Hapa nchini ziko takribani, hekta milioni 29.4 zinazofaa katika kilimo cha umwagiliaji. Lakini ni hekta 191,000 tu sawa na asilimia 0.6 ndizo zinazoendelezwa, tena chini ya uwezo. Kwa hiyo, sekta hii bado haijatumiwa vizuri, eneo hili la umwagiliaji. Sasa Serikali lazima ijue, katika eneo ambalo linategemewa kuleta uchumi hali ndiyo hiyo. Lakini vile vile nitoe mfano kule Kondoa. Kondoa tuna mabonde yenye maji ya kumwagilia, hekta zilizofanyiwa utafiti wa uhakika ni 6,882.

Lakini ni hekta 260.5 sawa na asilimia 4 tu ndiyo zinazoendelezwa lakini chini ya uwezo na Wilaya nyingine hivyo hivyo na nchi nzima hivyo hivyo, sasa matokeo yake

ndiyo hivyo. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali izingatie suala la kilimo, tukitoka katika eneo hilo tukafanikiwa uchumi utakua na umaskini utaondoka. Nasema tuchukue hatua za kufa na kupona Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na kadhalika, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na sisi Waheshimiwa Wabunge vile vile, ndiyo kazi yetu kuhimiza na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo lingine kubwa ni wakulima wanyonge wavuja jasho kukosa Benki yao ya Kilimo na Ushirika, Benki ni muhimu. Wakulima hawana eneo hili la Benki ya kuwasaidia katika shughuli za kilimo na shughuli za ushirika na Benki ya namna hii inaweza ikaanzishwa na Taasisi nyingi tu. Kwanza, Serikali yenyewe inawajibika, ndiyo ya kwanza ambayo inatakiwa lazima ianzishe Benki ya namna hiyo, lakini vile vile wahisani wenye nia nzuri, lakini haitoshi pia Sekta binafsi zinaweza zikaanzisha ama pia wadau wa kilimo na ushirika lakini inahitaji usimamizi na uwezeshwaji wa Serikali. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba ili tuweze kuwa na uchumi ulioboreka, ni lazima tuimarishe kilimo sasa kwa kiwango cha asilimia 50. Napenda nizungumzie eneo la elimu hasa katika shule za sekondari. Shule za sekondari hasa za kutwa zinakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, umaskini wa wazazi wao unachangia sana wanafunzi kuwa watoro, ni umaskini tu, ukienda katika nchi ambazo ni matajiri hakuna utoro mkubwa, lakini nchi maskini utoro ni mkubwa kwa sababu ya umaskini, watoto hawana lishe nzuri na kadhalika. Mimi nilikuwa nafanya utafiti katika maeneo yangu ni kwamba katika wanafunzi 200 wanaoanza shule, ni wanafunzi 130 tu ndiyo wanaomaliza na 70 wote wanayeyuka, hawasomi. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo mimi naomba Serikali ifute kabisa ada hii ya sekondari ili watoto wote maskini wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo hilo tatizo lingine ni kwamba kama ulivyoeleza shida kubwa ni ada watoto wanashindwa lakini vile vile lishe na pia ukosefu wa *hostel.* Wasichana wanaongoza zaidi kwa utoro kwa sababu hawana hostel katika shule za kutwa na umaskini unachangia kwa hiyo wanapata matatizo ya mimba na kadhalika. Kwa hiyo, lazima Serikali katika utaratibu wake tujenge *hostel* ili tuwape umuhimu wa kwanza wasichana wasome. *(Makofi)*

Lakini vile vile uhaba wa walimu. Walimu ni wachache sana na wataendelea kuwa wachache. Napenda nitoe mfano mmoja, kuna mwalimu mmoja anaitwa Mwalimu Nchii, anafundisha katika Sekondari ya Kikuyu, sasa ni mwaka mmoja na miezi minne hajapata mshahara tangu ameajiriwa na kinachomsaidia ni kwamba anakwenda kufundisha *tuition* ndiyo anapata hela za kumsaidia, sasa walimu wote wakihamia kwenye *tuition* hatutaboresha elimu hata kidogo. Naomba Serikali izingatie kwamba inapoajiri walimu iwalipe mishahara, walimu watatoroka na tunajua tuko katika soko huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie tatizo la kipekee la walimu. Mimi naomba walimu waangaliwe vizuri katika maslahi yao, mishahara yao itazamwe, ipigwe jeki lakini madai yao, malipo yao na vitu vingine vyote vishughulikiwe. Lakini la msingi kabisa, naomba walimu wapewe posho ya mazingira magumu. Mimi nimewahi kuwa

mwalimu kwa muda mrefu, tunaposema mazingira magumu ni kwamba walimu wanatumia chalk zenye vumbi, wanasahihisha madaftari mengi, wanaanza kazi hata kabla ya saa 1:00 asubuhi na wanamaliza hata baada ya saa 9.30 na shughuli nyingi tu. Katika ushindani wa sasa tusipowawekea posho maalum watatoroka, wataondoka. Kwa hiyo, naomba walimu hawa wafikiriwe kipekee ili tuweze kwenda nao sambamba, watusaidie kuwafundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kusema kwamba suala la kuhamia Dodoma ni utaratibu wa kudumu, ni mpango wa kudumu. Sababu zile zile zilizofanya tuamua kuhamia Dodoma bado zipo, Dodoma ni katikati eti, hatukusema tuhamie Dodoma tu kwa sababu tunapenda ila ni katikati ya nchi na ni pazuri sana eti. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, sasa sijui hii ndiyo Serikali ya CCM na hii ni sera yetu, mimi nilitarajia hapa milioni pengine hata mia nane zitengwe kwa ajili ya kuendeleza Makao Makuu ili tuhamie haraka sana na pia safari hii nilitarajia ya kwamba Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri Mkuu atasema, Wizara kadhaa tena safari hii zitahamia, sasa kimya maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa muda wa kuweza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba nitaongea maneno machache kwa sababu mengi nafikiri yamekwishaongelewa na Waheshimiwa Wabunge na pengine itakuwa si busara kurudia rudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba vile vile nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote waliohusika katika kuandaa hotuba hii, hotuba ni nzuri na ina maelezo mazuri ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tumeyaelewa vizuri. Kwa hiyo, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wa mawazo yangu kama nilivyosema, nitaongea kwa kifupi tu. Naomba nizungumzie maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali, wananchi wameniambia nije kuishukuru, niishukuru Serikali na hasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulifanya Jimbo la Kishapu liwe Wilaya. Wananchi wanashukuru sana katika jambo hili na wameahidi kuongeza jitihada zaidi za kuijenga Wilaya na kutoa mchango mkubwa zaidi wa uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, napenda kuishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hilo vile vile naomba niseme tu kwamba pamoja na kupata Wilaya, tumelipata katika muda mgumu kidogo, hali ya hewa imekuwa si nzuri, tunakabiliwa na tatizo la upungufu wa chakula. Nimefanya ziara katika Wilaya

yangu ambayo ina Kata 20, zote kwa kweli zina hali ngumu, si kwamba wananchi hawakuitikia wito wa kulima, wamelima vizuri tu kama ilivyo mila na desturi zao lakini kutokana na hali ya hewa kwa kweli imekuwa ni ngumu. Kwa hiyo, Wilaya nzima ya Kishapu ina hali ngumu ya chakula. Napenda kuiomba Serikali kwamba katika moja ya mipango yake ya kugawa chakula, iifikirie Wilaya ya Kishapu ambayo ina hali ngumu ya chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hilo kama nilivyosema, mimi naomba nichangie hoja moja tu kwa kifupi. Nataka nizungumzie juu ya uwiano katika mgao wa mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge letu lianze tumekuwa tukifuatilia hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri, tumeanza na ya Bajeti na sasa tuko hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeona makisio mengi ambayo yamefanywa na Serikali yetu katika kipindi cha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, katika mawazo yangu mimi nimegundua uwiano katika mgao wa mapato ya Serikali katika nchi yetu hauko sawa. Kutokana na hili iko baadhi ya Mikoa itakwenda kasi kimaendeleo na iko baadhi ya Mikoa ambayo itabaki nyuma kimaendeleo. Nataka niongee hayo kwa nini nasema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nizungumzie suala la mgawanyo wa raslimali za nchi na nataka nijielekeze vizuri zaidi kwenye maeneo yenye machimbo ya madini. Mimi ni mmoja wa wanaotoka katika eneo linalochimba madini ya almasi katika Mgodi wa Mwadui nadhani na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wa Mikoa mbalimbali, karibu nusu ya nchi yetu inatoa madini, tuna matatizo makubwa ya kimaendeleo. Lakini pamoja na kuwa na matatizo makubwa haya, viongozi tunajitahidi kuwahamasisha wananchi wajenge maendeleo yao. Lakini katika hilo vile vile inategemea uwezo na nguvu zao za kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nirudie upande wa sehemu ya madini. Sehemu ya madini sera iliyopo baada ya hayo madini kupatikana kwa mfano kama ni almasi au ni dhahabu, sera iliyopo mapato haya hupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ili kujenga maendeleo ya pamoja, hakuna kitu chochote kinachobaki katika eneo hilo la machimbo. Jambo hili linatupa maswali mengi na inafika mahali inaonyesha pengine sisi Waheshimiwa Wabunge wawakilishi wa maeneo hayo hatuitetei vizuri hoja hii, kuna matatizo makubwa, tuna tatizo la maji, tatizo la barabara na pia tatizo la shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninalotaka kuliongelea hapa, kwa nini nasema kwamba mgao wa mapato ya Serikali hauko sawa? Sera iliyopo sasa ni kwamba kwa upande wa wenzetu wenye mbuga za wanyama hupewa mrahaba kusaidia maendeleo ya eneo hilo. Nadhani ndugu zangu ninyi ni mashahidi mmekuwa mkisoma kwenye magazeti na kusikiliza redio, wakieleza jinsi wenzetu wanavyofaidika mrahaba na mbuga za wanyama, sisi wenye madini hatupewi chochote.

Napenda kuuliza kwamba tuna kosa gani katika Serikali hii? Ukiangalia hata athari anayeathirika zaidi ni huyu mwenye madini, kwanza wanaharibu ardhi halafu na haya madini yatakwisha. Mimi napenda nielezwe kwamba hivi sisi ambao tuna machimbo ya madini tulimkosea nini Mungu kutokupewa nafasi ya kuyatumia haya madini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe mfano, labda wengine watasema ooh mnajua mtaigawa nchi, nchi itagawanyika, mpaka sasa tumeishaigawa nchi hata ukiangalia sasa hivi hii Bajeti ya Serikali, kuna watu hapa wamepewa shilingi bilioni tano kwa ajili ya kufanya shughuli za kimaendeleo. Mkoa wa Shinyanga umepewa shilingi milioni 500, hebu angalia sasa shilingi bilioni tano na shilingi milioni 527 wapi na wapi, tutaendelea lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili nadhani kwanza siyo geni na wala halijaanza hapa Tanzania, ziko nchi nyingi za Kiafrika zinafanya haya. Kuna nchi nyingine kama Ghana ambayo ina madini, katika eneo la machimbo percent fulani inabaki katika eneo hilo ili kuweza kuisaidia ile jamii, sisi hapa kila kitu kinasagwa, wewe ni mpishi unapika wali unapakua mpaka ukoko, hivi kweli ni akili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie hili la Bajeti yetu, napenda leo niliongelee. Nimeeleza juu ya Bajeti yetu ilivyokuwa na nataka niwe wazi kwamba uwiano uliopo si mzuri ila unabagua na utatusababisha kurudi nyuma kimaendeleo. Ukiangalia hata katika Bajeti hii ya Kitaifa katika mgao wa Mikoa, nimejaribu kuweka utaratibu hapa, kwa mfano Mkoa wa Kagera umepewa shilingi bilioni 5.4, Mkoa wa Iringa shilingi bilioni 4, Mkoa wa Mbeya shilingi bilioni 3, Mkoa wa Morogoro shilingi bilioni 3.6, ukija hii Mikoa ya akina yahe Shinyanga shilingi milioni 527,718/=, Tabora shilingi 621,150/=, Rukwa shilingi milioni 318,897/= na Dar es Salaam kama nimeangalia vizuri shilingi milioni 240,000/= hela za ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi napenda kuuliza kwamba pamoja kweli kuna mipango mizuri ya nchi, hivi ninyi hamwoni kama kuna tofauti kubwa kutoka shilingi milioni 527,718/= na mtu ambaye amepewa shilingi bilioni 5, shilingi bilioni 5 gawa kwa shilingi milioni 527,718/= sasa hii haki iko wapi, hata ninyi mnaokaa kupanga, mnakaa kupanga mipango ya nchi mnaangalia kweli hii kitu? Sisi tunalaumiwa, tunaambiwa Waheshimiwa Wabunge wanaokwenda kule wala hawatetei, jamani tuangalieni! Hata Katiba inasema kwamba mapato yanayopatikana ni lazima tugawane wote sawa kwa sawa. Napenda kuwauliza kwa mujibu wa Katiba ya nchi kwamba, hivi kutoka shilingi bilioni 5.4 mpaka shilingi milioni 527,718/= ndiyo haki iliyoongelewa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kugawa maendeleo sawa? Katika hili mimi napenda kusema kwamba hakuna uwiano wowote katika maendeleo na kwa maana hiyo baadhi ya Mikoa itaendelea kubaki nyuma kimaendeleo hata mngefanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba niishie hapo lakini kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni ndugu yangu, basi napenda niseme tu kwamba naunga mkono hoja yake. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nishirikiane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuchangia kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda niungane na wenzangu vile vile katika kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya ambao wameingia Bungeni hivi karibuni kutoka Vyama vya *CUF* na Chama cha Mapinduzi. Tukio hili ni la maana sana kwa sababu Majimbo hayo wanayoyawakilisha yamekuwa hayana wawakilishi kwa muda mrefu. Kwa hiyo, wananchi sasa wamepata haki yao ya kuwa na wawakilishi wao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, mimi naunga mkono moja kwa moja hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa nilikuwa sijasema, sijapata nafasi ya kushiriki katika mazungumzo kwa hiyo niwashukuru na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa taarifa ya hali ya uchumi wa nchi na vile vile kwa Bajeti ambayo imewasilishwa na kupitishwa na Bunge hili. Napenda kusema kwamba kazi yao waliyoifanya ni nzuri sana na matokeo yake ni kwamba wananchi inaelekea wameipokea vizuri sana Bajeti ya Serikali ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii sasa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ambayo ni pana lakini vile vile ina kina. Imesaidia kutoa picha kamili kabisa ya shughuli za Serikali zilizofanyika katika kipindi kilichopita na shughuli za Serikali ambazo tunakusudia zifanyike katika kipindi hiki cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mimi nitapenda kusemea mambo machache sana. La kwanza, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi katika kushangilia mafanikio ambayo yameelezwa vizuri sana katika hotuba tatu ambazo zimetolewa mpaka sasa.

Bajeti ya Serikali ya mwaka huu imeonyesha kiasi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imedhamiria, kila uwezo unapopatikana kuwaondolea wananchi kero zinazowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii imeunda mazingira mazuri sana katika nchi yetu kwa sababu kama uchumi wenu unakwenda vizuri na siasa nazo zitakwenda vizuri.

Kutokana na kwamba hali ya uchumi wetu ni nzuri, uchumi unakua na kupanuka, matunda yake sasa yanaanza kutiririka mpaka kwa wananchi. Si suala tu la kuondolewa kwa kufutwa kodi ya maendeleo, lakini kazi hiyo imeanza kwa muda mrefu kidogo, suala la kufuta ada ya shule za msingi, suala la Serikali kuwasaidia wananchi kujenga shule zao, nyumba za walimu na kadhalika, suala zima la Serikali kuamua kuwalipa Makatibu

wa Vijiji na Makatibu wa Kata, yote hayo yanakwenda pamoja na yanaunda mazingira mazuri sana katika nchi yetu na ndiyo maana hata kwa upande wa kisiasa hali yetu ni nzuri sana, nchi imetulia, watu wanafanya shughuli zao kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mashaka haya ya msemaji aliyetangulia kabla ya huyu wa mwisho kuhusiana na uchaguzi ulivyokwenda Zanzibar, lakini kwa kweli niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba uchaguzi umekwenda vizuri katika nchi nzima na siyo Zanzibar tu. Umeunda mazingira mazuri sana kwa vyama kushindana bila ya kupigana na bila ya kutukanana, hayo ni mazingira mazuri kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa niseme kwamba haya mafanikio yaliyoelezwa katika hotuba hizi tatu, yanaonyesha kiasi gani Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin Mkapa na timu yake ya Waheshimiwa Mawaziri na viongozi wengine wote, walivyofanya kazi kubwa ya kukusanya nguvu hatua kwa hatua ili Serikali iweze kuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke tulikokuwa mwaka 1995 uchumi wetu ulikuwa unakua kwa kiwango gani, ni chini sana lakini kidogo kidogo sasa unakua kwa asilimia 6.2. Hilo linaonyesha kwamba inawezekana tukiongeza nguvu zaidi sisi wenyewe tutafika asilimia 7, asilimia 8 na hata zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema kwamba mkakati ambao umefuatwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, mkakati wa kukusanya nguvu ili kujenga uwezo ni mkakati madhubuti kabisa. Mimi nataka kuwahakikishia wananchi kwamba mkakati huo utaendelezwa ili mwakani tutakapokutana tena kwenye Bunge hili tushangilie zaidi na zaidi mafanikio ambayo yataweza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo nataka niseme kwamba, haya yote Serikali inafanya ya kujenga mazingira mazuri ili tuondokane na umaskini katika nchi yetu. Kwa hiyo, suala la kupambana na umaskini ni suala la msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme kwamba, Serikali imeonyesha jinsi inavyojitahidi kuunda mazingira mazuri ili kuondokana na umaskini katika nchi yetu. Haya tunayoyasema yote ni matokeo ya jitihada za Serikali kwa sehemu kubwa sana.

Sasa imebaki jitihada za wananchi na mimi ningependa niseme kwamba, mara nyingi tunapozungumza jitihada za wananchi tunaitazama tena Serikali pekee, mara nyingi sisi wenyewe nafasi yetu ya kushirikiana na wananchi na kuwaongoza ili na wao watoe mchango wao katika kubadili hali yetu ya maisha na kutokomeza umaskini, nafasi yetu mara nyingi huwa tunaipuuza, tunatazama wajibu wa Serikali tunasahau wajibu wetu sisi wenyewe. Kwa hiyo, nataka nishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, hakuna njia nyingine kwa wananchi ya kuondokana na umaskini isipokuwa wananchi wapanie kufanya kazi. Ni vizuri sote tuungane katika kuwashawishi na kuwashauri wananchi tunaowaongoza kwamba dawa ya kupambana na umaskini hakuna nyingine isipokuwa ni kufanya kazi kwa maarifa.

Sasa tukifanya hivyo kila Kaya itaondokana na umaskini kwa kuchapa kazi, kwa hiyo kila Kijiji kitaondokana na umaskini kwa kuchapa kazi na Taifa zima litaondokana na umaskini kwa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa neno moja ndogo, naona halijazungumzwa hapa. Bunge lako Tukufu mwanzoni mwa Mkutano huu lilichukua hatua ya nidhamu dhidi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu wanne.

Nataka niseme kwamba kitendo kile cha Bunge hili cha kuwawajibisha Waheshimiwa Wabunge wenzetu, ni kitendo cha kupigiwa mfano. Sisi wenyewe tunaweza kufikiria kwamba tumefanya jambo ndogo sana lakini ni jambo kubwa sana kwa sababu viongozi tunatakiwa tuwe waadilifu, viongozi hatuwezi kuchukua dhamana za kuongoza wenzetu wakati sisi wenyewe hatuongozwi na misingi na pia hatuongozwi na maadili.

Viongozi wakubwa kama Waheshimiwa Wabunge wakifika mahala wanakuwa tayari kubadilisha na kupotosha ukweli kwa maslahi ya watu binafsi, hiyo ni hali ya hatari sana. Lakini napenda kusema kwamba mimi nataka tujipongeze Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tumeonyesha mfano mzuri wa kuwajibika kwa kuwawajibisha wenzetu, Bunge hili litaheshimika zaidi kutokana na kitendo kile.

Wananchi walikuwa wanatusikiliza, walikuwa wanataka kuona tutafanya nini lakini kwa bahati nzuri tukasahau mambo ya vyama, tukasimama kwenye misingi ya uadilifu na tukachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona ni vizuri hili niliseme, lisipite hivi hivi tu, tumefanya kazi nzuri na kazi kubwa ni vizuri tujipongeze. Lakini kubwa zaidi tumejenga heshima ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MCHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ROBERT K. MASHALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni nzuri naiunga mkono asilimia mia. Baada ya kuunga mkono bajeti hii ninashauri Serikali iangalie maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo nayo yaingie kwenye mpango huu wa bajeti.

Kwa mfano, Wilaya yangu ya Bukombe ina matatizo mengi sana ya kukosa huduma za jamii na miundombinu ambayo itawawezesha kujikomboa katika suala zima la umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukombe haina umeme hata ule wa Generator, hakuna simu na tuna barabara moja tu yenye urefu wa kilomita 22 inayohudumiwa na Serikali kuu. Hivyo kwa sababu hizi zinawafanya wananchi wa Bukombe wajione kama wamesahauliwa na Serikali yao.

Jambo la kusikitisha zaidi ni pale wananchi wa Bukombe walipoomba mchango wa Serikali juu ya kazi kubwa waliyoifanya ya kujijengea hospitali ya Wilaya kwa kukamilisha ujenzi wa Ward nane na Serikali kuiomba ichangie ujenzi wa jengo la Utawala na Maabara lakini mpaka sasa haijatoa majibu ya kukubali au kukataa kutoa mchango wake. Maombi yamepokelewa na Mheshimiwa Festus Limbu - Naibu Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia bajeti hii iangalie uwezekano wa kutatua angalau tatizo moja kati ya haya. Naunga mkono hoja.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Waziri Mkuu, Mheshimiwa F.T. Sumaye. Vile vile napenda kuwapongeza watumishi wote walioko Ofisini kwako, kwa kuonyesha ushirikiano mkubwa wa kuandaa hotuba nzuri na yenye maana nzuri kwa Watanzania wote. Napenda kurejea moja kwa moja kwa kutaka kujua ufafanuzi ufuatao:-

1. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati ule wa uchaguzi mku mwaka 2000, ulifika jimboni kwangu Buchosa na baadaye Rais wetu alikuja na kutoa ahadi ya kujenga au kutengeneza barabara itokayo Nyakaliro hadi Lushamba, hadi hivi leo ahadi hii haijatekelezwa. Ninaomba nijibiwe na Waziri Mkuu kwa maandishi.

Mwisho naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, naomba kusema tangu awali kuwa naiunga mokno hoja/hotuba hii na imezungumzia mambo mengi ya msingi na muhimu kwa maendeleo ya jamii na Taifa la Tanzania.

Hata hivyo, naomba kuchangia katika maeneo machache yafuatayo:-

(1) Kuhusu soko la *Agoa, EBA, SADC* na kadhalika (ukurasa 21) bado inaelekea Serikali inatoa kipaumbele kwa ujenzi wa viwanda vikubwa vikubwa na kadhalika na sio viwanda vidogo vya kusindika mazao. Vile vile hakuna publicity na mikakati iliyo dhahiri? Napenda kupendekeza kwa orodha husika utangazwe sana katika magazeti, lakini vyama vya wafanya biashara na kilimo *(CCIAs)* za kila Mkoa na Zanzibar Chambers zishirikishwe kikamilifu ili waweze kutoa mchango.

(2) Kuhusu maendeleo ya TVT, kutokana na maendeleo makubwa ya teknolojia, nashauri Serikali ishirikishe watu binafsi katika kutoa huduma hii muhimu kwa Watanzania, ili isambae kwa haraka nchi nzima katika kufuata hii programu ambayo Serikali inaitekeleza pole pole. Kwa mfano inawezekana sana kufanya contract za muda ili vipindi vya TVT na hata *Radio Tanzania* virushwe kwa muda maalum hasa vile vipindi muhimu katika mikoa yote.

(3) Vita dhidi ya UKIMWI, bado ni kubwa na mikakati iliyopo ni mingi na kila aina. Lakini naomba sana Serikali kuangalia uwezekano wa kuleta sawa husika kwa bei ya nafuu. Bado gharama za sasa zilizopo ni kubwa sana. Kuna nchi (jina sikumbuki) ambayo hivi karibuni ilitiliana mkataba na kampuni moja ya India - na kufanikiwa kuwa itapatiwa madawa hayo kwa chini ya nusu ya bei ya soko. Hivyo nasi tungeweza kunufaika na mpango kama huu.

(4) Mheshimiwa Spika, katika ukurasa 70 suala la kuwawezesha Watanzania inaelekea karib litapata muafaka. Ni matumaini ya wengi wetu kuwa hali hiyo itasaidia hali ya maisha ya Watanzania wengi. Napendekeza mpango huu uguse sehemu zote za nchi yetu mkataba uwe unagusa kila Wilaya, kwa makusudi mazima la sivyo tutaona mpango huu ukitekwa nyara na wajanja wachache katika miji mikubwa ya Mikoa na wengine kuambulia patupu.

Naomba kusema tena kuwa naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge, Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ya kumshauri Rais wetu vizuri kwa kipindi sasa cha miaka minane (8) toka 1995-2003 tangu kuwa Waziri Mkuu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kusimamia Serikali ni kazi ngumu sana, Watanzania wote wanamwangalia yeye, pia sisi Wabunge tunashukuru kwa kutuongoza vizuri tukiwa Bungeni na nje ya Bunge. Tunashukuru anathamini mawazo yetu tunayoshauri kwa Serikali yetu ya CCM.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mapendekezo yangu katika hali ya ulinzi na Usalama. Tanzania tulikuwa kisiwa cha amani lakini sasa Tanzania imegeuka kisiwa cha damu. Ukarimu wetu ulituponza wa kuhifadhi wakimbizi, lakini tulifanya kwa nia njema, lakini wale wabaya wametumia nafasi hiyo kupoteza maana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wimbi la majambvazi limezidi kuongezeka labda sasa uletwe Muswada wa kupunguza majambazi kwa kutunga Sheria ya kunyongwa wote wataopatikana na makosa hayo. Nafikiri tutapungiza tatizo hili. Aidha, niombe vitambulisho sasa vitengenezwe haraka sana na silaha zote zikusanywe kwa wote walionazo kinyemelea.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri Mkuu kwa kusimamia kwa vyama vya siasa kwa karibu sana, bado kuna tatizo la kuvifumbia macho vyama vingine vinashughulika na ujasusi, ugaidi na udini.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa 1992 iletwe haraka sana. Inasikitisha dini zingine zinatumiwa na mambo ya siasa. Mfano, dini ya Waislam kuandamana kutaka kwenda Ubalozi wa Amerika, walipokatazwa waliamua kuchoma bendera, hii ni dini kweli au siasa???

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu katika hili, "Amani na Imani" zimetoweka kama yeye (Waziri Mkuu) ni msimamizi wa shughuli za Serikali anatuambia nini sisi Watanzania?

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Waziri Mkuu kwa kutueleza sasa TVT itasikika na kuonyesha matangazo yake Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya, Lindi na Tabora kwa awamu hii ya kwanza. Inapendeza Televisheni ya Taifa wananchi nao wafaidike na kodi yao ambayo walitoa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu waliangalie upya kuhusu usimamizi wa maamuzi yake kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Mimi naona maagizo yake hayatekelezwi na Wakuu hao kwa sababu wako chini ya TAMISEMI. Napenda kutoa mfano, akitaka kutoa agizo la Mkoa utakaokuwa na njaa Mkuu wa Mkoa/Wilaya awajibike, hii haina ugumu maana bado watasubiri maagizo mengine toka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa (TAMISEMI) ndipo watekeleze.

Mheshimiwa Spika, nashauri viongozi nilioiwataja wangerudishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili wawajibishwe na Waziri Mkuu moja kwa moja. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia apewe fedha alizoomba.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wasaidizi wake wote kwa hotuba yake nzuri yenye kuleta matumaini kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kututembelea Wilaya yetu na kutoa ushauri na maagizo muhimu mbalimbali hivyo yote yamepokelewa na wananchi vizuri sana na kuahidi kuyafanyia kazi kikamilifu kwa faida yao na Taifa kwa jumla. Wananchi wa Mbinga wamefurahia sana ujio wake na wanaomba mara zote Mheshimiwa Waziri Mkuu upatapo nafasi awatembelee.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwa makini sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuna kabisa mradi wa kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa Mkoa wa Ruvuma pamoja na Wilaya zake zote kutoka Makambako kupitia Njombe hadi

Songea kama tunavyoelezwa. Mimi sielewi kwa nini mradi hu umesahauliwa? Vile vile mradi wa umeme Mchuchuma na mradi wa chuma Liganga. Hotuba zote tatu ziko kimya na haifahamiki ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, nafikiri pengine mpango wa kupeleka umeme Mkoa wa Ruvuma wa *"National Grid"* ni mpango wa muda mrefu lakini wananchi wa mji wa Mbinga wamechoka sana kuishi na giza, kweli wamechoka. Wangependa sana waishi kama Watanzania wenzao wanaofurahia maisha kwa kutumia umeme.Hali hii ya giza inawarudisha nyuma kwa maendeleo.Je, hali hii itaendelea hadi lini?

Mheshimiwa Spika, kupitia meza yako, kwa heshima zote tunaomba sana *TANESCO* isambaze nyaya za umeme mji wote wa Mbinga na baada ya hapo waendeleshe umeme kwa kutumia *Generator* lililonunuliwa na Halmashauri ya Mbinga. Njia hii ni njia ya haraka ya kuipatia umeme mji wa Mbinga, badala ya kusubirisha mpango wa muda mrefu usiofahamika ni lini utaanza na lini utakamilika. Mpango huu wa muda mrefu pengine unaweza kuchukua miaka (40) arubaini ijayo kwa suala la umeme mji wa Mbinga, hatuwatendewi haki hata kidogo wana Mbinga.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningeomba vile vile kuwa Serikali ifanye kila iwezalo kukamilisha mradi wa kutengeneneza umeme kwa kutumia mkaa wa mawe Mchuchuma usiotegemea hali ya hewa. Mradi huu ungekamilika ungeondoa kabisa tatizo la mgao wa umeme nchini unaosababishwa na upungufu wa maji na hasa mwaka nchi inapokumbwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tatu kwa mafanikio mengi yaliyoonekana kuanzia 1995-2003. Hakuna mtu yoyote mwenye akili asiyepongeza. Kutokana na mafanikio hayo na uzuri ambao umeonekana kwenye bajeti ya Waziri wa Fedha huwezi ukakataa mwelekeo wa hotuba ya Mawaziri wote kwani Bajeti ndiyo kingozi wa mwelekeo wa mapitio ya Wizara zote.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nami nipitie baadhi ya maeneo machache kwenye hotuba yako. Kwa muda mrefu Wabunge wamelalamika kuhusu Ofisi zao lakini hakuna jitihada zinazoendelea tofauti na maelezo ya hotuba. Hakuna uwezekano wa Wabunge kufanya shughuli bila Ofisi. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi kujenga Ofisi za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kutoa mbolea kwenye maeneo za mikoa minne ambayo inazalisha chakula kwa wingi. Utaratibu huo uliyochukuliwa na Serikali utasaidia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tatizo kubwa linalo wakabili wakulima na wafugaji ni masoko. Wananchi wanaoishi karibu na mipaka mfano jimbo la Longido wanategemea

minada na masoko ya nchi jirani lakini usumbufu ni mkubwa sana mpakani. Huku Wakenya wao wanakwenda maeneo yote ya Tanzania. Naomba kwa kua Serikali imepunguza kero za wananchi iangalie usumbufu mkubwa ulioko mipakani, biashara ni ushindani lakini kama kuna vikwazo ambavyo zinawekwa hakuna ushindani tena.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka jana Serikali imetumia shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) kwa ajili Ujenzi wa Chimwaga ya jengo hilo mwaka huu Serikali imetenga fedha kiasi kile kwa mwaka jana kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo. Mimi bado sielewi jengo hilo ni la nini ni afadhali tupate maelezo ya kuridhisha kuhusu jengo hilo. Kama imeshindikana kuhamia Dodoma itakuwaje ikawezekana kuhamia Chimwaga mbali na mji huu. Nasikitika kusema kuna wananchi ambao hawana maji mfano Kijiji ambacho nakitaja kila mwaka cha Kiserian wanachota maji kilomita 28 kijiji cha jirani. Je, hao wananchi ambao wanateseka kila mwaka bila kupata maji watategemea nani? Naomba wananchi hao wakumbukwe mwaka huu. Nashangaa kama watu watakufa kwa shida ya maji huku Serikali inafanya miradi mingine ambayo haitekelezeki.

Ukiondoa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ni kupunguza kazi za Waziri Mkuu kwani malalamiko mengi ambayo yangeshughulikiwa na Waziri Mkuu zinachukuliwa tofauti na wakati uliopita. Mtumishi mbovu anachukua muda mrefu kudhibitiwa, kwa hiyo Halmashauri nyingi zimezorota.

Baada ya kueleza hayo naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika. Kuhusu suala la kuuza nyumba za Serikali kwa watumishi wa Serikali linalalamikiwa sana na Wabunge. Ningependa kupendekeza kama ifuatavyo:-

(1) Nyumba zilizoamuliwa kuuzwa ziendelee kuuzwa kwa wale watumishi wa umma na viongozi wengine wanaoishi humo.

(2) Lakini ule mfuko unaotokana na mauzo hayo usitumike tu kwa kujenga nyumba ili kuwauzia watumishi wa Serikali tu, bali wafanyakazi na viongozi wote wa nchi wakiwemo Wabunge na kadhalika. Kwa kweli Wabunge pia ni watumishi wa Serikali kupitia kwa wananchi. Utaratibu wa mauzo na malipo ya nyumba hizo uwe wa wazi na uandaliwe kwa namna itakayowezesha wote waliokopeshwa kulipa deni lao.

Nadhani si vyama kuwabagua Wabunge na viongozi wengine kwamba si watumishi wa Serikali. Ni makosa! Kama ni suala la nguzo tofauti, mbona Mahakimu wanachukuliwa ni watumishi wa Serikali (na wanakopeshwa nyumba hizi) wakati nao wako nguzo tofauti na Serikali *(Executive)?*

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

*Radio Tanzania* - Nawapongeza wafanyakazi wa *Radio Tanzania (D)* kwa kazi nzuri wanayofanya wakati mwingine katika mazingira magumu. Aidha, matengezo ya

Kituo cha Nachingwea yamekua yanaboreka siku hata siku na kwa ujumla usikivu wake ni mzuri. Tatizo ambalo linaikabili *RTD Nachingwea* ni ucheleweshwaji wa kulipa gharama za umeme na hii mara nyingi hupelekea kukatwa kwa huduma hiyo ya nishati na hivyo kuathiri shughuli zake wakati mwingine kwa vipindi virefu. Ninatoa rai kuwa uongozi uzingatie kulipa ankara zake za umeme ili huduma ya redio usiathirike.

Maelezo yalitolewa wakati *TTCL* inabinafsishwa kwamba wawekezaji wapya wataendeleza miradi yote ambayo ilishabuniwa na shirika wakati au kabla ya kubinafsishwa. Moja ya miradi hiyo ni uboreshaji wa huduma za simu katika Mikoa ya Kusini hususan Mikoa ya Lindi na Mtwara - kwa upande wa Mkoa wa Lindi mradi wa kuboresha mtandao wa simu ikiwa ni pamoja na kuziondoa exchange zote za kunyonga zilizopo Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Mtama na Kilwa. Lakini mpaka sasa hakuna lolote linaloendelea. Usikivu wa simu hizo ni duni sana na pengine kwa muda mrefu huwezi kupata huduma hiyo. Kero zaidi ni pale wahudumu wanaofanya kazi kwenye mitambo ya *Exchange* wanapojibu kwa jeuri wakati ukiwaomba msaada wa kuunganishwa.

Aidha, wakati ambapo huduma za simu zinaendelea kuboreshwa kila wakati teknolojia inapobadilika na kuna mlundikano wa wazi wa hudma za simu ukijumlisha simu za mkononi (angalia ramani za mtandao wa *TTCL, VODACOM, CELTEL, MOBITEL etc),* I jambo la kusikitisha kuwa maeneo fulani ya Tanzania yanatengwa na huduma hizo ambazo ni muhimu katika kuleta maendeleo ya biashara, utawala na kadhalika. Ni matumaini yangu kuwa Serikali na hususan Wizara ya Mawasilianio na Uchukuzi itatoa maelezo ya kina na kueleza kwa uwazi ni lini simu hizi za kunyonga *(magneto)* zitaondolewa ili wananchi wa Ruangwa, Nachingwea, Liwale na Kilwa nao wawe karibu zaidi na Watanzania wengine.

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, na mimi natoa mchango wangu mdogo kwa Ofisi hii. Nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshinda katika uchaguzi mdogo ambao ulifanyika *May 18,* mwaka huu, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nami pia naungana naye kuhusu ulivyoendeshwa uchaguzi huo kwa amani, usalama na haki - hasa kwa upande wa Pemba ambapo mimi nimeushuhudia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano katika hotuba yake ya kila mwisho wa mwezi, kwa mwezi *May, 2003* naye alipongeza hali ya uchaguzi ulivyokwenda, sasa yule ambaye anajaribu kuupinga ukweli huu analo jambo la kwake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kazi nzuri ambayo Tume yetu ya Uchaguzi ya Taifa *(NEC)* ningependekeza pafanywe mabadiliko walau Tume hii ifanane na ile Tume ya Uchaguzai ya Zanzibar *(ZEC)* ambayo imepatikana baada ya muafaka baina ya CCM na *CUF.* Kadhalika Watendaji wa Tume wapatikane katika hali ya uwazi na kidemokrasia badala ya utaratibu wa sasa kuwa Wakurugenzi wa Wilaya, Makatibu

Tawala wa Wilaya na Watendaji wa Kata huwa Wasimamizi wa Uchaguzi. Hii kwa kiwango kikubwa inabana na kutilia shaka kupatikana haki kwa wadau wote.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine nauelekeza katika uanzishaji wa Daftari la kudumu la wapiga kura. Miongoni mwa matatizo ambayo kwa kiasi kikubwa yanapatikana katika zoezi zima la uchaguzi ni kukosekana kwa Daftari la kudumu la wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, Daftari hili la kudumu limetajwa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Pia kuanzishwa kwake kumetarajiwa mara tu baada ya uchaguzi mkuu wa 2000 na tulitegemea daftari hili liweze kutumika rasmi katika uchaguzi mkuu wa 2005. Lakini hapa napata shaka kwamba muda umekwenda sana na sidhani kwa muda uliobaki itawezekana kukamilika shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, wasi wasi wangu mwingine ni kuhusu matakwa ya fedha kwa Tume ya Uchaguzi na fedha ambazo zimetengwa hadi sasa ni chache mno. Yote hayo yanakwamisha matayarisho ya daftari hili.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anitoe wasi wasi wangu huo hasa kuhusu mabadiliko ya Tume ya Uchaguzi ili uendane na matatizo ya demokrasia zaidi. Pia usimamiaji mzuri wa kuanzisha Daftari na kukamilishwa kwa muda unaotakiwa. Ahsante sana.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu awali ya yote nakupongeza sana wewe, Mawaziri wa Nchi, Ofisini kwako, Katibu Mkuu na wasaidizi wengine wote kwa hotuba nzuri uliyoitoa, kwa kweli imekuwa nzuri na changamoto kwa maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, napongeza sana hatua ya Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwalipa mishahara Watendaji wa Kata na Vijiji. Hatua hii itawafanya wafanye kazi kwa uaminifu na kujituma. Naomba Ofisi yako iwatafutie vitendea kazi mapema ili waanze kuchemka kuleta maendeleo kwenye maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hivi kuna kero ambayo imeishajitokeza upande wa *Radio Tanzania,* na *Radio* zingine za watu/mashirika binafsi hasa wakati wa taarifa za habari. Hapo mwanzo kwa mfano taarifa ya habari *Radio One,* ilikuwa inatangazwa/somwa saa 1.45 jioni watu walikuwa wanasikiliza na saa mbili usiku wanasikiliza *Radio Tanzania. Radio Free Africa, Radio Tumaini, Radio Zanzibar* na kadhalika, zilikuwa zinajiunga na *Radio Tanzania* kwa taarifa habari ya saa mbili. Utaratibu huu ulibadilika kienyeji enyeji tu. Naomba izingatiwe ya kwamba wananchi wanapenda kupata taarifa toka *Radio* mbalimbali kwa hiyo Ofisi yako ihakikishe inatengeneza utaratibu mpya ambapo utaratibu wa zamani unafuatwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kuipongeza sana Tume ya Kuthibiti ukimwi *(TACAIDS)* kwa kazi nzuri inayofanywa, nashukuru sana kwa utaratibu mzuri walionao wa kupewa fedha baada ya kupitia na kutathimini miradi toka Wilayani. Pia napongeza

sana kwa utaratibu mzuri ulioko wa kushirikisha Asasi zote zilizopo Wilayani, Mashirika ya Dini na kadhalika. Naomba tu kwa Wilaya ambazo hawajapata mgao wa fedha hizo wapewe waendelee kupambana na hili gonjwa la hatari (UKIMWI).

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kutoa fedha hizi za UKIMWI naomba ufuatiliaji uwe wa karibu sana kuona zinatumiwa kwa malengo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikukumbushe ya kwamba mwaka huu maeneo mengi yana uhaba wa chakula. Wananchi sasa hivi bado wanao uwezo wa kununua chakula naomba Ofisi yako ihakikishe chakula cha njaa - cha kununua kipelekwe maeneo yote yenye shida wananchi waanze kununua, badala ya kuchelewesha hatimaye wananchi waanzishe manung'uniko. Naunga mkono hoja 100%.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri kuhusu mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi yake na Ofisi ya Bunge 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, suala la uzalishaji mali (uk.19/20 kifungu 22). Natambua nia njema ya Serikali ya kukuza kilimo cha kujikimu na kukifanya kififikie kiwango cha Biashara ili kuinua hali ya maisha ya wananchi haa hasa waishio vijijini.

Hatua ya Serikali ya kukarabati skimu kumi na mbili za umwagiliaji maji mashambani zenye jumla ya hekta 3515 katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Bagamoyo (Bagamoyo na Ruvu) na skimu 65 nyingine (uk.64 kifungu 72) zenye jumla ya hekta 32,516 ni hatua nzuri sana na ya kutia moyo sana.

Lakini skimu hizi 77 zenye jumla ya hekta 36,031 zinawakilisha sehemu ndogo sana ya maeneo tuliyonayo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Eneo hilo ni asilimia 24% tu ya lile lilikuwa likitumika kwa kilimo cha aina hii katika mwaka 1993.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ndi kilimo cha uhakika zaidi katika uzalishaji wa chakula nchini lakini ukweli wa mambo ni kwamba umuhimu wake tunauongelea zaidi kuliko kuutekeleza. Wakati sio kwamba umefika bali sasa umepita sana kwa nchi yetu kutekeleza kwa vitendo thabiti mpango huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua zake za kukuza utalii kwa kuanzisha mbuga mpya ikiwemo ile ya Sadan katika Wilaya ya Bagamoyo (uk.27 kifungu 31) na maeneo ya hoteli za kitalii katika ufukwe (pwani) wa Bagamoyo (uk.34 kifungu 39).

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo sana kiutendaji, kitaalam na kifedha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo sehemu ya Barabara - kuanzia ilipoishia Barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam, hadi eneo la Nunge ziliko hoteli hizo za kitalii ni mbaya - mbaya sana. Napenda kuiomba Serikali kuu iangalie uwezekano wa kusaidia ukarabati wa sehemu hii ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za kiuchumi, nampongeza Waziri Mkuu kutilia maanani ujenzi na utunzaji wa barabara vijijini. Ni kweli kabisa hali ya barabara za vijijini ni mbaya sana sana (uk.31 kifungu 36) Wilaya ya Bagamoyo imeathirika zaidi katika eneo hili kutokana na fedha za mfuko wa barabara kufungiwa kwa karibu mwaka mmoja kutokana na makosa ya watendaji wa Halmashauri ambayo wao hawana namna ya kuzuwia lakini ndio walioathirika vibaya sana bila ya wao kuwa na hatia yoyote.

Mheshimiwa Spika, Watendaji hawa wanasababisha madhara kama haya bado wako kazini na bila ya kemeo la namna yoyote. Wako pale kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali za Mitaa (uk.47 vifungu 55 na 56) naipongeza Serilai kwa kuanzisha cheo cha Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji. Miongoni mwa kazi zao muhimu ni kuongoza na kuratibu shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Serikali ya kijiji ni Serikali kamili. Dhana hii ifafanuliwe vizuri na iwekwe katika hali ya kueleweka vizuri kule vijijini.

Vijiji vingi havitekeleji majukumu ya msingi yaliyo ndani ya mamlaka zao, zaidi kwa kutokutambua uwezo wa kiserikali ulio mikononi mwao. Hili ni suala zito lisiloeleweka vizuri kwenye vijiji vyetu karibu vyote.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri sana inayoonekana kufanyika katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mku wa Serikali kwa Hesabu za Serikali za Mitaa ni matokeo ya kazi nzuri sana ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* iliyofanyiika katika kipindi hicho. Kuongezeka kwa Hati Safi kutoka Hati 3 (2000) hadi kufikia Hati 68 (2001). Vile vile kushuka kwa idadi ya Halmashauri zilizopata Hati Chafu kutoka 76 na kufikia 40. Hali hii inaleta matumaini makubwa. Naipongeza Kamati ya *LAAC* naitakia kila la kheri iweze kuendeleza mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora (uk.49 kifungu 57/59) Mahakama za Mwanzo ndio zilizo karibu sana na wananchi na ndio zilizo katika ngazi za awali katika kulinda na kutetea haki za binadam. Mafunzo yaliyotolewa kwa Mahakimu wa Mahakama hizo 600 ni jambo zuri sana linalohitaji kudumishwa.

Taasisi ya Kuzuia Rushwa inastahili pongezi kwa kupanua Ikama yake na kusogeza huduma zake karibu na wananchi. Kusogeza huduma hizo kwenda sambamba na hatua thabiti za kuwashughulikia wala rushwa ambao wanafahamika na kwa hali ya kawaida tu mtu hawezi kuelewa uwezo wa kujilimbikizia mali pamoja na maisha ya anasa wanayoishi maeneo yale ya vijijini - wameutoa wapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika:-

(1) Ofisi za Wabunge majimboni: Kila mwaka Waheshimiwa Wabunge wengi tu tumekuwa tukilalamikia kutokuwa na Ofisi au kuwa na Ofisi chakavu mno zisizo na

hadhi yoyote ya Kibunge. Majibu tunayopewa siku zote ni kuwa Mikoa inapewa fedha kwa ajili ya Ofisi za Wabunge. Katika vitabu vya Kasma na Maendeleo ya Mikoa yapo haya yafuatayo:-

(a) Ujenzi na ukarabati Ofisi za Wakuu wa Mikoa.
(b) Ujenzi na ukarabati nyumba za *RCs.*
(c) Ujenzi na ukarabati Ofisi za Ofisi za ma-*DC.*

Hakuna ujenzi wala ukarabati wa Ofisi za Wabunge huoni huu ni ujanja wa Ofisi yako ili suala hili lilalamikiwe siku zote, kwa nini hakuna kasma ya Ofisi za Wabunge iliyowekwa wazi?
(2) Fedha za Maendeleo Mikoani: Mwaka jana wakati nikichangia hoja ya Ofisi ya Rais Mipango niliomba Ofisi hiyo ibadili ufinyu na uonevu wa kutoa fedha kidogo mno kwa mikoa ya Rukwa, Kigoma, Tabora na Singida. Niliahidi asipofanya hivyo nitaomba kumwona Rais wa Jamhuri. Mwaka huu 203 nikichangia hoja hiyo niliomba maelezo kuhusu jambo hili hili. Lakini sikujibiwa kabisa kwamba hoja hii ni upuuzi mtupu.

Siku ya Ijumaa nilikutumia takwimu ghafi juu ya fedha ya maendeleo iliyotolea kwa mikoa ya Rukwa, Kigoma, Tabora na Singida kwa kipindi cha miaka sita. Pia nilifanya mlinganisho na mikoa mitano ya Arusha, Mara, Iringa, Kagera na Kilimanjaro kwa kipindi cha miaka sita. Huu ni ukweli usiofichika hata kipofu atatambua uonevu wa wazi unaofanywa na Serikali yako kwa mikoa ya Rukwa, Kigoma, Tabora na Singida. Naomba maelezo ya kuridhisha la sivyo naomba ruksa yako nimpelekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania takwimu hizi ili labda yeye atoe uamzi juu ya jambo hili kwani kwa kipindi cha miaka kumi Ofisi yako imeona inafanya haki kabisa kutunyima sisi fedha za maendeleo wakati wengine wanapewa mabilioni nataka kufanya hivyo ili njitekeleze ahadi yangu ya mwaka jana. Rejea Hansard hoja ya bajeti 2002.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuingia katika Bunge hili, na pili nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kutupokea Wabunge wapya sote bila ya usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, kwa kutupongeza na sisi Wabunge wa *CUF* bila ya upendeleo kama wanavyofanya Wabunge wengine wa CCM kwani nimejifunza tokea niingie Bungeni kuna Wabunge wa CCM wanaona jeuri kuitaja *CUF.*

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia katika hotuba yenyewe, kwanza ninaanza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(NEC).*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa kuwa Tume ya Uchaguzi ni chombo muhimu sana katika demokrasia ya nchi, hasa inayofuata mfumo wa vyama vingi, kwa hiyo Tume yetu sisi ambayo inatumika hivi sasa, mimi naona ifanyiwe marekebisho ili iendane na nchi ambayo inafuata mfumo wa vyama vingi, kwa nini nikasema hivi nasema hivi kwa sababu viongozi wote wa Tume waliopo hivi sasa wamechaguliwa na Mheshimiwa Rais tu hakuna wanaotoka kwenye vyama vya siasa wala wanaotoka

sehemu za Sekta binafsi wote ni watu waliotoka kwenye Serikali kwa hivyo basi mimi naona hawa hawawezi kutenda haki lazima watapendelea chama cha Rais ndiye aliyewaweka

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watendaji wa Tume nao vile vile walipo hivi sasa na wao hawafai kwani wasimamizi wa uchaguzi wa Wilaya wanakuwa ni Afisa Tawala au Wakurugenzi wa Miji watu ambao ni wafanyakazi wa Serikali na wao hawawezi kutenda haki vile vile, ikiwa tumekusudia kweli tuwe na nchi yenye demokraia ya kweli basi wote humu mufanyiwe marekebisho. Nafasi hizo zitangazwe wazi na waombe watu waliokuwa si watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi wa Vijiji pamoja na vitongoji nao pia uhamishwe kwenye Wizara ya Waziri Mkuu na upelekwe kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi na wafanyakazi wake nao wachaguliwe kwa kuomba nafasi kwenye Tume na utaratibu huu unaotumika hivi sasa haufai.

Mheshimiwa Spika, pili naomba kuchangia katika matukio ya maafa, nieleze masikitoko yangu kwa Mheshimiwa Waziri kwamba nasikitika katika hotuba yake alipozungumzia kuhusu maafa hakutaja kabisa maafa ya tarehe 27/1/2001 ambayo yalifanywa kule Visiwani (Zanzibar) na zaidi katika kisiwa cha Pemba katika jimbo langu la Micheweni, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametaja maafa ya matetemeko ya ardhi, vimbunga pamoja na ajali ya gani moshi, lakini huku hakutaja kabisa, wakati katika muafaka matukio hayo ya maafa tayari yamekwisha undiwa Tume na Tume tayari imekwisha vikisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais na yeye ameshaitangaza hadharani. Suala je, wale waliouliwa na kujeruhuwa na kunajisiwa kule Zanzibar hawana haki ya kupewa fidia kama Watanzania wengine wanavyofanyiwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba jibu wakati utakapo jibu hoja za Wizara yako. Kuhusu vyombo vya habari navyo havitendi haki kabisa si *TV* wala Redio vyote vinapendelea chama tawala. Na wakati tumekubaliana ni vyombo vya umma kwa hivyo vitoe huduma kwa wadau wote si hivyo tu magazeti nayo hivyo hivyo, kwa mfano ni hivi karibuni tu tuliwaita waandishi wa habari hapa Bungeni kwa aijli ya kuitangaza kambi yetu ya upinzani Bungeni lakini magazeti ya Tanzania habari yetu waliziweka katika ukurasa wa ndani hakuna gazeti lililoandika kwa herufi kubwa kurasa za mbele.

Mheshimiwa Spika, hivi vyombo vya umma kama TVT na Redio Tanzajia na vitutendee haki kwani vinakula fedha za kodi za wananchi wote. Kwako naomba unifikie hapa kwa mara ya mwanzo. Ahsante sana.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ndefu iliyofafanua na kuweka mambo mengi bayana. Namsifu kwa uwezo wake wa kusoma huku akinywa maji kidogo kidogo na kumudu kumaliza kurasa 76 bila sauti kutetereka.

Kwa kuwa Ofisi ya Waziri ni mratibu wa shughuli zote za Seriklai ninaomba nizungumzie suala la umaskini. Nchi yetu ni maskini na wananchi wake ni maskini sana

(asilimia kubwa). Umaskini una vigezo vingi, kukosa elimu, kukosa huduma za afya, miundo mbinu duni ya usafiri. Kukosa nyumba bora, chakula bora, mavazi bora na kadhalika.

Tunashukuru Serikali kwamba imeweka mikakati ya kuhakikisha kuwa watoto wotre wanapata angalau elimu ya Msingi huduma za afya zinaboreshwa na hata barabara kuu na zile za vijijini zinatengenezwa. Lakini nina hakika Serikali haitaweza kuwagawia watu fedha ili kumaliza matatizo yao. Ni lazima wafanye kazi kwa bidii na maarifa ili kuweza kukidhi mahitaji yao. Wapo baadhi ya watu hawapendi kufanya kazi na hasa vijana. Kilimo ni sekta ambayo inayoweza kuajiri watu wengi lakini vijana hawaipendi. Serikali ni lazima iunde mkakati wa kuwalazimisha watu kufanya kazi kwa bidii na kwa maarifa ili kila mmoja binafsi aweze kutatua matatizo yake binafsi. Kwa kuwa maafisa watendajni wa vijiji na wa Kata wataajiriwa na Serikali na shughuli ya ukusanyaji wa kodi ya maendeleo imeondolewa nashauri kwamba watendaji hawa wasimamie maendeleo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watu wote hasa vijana wanafanya kazi. Ni jambo la kawaida kuwakuta watu wakinywa pombe tangu asubuhi hadi jioni. Watendaji wa Kata lazima wadhibiti hali hii. Uwepo mpango wa kazi kuanzia kaya-kijiji-kata na kadhalika na mipango hiyo itekelezwe. Bila hivyo umaskini utaendelea kutuelemea. Vitabu vitakatifu vimesisitiza umuhimu wa kila mtu kufanya kazi na adhabu ya mtu asiyefanya kazi ni kwamba asile. Vitabu hivyo vinasema ufanye kazi kana kwamba hutakufa lakini pia wakati unaposali usali kasna kwamba unakufa dakika hiyo.

Ufike wakati wa kutooneana haya au kuogopana ikibidi watu walazimishwe na sheria kufanya kazi vinginevyo mwaka 2005 utafika na watu bado wanaishi katika nyumba za tembe au ngondamo katika maeneo mengine. Huo ndio ushauri wangu. Naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

1. Suala la ubora wa mazao kwa masoko ya nje ni la muhimu sana hasa kwa mazao ya biashara. Ili mafanikio yaweze kufikiwa kwa haraka, wakulima wahamasishwe kuanzisha na kujiunga katika vikundi vya uzalishaji. Wahisani wengi wanapenda kufanya kazi na kusaidia vikundi au vyama vya ushirika kwa kutoa pembejeo, elimu ya kilimo bora na miundombinu mbalimbali. Kwa kuwa ubora wa mazao ndio unaozingatiwa sana katika soko, nashauri fedha ya *STABEX* itakapotolewa, nik vizuri kipaumbele kielekezwe kwenye miradi au *programs* zinazolenga kuboresha mazao hasa ya biashara kama kahawa.

2. Napenda kupongeza kazi nzuri inayofanywa na mradi wa Huduma za Fedha vijijini *(Rural Financial Services)* katika kufufua na kujenga uelewa miongoni mwa viongozi wa *SACCOS* na *SACCAS.* Kwa kuwa mradi huu unalenga kurudisha nguvu ya Vyama vya Akiba na Mikopo ambayo ni nguzo muhimu sana katika kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi wetu. Nashauri mradi huu usambazwe katika Wilaya zote hasa

zilizoanzishwa *SACCOS* nyingi na zikalegalega kwa kukosa uongozi wenye uadilifu hasa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Arusha. Kuna mabadilko ambayo yameanza kuonekana katika *SACCOS* zinazohudumiwa na mradi huu katika Wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro. Yapo matumaini makubwa ya kufufua upya *SACCOS*.

3. Uhusiano wa kimataifa kati ya nchi ya Malawi na Tanzania hivi sasa ni mzuri kinyume na miaka ya 70 ambayo kiongozi mmoja wa Malawi alidai kuwa Watanzania wote waishio kando kando mwa Ziwa Nyasa ni Wamalawi. Ilijitokeza hali ya kutoelewana. Hivi karibuni kumejitokeza hata ramani nyingi za Afrika zinazotolewa sasa zinaonyesha mpaka wa Tanzania na Malawi upo kandokando mwa Ziwa Nyasa upande wa Tanzania ikiacha Ziwa lote upande wa Malawi. Ni vizuri Serikali yetu sasa ianze kuzungumza na wenzetu hasa kwa wakati huu ambao kuna amani kati yetu. Kizazi kijacho kinatakiwa kuelewa uhakika wa mipaka yetu.

Baada ya ushauri huo mfupi, naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu asilimia mia.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake wote wawili kwa pamoja wakishirikiana na Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na wataalam wao wote kwa kushirikiana pamoja na kuandaa Bajeti yao kwa ufanisi zaidi hasa ikizingatia Wizara hio ndio Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru kwa kuzingatia ujenzi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar ambayo ni muhimu sana kwani ni miongoni mwa Ofisi mbili ndogo za Bunge ndani ya nchi hii, ukweli Ofisi iliopo sasa haina hata hadhi ya kuitwa Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, suala la wakimbizi ni tatizo kubwa katika nchi yetu na ni suala ambalo kwa upande wa nchi yetu hivi saa limekuwa kero na ni chanzo kikubwa cha uhalifu na ujambazi ndani ya nchi yetu kwani imebainika kuwa silaha nyingi zinazofanyiwa uhalifu na ujambazi zinatoka nchi jirani ambako wenzetu mpaka hii leo wanaendelea na vita ambavyo haijulikani vitamalizika lini. Kwa hilo uamzi wa Serikali kuamua kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao ili tuondokane na mizigo ambayo haitusaidii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo kwa wananchi wetu ukweli ni muhimu sana kuwapatia wananchi wetu hasa tukizingatia kuwa wengi wa watu wetu ni maskini sana tunapowapatia mikopo ilio nafuu wataweza kujiendesha katika maisha yao na kujikwamua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kupambana na madawa ya kulevya ni uamuzi sahihi Serikali kwa nguvu zake zote kuamua kulipiga vita, lakini nasema bado Serikali haijatafuta chanzo cha tatizo hili kwa makini kwani hao wote wanaokamatwa ni samaki wadogo wadogo kwani naamini kazi hizo kutokana na thamani yake ni lazima mtu awe na uwezo wa kifedha wa kutosha sana hawa ndugu zetu wanaokamatwa kila siku mimi

naamini ni Agent wadogo tu sasa tutafute chanzo ili tuwapate hao wahusika wakubwa ndipo tutakapo kimaliza na kulitokomeza kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja hii asilimia moja 100%. Ahsante.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wasaidizi wake kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa maendeleo ya Watanzania. Na hivyo naunga mkono hotuba hiyo mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha mchango wangu kama ifuatavyo:-

1. Utawala Bora unawahusu watu/wananchi watumishi na viongozi na kwamba Mahakimu kama ndio hutoa haki kisheria kwa kesi zinazofikishwa mbele yao. Kwa nini kesi huchukua miaka zaidi ya mitatu bila kutolewa hukumu na kuathiri maisha ya watuhumiwa? Na ukitaka kujua sababu gani zinacheleweshwa kesi hizo, maneno ya jumla ni kwamba "Mahakama haiingiliwi". Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili lirekebishwe ili ukweli wa utawala bora udhihirike kwa wananchi na watumishi. Kwa sababu kesi ya watumishi wa *TTCL* ipo Mahakamani muda mrefu na familia zinateseka. Katika kesi hii ya watumishi wa *TTCL* haina kufanya upelelezi kwa Polisi, kinachotakiwa ni kujua kuwa watumishi wanastahili au hawastahili basi Hakimu atoe hukumu ili watumishi hao wajue la kufanya kwa maisha yao.

2. Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba upanuzi wa barabara ni nzuri lakini utekelezaji wa *TANROAD* unaleta kero kubwa kwa wananchi wanaobomolewa nyumba zao bila kulipwa fidia. Wananchi wanajua *TANROAD* imeanzishwa mwaka 2000 na kwamba masuala ya huko nyuma hawajui. Enzi ya *PWD* upana halali wa barabara hadi unapostahili kujenga nyumba bila kukiuka utaratibu ni mita 15 na siyo mita 22.5 kama wanavyofanya *TANROAD.* Sasa kwa nini Serikali inakubali dhuluma kwa wananchi wake? Mimi nashauri waliobomolewa nyumba zao sehemu za Mbagala hadi Kongowe walipwe fidia na wasiyumbishwe mara nenda kwa *DC,* mara *TANROAD,* mara *RC.* Ni busara kuwapa lugha nzuri na yenye mwelekeo wa matumaini. Tatizo hili litaleta chuki kati ya wananchi na Serikali yetu ya CCM na hasa kipindi cha uchaguzi wa vitongoji na mitaa 2004 kwa Wilaya-Temeke.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Serikali kufuta kodi ya maendeleo na kodi zingine zilizokuwa zinatozwa na Halmashauri, wananchi wamefurahi sana. Sasa bado upande wa viongozi wenzetu (Madiwani) wamekuwa duni kimaisha. Hawana uwezo wa kununua gari wala pikipiki, kutokana na posho duni wanazolipwa wakati wa vikao vyao. Mimi nashauri Serikali ipange malipo ya posho kwa kima sawa kwa madiwani wote nchini na kwa njia hiyo watakuwa na uwezo wa kukopa gari au pikipiki. Tukiwaimarisha Waheshimiwa Madiwani kwa jumla nchi nzima, chaguzi zetu za Urais, Ubunge, Udiwani na kadhalika, utakuwa hauna mvutano. Kwa sababu kila mmoja wa nafasi hizo analipwa posho nzuri na mikopo ya vyombo vya usafiri na kadhalika.

Baada ya maelezo hayo machache narudia tena kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye matumaini kwa wananchi wa Tanzania.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

(i) Mabonde yote ya umwagiliaji yatumiwe vizuri kwa kilimo cha umwagiliaji ili kuondokana na tatizo la njaa nchi yetu ina mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

(ii) Sekta ya Mifugo: Kwa kuwa sekta ya Mifugo inachangia pato la Taifa hivyo nashauri ufugaji wetu uboreshwe ili mifugo hiyo iwe bora na kuchangia pato la Taifa. Serikali iimarishe vituo vya utafiti wa Mifugo kikiwamo Kituo cha Utafiti wa mifugo cha Mpwapwa. Kituo cha utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa kilianza tangu 1905 na ndicho kituo cha kwanza cha utafiti wa mifugo hapa nchini, hivyo naishauri Serikali wakati umefika sasa kituo hicho kipandishwe hadhi na kuwa kituo cha utafiti wa mifugo cha Mpwapwa kipewe hadhi ya kitaifa - *National Livestock Research and Development Centre* ili kihudumie nchi nzima badala ya kuhudumia Kanda tu. Serikali isaidie ukarabati wa majiosho. Halmashauri za Wilaya uwezo wake ni mdogo.

(ii) Sekta ya Afya: Serikali ihakikishe inatatua tatizo la upungufu wa watumishi katika hospitali za Mikoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Kila hospitali ya Wilaya iwe na wataalam wafuatao:-

- *Physicians;*
- *Dentist;*
- *Paedetrician;*
- *Gynacologist;*
- *Eye Specialist.*

Mheshimiwa Spika, wataalam hawa wakiwepo wataboresha huduma za afya katika hospitali zetu za Wilaya kuhusu Idara ya Afya, Tiba. Kuhakikisha kwamba vituo vya afya na zahanati zote wanapatiwa darubini kwa ajili ya kuchunguza magonjwa, Maabara ziimarishwe katika vituo hivyo, hivi sasa zahanati nyingi hakuna darubini.

Kwa kuwa barabara nyingi za vijijini ni mbaya sana na huko vijijini ndiko kunakozalishwa mazao ya chakula na biashara basi Serikali itenge fedha za kutosha za kutengeneza barabara hizo. Bado nashauri *fuel levy - 30%* inatengwa kwa ajili kutengeneza barabara vijijini ni kidogo sana. Nashauri Serikali ichukue 60% na Halmashauri za Wilaya 40% badala ya 30%. Barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa-Lupeta, hadi Mlali hadi Pandambili itengenezwe na itengewe fedha za kutosha.

*CDA* - Uhamiaji Makao Makuu Dodoma, napongeza juhudi zinazofanywa na Serikali za kuhamia Dodoma hata hivyo fedha za kutosha zitenge kwa ajili ya kuhamia Dodoma. Wizara zingine zihamie Dodoma. Naunga mkono hoja hii asilimia 100.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika. Kwanza kabisa nachukua fursa hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili ambao wapo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi wanavyojitahidi kuwajibika katika nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, mimi mwanzo wa mchango wangu ni kuhusu suala la ufuatiliaji wa balaa la njaa nchini takribani ni kuwapo kwa askiba ya chakula nchini ni muhimu sana, hii itasaidia sana watu wetu kufikia kula mizizi ya miti nadhani si sahihi itakuwa vizuri kama nitathibitishiwa wale watu wa Bagamoyo waliofikia hatua hiyo walisaidia vipi na waliathirika kiasi gani.

Pili Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu hivi sasa itekeleze majukumu yake zaidi kwa vitendo hasa katika masuala ya ujambazi kwa kutumia mbinu ya kuimarisha sungu sungu wa mitaa yote husika na zaidi ziwepo mbinu mahsusi za motisha kwa watakaobainisha kutoa habari mapema kuliko kuambiwa maafa. Kwani nina hakika ndani ya mitaa yetu, vijana walio wengi wahafahamu kila kitu ila tu ukosefu wa kuwahamasisha ndio haupo. Juu ya vita dhidi ya UKIMWI, si vibaya kuiga yale mambo mazuri hivyo tusome kwa majirani zetu wa Uganda walivyo-*improve* katika kiwango cha sifa kubwa katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka huu watu wote wa itikadi mbalimbali wameiunga mkono hotuba ile kwa asilimia zote, hii imetuletea sifa kubwa kwa chama chetu, baraza la Mawaziri, na Watalaam wetu. Lakini tutafedheheka sana kama matakwa ya bajeti hii hayatatekelezwa hivyo naomba kama Ofisi ya Waziri Mkuu ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali awe anafuatilia kwa kupata ripoti ya utekelezaji wa maazimio kila baada ya miezi mitatu ili mwisho wetu mipango ya mwaka uwendane na matumaini ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge usitupeleke pahali pabaya, nadhani ukweli lazima uelezwe bayana kwani Wabunge ni sehemu muhimu ya mhimili hivyo wangepaswa waelezwe kama upo uwezekano au hapana kwa muda huu na ni lini matarajio ya Serikali kushughulikia suala hilo tofauti na ahadi nyingi na zenye matumaini hewa.

Mheshimiwa Spika, lazima Mheshimiwa Waziri Mkuu afanye jitihada za lazima kubadilisha majengo ya nyumba za polisi kwani nyumba hizo hazifai hata kuwa mahabusu kwani sio tu kupitwa na wakati lakini hazifai hata kuonekana kwa macho katika bajeti iliyopita, uhuru wake takriban miaka arobaini iliyopita.

Napenda pia kutoa rai kwa Waziri Mkuu kuwa mwangalifu sana na kauli za wanasiasa baadhi, kwani wengine hutaka kuonyesha ubabe kuliko Serikali kwa vitisho

vipi kama kiongozi kusema “Naweza kufanya jambo kuwa gumu na ikibidi nchi isiweze kutawalika”, hayo matashio lazima yajibiwe haraka vinginevyo wao ndio wataonekana ni dola wakati wao bado wapo benchi hivyo lazima waelekezwe nini maana ya utawala bora na wasihisi kwamba utawala bora usimamiwe na chama tawala tu bali hata wao wanapaswa kutanguliza lugha bora kabla hawajapata kutawala.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, binafsi Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimpongeze kwa kukomaa kwake kisiasa kwani Waswahili wanasema mkubwa jaa, hivyo wapinzani kumtupia shutuma na yeye kuendelea tu na kuchapa kazi ndio sulubu, hivyo mwisho watachoka na kuanza kuunga mkono hoja za Serikali moja baada ya nyingine, mwisho kabisa naomba ampokee ndugu Sanare na ampe mashirikiano yote ili aonyeshe uzoefu wake wa kuwatumikia Watanzania kama alivyozoea ahsante.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa pongezi kwa Wabunge wapya, walioingia katika Bunge lako tukufu kwa kipindi hiki cha Bajeti hasa wale walioingia kwa tiketi ya CCM.

Kabla sijatoa mchango wangu, ninaomba kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa hekima na busara nyingi kwa Watanzania wote. Naomba nianze kuchangia kuhusu Wabunge wa Bunge la Juumuiya ya Afrika Mashariki ambao wanapigiwa kura na Bunge lako tukufu. Kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge Wabunge hao hulazimika kutoa taarifa ya utendaji wa majukumu yao katika Bnge hili kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje. Napendekeza kuwa wakati taarifa inayohusu utendaji na shughuli zao inapojadiliwa na Bunge kupitia Kamati yetu ya Nje, Wabunge hao wawe ndani ya ukumbi, ili wasikilize, na hili linawezekana kwa kutumia ule utaratibu wa kutengua Kanuni zetu kama ilivyo kawaida ya Bunge hili. Naomba nimalizie mchango wangu kwa kuzungumzia kuhusu wajumbe wa Bunge ibara ya 66 ya Katiba. Ibara hiyo inaelezea kuhusu aina ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, moja ya aina ya Wabunge ni wale Wabunge watano wanaochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwao Ibara ya 66 (c). Wakati aina nyingine za Wabunge zimekuwa zikiongezeka kila wakati, ikiwa ni pamoja na ile aina ya Wabunge wa Majimbo na wale wa viti maalum. Lakini idadi ya Wabunge waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi imebakia kuwa ile ile. Hivyo pendekezo langu kuwa “ongezeko kuhusu aina hii ya Wabunge lifikiriwe hasa mwaka 2005”.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kusema kuwa naunga hoja hii mkono asilimia mia moja bila matatizo. Naomba nimpongeze Waziri Mkuu na Mawaziri waliopo katika Ofisi yake kwa bajeti yenye matumaini mengi.

Naomba nichangie katika swali moja muhimu ambalo sasa hivi tunalitilia mkazo sana, nalo sio lingine ila ni ardhi. Sasa ni mali na jinsi tutakavyoona baadaye kila mahali sasa watu vijijini wameshatambua kuwa ardhi ni rasilimali sasa. Tatizo langu likko

kwenye mipaka ya vijiji na vijiji Kata na Kata, Wilaya na Wilaya na hata Mkoa na Koa. Katika sehemu nyingi sasa watu wanagombea mipaka. Hivi tangu wakati wote hapakuwa na mipaka? Katika sehemu nyingine mawe yanamewekwa upya, mbaya zaidi ni pale upande mwingine unapofanya hiyo bila kushirikisha upande wa pili.

Katika vijiji vya Singida Mjini na Singida Vijijini tatizo hili lipo na kila siku linazidi kuwa kubwa. Inaonekana uongozi wa Wilaya bado haujaona kuwa ni tatizo na hivyo kulipa umuhimu wa pekee kwa kulitatua. Naomba mahali popote palipo na matatizo ya ardhi yasitolewe majibu rahisi ila patafutiwe suluhisho la kudumu ambalo litaepusha kuvunjika kwa amani. Ili kuweka matumizi bora ya ardhi ni lazima watu wajue kiasi ya ardhi walio nayo katika kijiji chao. Tafadhali hili tatizo lishughulikiwe kila Wilaya.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji makini wa hotuba yake. Aidha, nimpongeze pamoja na wataalam wa Ofisi yake kwa maandalizi mazuri ya Bajeti hii.

Napenda kuchangia jambo moja tu nalo ni ujenzi na uimarishaji wa Ofisi za Wabunge Majimboni mwao.

Napendekeza kuwepo na Makatibu wa Bunge wa Majimbo ambao wataajiwa moja kwa moja na Ofisi ya Bunge Dodoma ingawa wataishi Majimboni. Makatibu hawa watakuwa ndio walinzi wa mali za Bunge ambazo Serikali inaendelea kuziweka katika Ofisi za Majimbo kwa niaba ya Katibu wa Bunge. Makatibu hawa wa Majimbo wawe wanaweza kuhamishwa kutoka Jimbo moja hadi Jimbo au kupelekwa Makao Makuu ya Bunge Dodoma kwa kadri Ofisi ya Spika itakavyoona inafaa. Utaratibu wa kuajiri Makatibu hawa utaiwezesha Ofisi ya Spika kuwa karibu na wananchi kiutendaji wa Bunge ndani ya Jamii. Hawa Makatibu watakuwa ndio wataalam wa dhana ya uwakilishi wa Bunge. Wabunge ni wanasisasa na huingia na kutoka Majimboni kwa vipindi lakini *presence* ya Mahakama Serikali na Bunge lazima vyote vitakuwepo kwa utaratibu wa kudumu Vijijini. Mbunge si mtaalam, bali ni mwanasiasa wakati Serikali na Mahakama zina uwakilishi wa kitaalam na kudumu huko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, makatibu wa Majimbo watawasaidia sana Wabunge wapya kuhusu taratibu za kibunge Majimboni.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na kuunga mkono hoja yake mia kwa mia. Namtakia kila la kheri katika utendaji wake mzuri.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo imeandaliwa kwa umahiri mkubwa sana. Pongezi hizi pia ziwafikie Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Siasa na Habari) pamoja na Watendaji wote ambao walishiriki katika maandalizi ya hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na uamuzi wa Serikali kwa kuanza ujenzi wa Ukumbi mpya na wa Kisasa wa Bunge Mjini Dodoma. Lakini hata hivyo kasi ya kuhamia Dodoma hasa upande wa Serikali ni ndogo na inakatisha tamaa. Inaelekea wapo watu ambao hawapendi kuhamia Dodoma. Ili kuharakisha zoezi hilo nashauri Serikali iache badala yake ianze kujenga Dodoma kwa kuanzia Ofisi ya Wizara ya Fedha, ingekuwa moja ya Ofisi hizo pamoja na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kuwapa changamoto Mabalozi nao kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na zoezi la Serikali kuuza nyumba za Serikali na kujenga mpya, basi Serikali ijenge nyumba hizo Dodoma badala ya kuendelea kujenga nyumba za watumishi Dar es Salaam kama inavyofanyika sasa. Nashauri Serikali iweke programu itakayoonyesha hatua mbalimbali za kukamilisha zoezi la kuhamia Makao Makuu kwa kuzingatia muda *(time frame).*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2002 yametoa picha kuhusu matatizo yanayowakabili baadhi ya Wabunge katika uwakilishi wao. Yapo Majimbo ya Uchaguzi ambayo hayafikiki kiurahisi lakini vile vile yana watu wengi. Inapofika kuhudumia Jimbo, gharama zinakuwa sawa yaani Mbunge anayewakilisha eneo kubwa na watu wengi na yule anayewakilisha eneo dogo na watu wachache analipwa kiasi kile kile na matokeo ya utaratibu huu ni kuwanyima baadhi ya wananchi kuwakilishwa vizuri. Nashauri Serikali iangalie namna ya kuwa na usawa katika kugawa Majimbo kwa lengo la kuwatendea haki wananchi. Tume ya uchaguzi ingetembelea Majimbo yake yenye watu wengi, eneo kubwa na suafiri wa shida ili kutoa maelekezo ya uwezekano wa kugawa Majimbo bila upendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na magazeti lukuki, *radio* na televisheni, habari zinazosikika zaidi ni mambo ya viongozi na wakazi wa Mijini. Bado mambo yanayotendeka Vijijini hayaripotiwi na Waandishi wa Habari kwa sababu ya uduni wa mawasiliano. Upo mtindo ambao ni hatari kwa uhuru wa Waandishi kwamba, gharama za kumgharamia Mwandishi wa Habari hutolewa na yule ambaye anapenda taarifa au habari zake zitangazwe. Matokeo yake ni taarifa nzuri tu zitatangazwa katika mazingira kama haya. Nashauri suala hili liangaliwe ili kuona namna gani Waandishi wa Habari watatoa taarifa sahihi bila upendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbinga inao wakazi zaidi ya laki nne. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Mwandishi wa Habari katika Wilaya hiyo?

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini hasa vurugu za nchi za Kongo si suala la kupongeza. Hali ni mbaya hata mikataba ambayo inatiwa saini ni njia ya kuahirisha matatizo yanayowasibu watu wa Kongo. Kiini cha matatizo ya watu wa Kongo bado ni kitendawili. Ipo haja ya kujifunza zaidi hali halisi ya Kongo na majirani ambao lengo lao ni kugawana utajiri wa Kongo na hatimaye kurejesha ukoloni mamboleo. Ujambazi unaoendelea hapa nchini hauwezi ukachukuliwa kama ni uhalifu wa kawaida. Ni budi utafiti wa kina ufanyike ili kuwa na uhakika kuwa mauaji yanayojitokeza si njama za maadui za kutingiza amani na utulivu uliopo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkongo hoja hii mia kwa mia kwa kutoa shukrani zangu binafsi na za wananchi wa Mbinga Mashariki kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kututembela hapo tarehe 23 Mei, 2003. Tumefarijika sana kwa ujio wake, hasa ikizingatiwa kwamba moja ya kero ambazo zimekuwa pingamizi la maendeleo zimepatiwa ufumbuzi mara moja. Kero hizi ni pembejeo ya kilimo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mawaziri Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Seif Khatib, Katibu Mkuu, Bibi Rose Lugembe, bila kuwasahau wataalam wao kwa kazi nzuri ya kuandaa Bajeti yenye mtazamo wa kiutekelezaji thabiti wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2003/2004.

Baada ya pongezi hizo, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Katika ukurasa wa saba kuna suala la ujenzi wa ukumbi mpya wa kisasa wa Bunge, kuanza kujengwa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuona kuwa Serikali imepania kuboresha mazingira ya kukutania Wabunge ila ninashauri kuwa Ukumbi mpya uzingatie mahitaji maalum kwa Waheshimiwa Wabunge wenye ulemavu na wananchi wenye ulemavu ambao watajaliwa kutumia ukumbi huo. Mathalan ngazi zisiwepo katika sehemu zote za kuingilia ukumbini, pawe na vyoo maalum angalau viwili na mahitaji yoyote mengine ambayo wasanifu majengo wanayafahamu.

Suala lingine katika ukurasa wa 16 ni kuhusu mikopo inavyotolewa na Serikali kwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ambayo hukopeshwa wanawake na vijana kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, fedha za mikopo hii huchangiwa na Wizara husika na Halmashauri za Wilaya. Lakini inaelekea Halmashauri nyingi hazichangii kabisa au zinachangia pungufu na asilimia tano ya makusanyo ya fedha kila mwaka kwa kila mfuko. Kwa msingi huo, ingawa Mheshimiwa Waziri Mkuu amewakumbusha Watendaji wa Halmashauri lakini utekelezaji wake umekua mdogo mpaka sasa. Hivyo labda ubuniwe utaratibu mpya utakaoweza kuwahimiza Wakurugenzi kuchangia kikamilifu katika mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo Halmashauri chache tu ndiyo zina utaratibu wa kuhamasisha vikundi vya wanawake na vijana wenye ulemavu vya uzalishaji mali kuundwa na kuvipatia mikopo kwa ajili ya kuongeza mtaji wa shughuli zao. Sasa kwa vile watu wenye ulemavu walio wengi ndio maskini zaidi humu nchini, ninashauri Wizara husika ziweke msukumo zaidi katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu nao wanawezeshwa kwa kupatiwa mikopo hiyo kama inavyokuwa kwa jamii ambayo si walemavu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 65 limezungumziwa suala kuhusu vita dhidi ya Ukimwi. Pamoja na kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zimejengewa uwezo wa kusimamia na kudhibiti kuenea kwa Ukimwi katika maeneo yao, lakini hali ilivyo ni kwamba katika kuandaa programu za kudhibiti Ukimwi watu wenye ulemavu hawahusishwi wala kushiriki kama wadau katika maeneo hayo. Kwa msingi huo, watu wenye ulemavu walio wengi huachwa bila taarifa muhimu kuwanazo kuhusu Ukimwi.

Hivyo wanaweza wakawa ni miongoni mwa waathirika, ikizingatiwa kuwa kundi hili lina mahitaji maalum ambayo yanapaswa kutolewa ndipo liweze kupata taarifa husika. Kwa mfano watu wasioona wanapaswa kuelimishwa kwa mbinu maalum za kuwawezesha kutambua (kupapasa) kondomu salama; viziwi wanapaswa kuelimishwa kwa kutumia wakalimani wa lugha ya alama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, ni kwa kiasi gani Mamlaka za Serikali za Mitaa ziko *aware* na mahitaji kama haya? Hivyo ninashauri *TACAIDS* itoe maelekezo kwa hizo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu jinsi gani ya kutoa elimu ya Ukimwi kwa watu wenye ulemavu wa aina tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ushauri huo, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu katika kujadili hotuba ya Waziri Mkuu katika mambo mawili. Kwanza Ukimwi na pili, ombi la kuigawa Wilaya ya Kilosa. Lakini kwanza kubwa, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, janga la Ukimwi linaendelea kuwa tishio kubwa kwa maisha ya Watanzania na ni kikwazo kwa maendeleo ya Taifa kwa kuangamiza idadi kubwa ya nguvu kazi ya Taifa. Pamoja na juhudi zote zilizochukuliwa katika kupambana na Ukimwi tangu mwaka 1985 ulipoanzishwa mpango wa kwanza wa Taifa kupambana na Ukimwi, kasi ya maambukizo bado haijapungua isipokuwa katika sehemu chache.

Nionavyo mimi, iko haja ya kubadili mkakati mzima na mbinu zinazostahili kutumiwa kupunguza maambukizo na kutumia mafunzo yaliyopatikana katika maeneo ambayo yameonyesha mafanikio ya kupunguza kasi ya kuenea kwa Ukimwi kwa mfano katika Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, Wilaya za Muleba na Bukoba Vijijini katika Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Magu katika Mkoa wa Mwanza. Vile vile, ile haja ya kujifunza na kutumia mbinu zilizowezesha nchi ya Uganda kupata mafanikio na kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizo ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi (VVU/UKIMWI)

Hivi sasa njia zote za maambukizo zinajulikana na hatua zinazostahili kuchukuliwa kupunguza au kuzuia maambuziko zinajulikana ikiwa ni pamoja na matumizi thabiti na sahihi kwa kila tendo la kujamiiana au ngono. La msingi kabisa ni kwamba, hatua zinazostahili kuchukuliwa zilingane na ukubwa wa tatizo. Ukimwi umekwishatamkwa kuwa ni janga la Taifa na mapambano dhidi ya Ukimwi ni vita. Kwa maana hiyo, mapambano dhidi ya Ukimwi lazima yawe katika hali ya vita. Hivyo basi hatua zote zinazostahili kuchukuliwa zichukuliwe kwa dhati na kwa nguvu zote na kwa

haraka katika maeneo yote bila kuchelewa na hatua hizo ziendane na kutengwa fedha za kutosha kutekeleza sera muafaka ambayo tayari ipo, uongozi imara wa kisiasa na ushiriki wa dhati wa umma.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa ni kwamba, hatuonyeshi msukumo wa kufanya mambo kwa hima na haraka. Tumechelewa sana kufanya Wilaya na jamii Vijijini kwenye Kata na Tarafa kuwa ndio uwanja wa mapambano na kutenga fedha za kutosha kutumiwa Wilayani na katika jamii. Dalili iliyo wazi ni kiasi cha fedha zilizotengwa katika Bajeti ya *TACAIDS* ya mwaka 2003/2004 Sh. 999,528,105/= ndizo zilizopangiwa kutumiwa kwa vifungu vyote kwenye Wilaya na jamii ambayo Sh.3,295,453,895/= zimetengwa kwa vifungu vyote kutumiwa kwenye Makao Makuu na Idara zake. Idadi kubwa ya Watanzania wako Vijijini. Nguvu na juhudi kubwa zielekezwe Wilayani na fedha nyingi zaidi sharti zipangwe kutumiwa Wilayani na Vijijini zaidi ya ilivyo kwenye Bajeti. Kinachotakiwa ni kuwa na *Intesndified District Response.*

Mheshimiwa Spika, bado wananchi Vijijini hawajashirikishwa vya kutosha, hawajahamasishwa vya kutosha na kupatiwa fedha za kutosha kupanga mipango yao Vijijini na katika Kata. Vijijini ndiko tutakakogundua Mila na Desturi zinazosaidia kuenea kwa ugonjwa na kudhoofisha juhudi za kupambana na Ukimwi. Vijijini wananchi wanastahili kupambana katika vikundi kupatiwa elimu shirikishi kwa mtindo uliotumiwa katika kampeni ya "Mtu ni Afya" katika miaka ya 1970 ili waelimishwe, waelimishane na wahamasishwe kutumia njia muafaka kuzuia kuenea ugonjwa wa Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, uongozi katika ngazi zote bado sio imara katika kuratibu juhudi zinazochukuliwa na Serikali, Mashirika yasiyo ya kiserikali, Mashirika ya Dini na watu mbalimbali wanaojitolea katika jamii. Viongozi wa aina zote katika jamii wawajibike na wawajibishwe. Kundi moja linalostahili kuwa mstari wa mbele ni sisi Wabunge tuwezeshwe kwenye Majimbo yetu ya Uchaguzi kwa kuandaliwa Semina, Warsha Vijijini ili tushiriki kwa kushirikiana na makundi yote yanayojishughulisha katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Mashirika yasiyo ya Serikali yametengewa Sh.10,427,184,900/= kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Serikali lazima iratibu kazi zinazofanywa na Mashirika yasiyo ya Serikali na Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Spika, tunapoteza muda mwingi na fedha nyingi katika warsha na semina za kurudiarudia kwa makundi yale yale na watu wale wale wanaoshiriki katika semina na warsha kila wakati na lililo baya zaidi warsha hizo na semina hizo zinaendeshwa zaidi Mijini kuliko Vijijini. Tubadili mtindo huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara zote zinategemewa kuwa na *Technical Committees* kwa ajili ya Ukimwi. Wizara nyingi hazionyeshi kuwa zimeunda Kamati hizo na kuzitengea fedha Ofisi ya Waziri Mkuu ichukue jukumu la kuhimiza Wizara zote za Serikali na Taasisi za Serikali zishiriki kwa ukamilifu katika kudhibiti maambukizo ya VVU/UKIMWI katika sekta zao.

Katika hali halisi tunajau kwamba yapo makundi katika jamii ambayo ndio yako katika hatari kubwa ya kupata maambukizo ya VVR/UKIMWI na ndio yanayochochea kuenea kwa ugonjwa wa Ukimwi. Makundi hayo ni makahaba, wahudumu wa *Bar,* Wanajeshi wa Mejeshi yote, Jeshi la Wanachi, Polisi, Magereza na Uhamiaji; Madreva wanaosafiri kwa magari yanayokwenda masafa marefu katika barabara kuu, wafanyakazi wa migodini, vibarua wa simu kwenye mashamba makubwa, watumiaji wa madawa ya kulevya, wasenge na wanawake kwa ujinsia wao. Makundi haya lazima yabainishwe na tuyaendee makundi haya yashirikishwe kwa dhati kabisa yawe ni sehemu muhimu ya mapambano dhidi ya Ukimwi. Mkakati wa kupeana taarifa, elimu na mafunzo na mawasiliano kama njia mbalimbali *(information, education, communication)* utumike kwa nguvu zote na kwa ukamilifu. Mafunzo ya rika yatumike ili wanarika wahamasishane, waelimishane wenyewe kwa wenyewe kwa kutumia Wafundishaji wa Rika *(Peer Health Educators)* miongoni mwao. Wapatiwe ushauri nasaha ili wawe tayari na wakubali kupimwa damu kugundua VVU. Lengo liwe wabadilike katika miendendo yao ya maisha na tabia zao katika mambo ya kujamiiana kwa kujamiiana kwa njia salama.

Imeonekana wazi kuwa njia inayofaa sana kupunguza au kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Ukimwi katika jamii ni kupunguza kuzuia maambukizo katika makundi hayo.

Ukimwi ni ugonjwa wa vijana hasa kati ya umri wa miaka 15 hadi miaka 39. Watoto wa Shule katika Shule za Msingi na vijana katika Shule za Sekondari na Vijana walio nje ya Shule wanastahili kuwahiwa mapema wasiathirike. Elimu dhidi ya Ukimwi na Elimu ya Maisha, Mafunzo ya Rika, Kamati za Ukimwi Shuleni zinazoshirikisha wazazi na kuwapa walimu, walezi hasa kwa ajili ya wasichana, ni mkakati ambao umeonekana unafaa kuzuia watoto na vijana Shuleni wasiambukizwe VVU/UKIMWI na mkakati huu ukitumika na kutekelezwa kote nchini tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana kuwaepusha vijana wetu walioko shuleni wasiambukizwe.

Mheshimiwa Spika, kwa vijana walio nje ya Shule hawa tuwaendee na kuwahamasisha wajiunge kwenye vikundi. Katika Vikundi vyao vya Uzalishaji Mali, Vikundi vya Sanaa na Vilabu vya Michezo wahamishwe na waelimishwe na washiriki katika Mafunzo ya Rika na wahimizwe wajitokeze kupatiwa ushauri nasaha na wapimwe damu zao. Hatua hizi zitawalinda vijana na kuwaepusha na maambukizo ya VVU/ UKIMWI.

Katika kuzuia maambuziko toka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa mimba, wakati wa mama kujifungua na baada ya mama kujifungua, anaponyonyesha mtoto, naomba Serikali iweke msimamo kwamba wanawake wote wajawazito wanaogundulika kuwa na VVU wapewe *Niverapine* au tiba ya kuuzia virusigeuzi kuzuia watoto wachanga wasiambukizwe VVU/UKIMWI. Dawa hizi zina bei kubwa lakini Serikali ikisaidiwa na Mashirika yasiyo ya Serikali na Mashirika ya kujitolea, inaweza kumudu gharama za kuzipata dawa hizi.

Vifaa vya kupima damu kugundua VVU vinastahili kuenezwa kwenye hospitali zote na Vituo vya Afya vyote nchini na kuhakikisha wataalam wa Maabara wanakuwepo katika sehemu hizo zote. Pia Vijiji ambavyo ni Vituo vya magari yanayosafiri kwa masafa marefu katika barabara kuu kama vile Dumila, Magubike, Gairo, Mikumi na
Kidatu katika Wilaya ya Kilosa na katika Wilaya nyingine, vinastahili navyo viwe na vituo vya kupima damu. Hivyo ndiyo njia ya uhakika ya kuwagundua wenye VVU na wanaostahili kupewa ushauri nasaha wanapogundulika kuwa wameambukizwa VVU waweze kuishi kwa matumaini.

Watu wenye kuishi na VVU/UKIMWI wanastatihili kupatiwa matunzo na misaada ya hali na mali. Unyenyepa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI unastahili kupigwa vita kwa nguvu zote. Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI ni ndugu zetu, jamaa zetu, watoto wetu, baba zetu, dada zetu, kaka zetu na rafiki zetu. Lazima tuwachukulie kuwa ni sehemu ya jamii tuliyonayo sasa. Unyenyepa na ubaguzi utapungua na mwisho kutoweka ikiwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI watashirikishwa kwa ukamilifu katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Wao ndio wenye uelewea wa hali halisi ya kuwa na VVU/UKIMWI na wanaoweza kuwa walimu wazuri na kuielekeza jamii mambo gani ya kufanya kuzuia kuenea kwa maambukizo ya VVU/UKIMWI na jinsi ya kuishi kwa matumaini.

Mheshimiwa Spika, sasa nina ombi moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Wilaya ya Kilosa mapema mwaka huu mwezi Aprili, 2003, katika Mji mdogo wa Gairo, wananchi walitoa ombi kwa Waziri Mkuu la kutaka Wilaya ya Kilosa igawanywe kuwa Wilaya mbili. Kama Mbunge wa Jimbo la Gairo, ninayo heshima ya kukumbusha juu ya ombi hilo. Wilaya ya Kilosa kwa eneo ni kubwa na kwa mandhari ya nchi au topografia ni vigumu kuyafikia maeneo yote kwa urahisi kwa wakati mmoja. Kwa sensa ya mwaka 2002 Wilaya ya Kilosa ina wakazi 489,513 Kata 37 na Tarafa tisa. Maombi ya kuigawa Wilaya ya Kilosa yalikwishafikishwa Serikalini na tayari yapo katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa takrban miaka mitatu sasa. Matumaini yangu na ombi langu kwa niaba ya wananchi ninaowawakilisha Bungeni ni kwamba Serikali italifikiria ombi hilo kwa makini kwa mategemeo kwamba kwa zoezi lolote litakalofanyika kugawa Wilaya, Wilaya ya Kilosa itakuwemo.

Mwisho, narudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Nchi (Sera), Mheshimiwa Seif Khatib, Waziri wa Nchi, (Siasa) na Habari pamoja na Katibu Mkuu Rose Rugembe, kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo. Hatuba hii ina mantiki na inagusa hisia za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuhamia Dodoma ni vizuri tukasema wazi kuwa haiwezekani kuliko kuwa na kigugumizi. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema sasa nimehamia Dodoma. Tukapiga Makofi na vigelegele. Mwaka huu hotuba haizungumzii suala la Dodoma, kulikoni? Kama haiwezekani si tuseme?

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kidogo kuhusu Vyama vya Siasa vinavyovamia Majimbo na kutukana viongozi wa Serikali na Wabunge. Tunaomba hawa Waheshimiwa wawe wastaarabu. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tunao uwezo wa kutembelea Majimbo mengine. Lakini kutukana sio mila wala desturi yetu. Jambo hili ni hatari. Tusisukumwe kufika huko.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza TVT, TT, CTN na Redio Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya. Siwasahau Waandishi wa Habari wanaowakilisha magazeti mbalimbali. Kazi wanayofanya ni kubwa kwa ajli ya ku - *cover Budget Session.*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Watendaji wake kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mambo yote muhimu kama yalivyotolewa katika Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na kutengewa fedha katika bajeti ya Taifa yameguswa kikamilifu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye pia ndio Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali kwa ujumla. Kwa msingi huo basi, kazi kubwa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kusimamia utekelezaji wa mipango yote ya bajeti ya mwaka 2003/2004, bajeti inayoelekeza nguvu zake kuwaelekea walengwa yaani wananchi walio wengi.

Pamoja na uzuri wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado ingekuwa sahihi hotuba hiyo kugusia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Ofisi za Wabunge, kwa kuwa Ofisi ya Spika haitatoa hotuba ya bajeti, basi kwa nafasi ya Ofisi ya Waziri Mkuu ingepaswa kugusia nia ya utekelezaji wa ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo yao, kama ambavyo hatuba hiyo imegusia ujenzi wa Ukumbi mpya wa Bunge. Kwa kuwa tatizo la Ofisi za Wabunge limekuwa kero kuu kwa Wabunge wengi, haingekuwa inatosheleza kutegemea kwamba Ofisi ya TAMISEMI itatoa kauli au mapendekezo ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge bila kuwa na msisitizo kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu malipo ya wazee wapiganaji wa Tanzania wakati wa Vita Kuu ya Dunia kwa Serikali ya kikoloni ya Uingereza. Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndio iliyokuwa mratibu wa malipo ya Askari hao wa vita na kwa kuwa kutokana na matatizo ya uongozi wa chombo cha Wapiganaji hao Serikali ya Uingereza iliamua kusitisha malipo ya Wapiganaji hao na kwa kuwa bado Wapiganaji wengi wanaendelea kufuatilia malipo ya fedha hizo kupitia Ofisi za Wilaya na Mikoa, basi Mheshimiwa Waziri Mkuu angetoa kauli ya mwelekeo wa hali ya malipo ya kufuta machozi kwa Wapiganaji hao kutoka Serikali ya Uingereza. Kwa hali yoyote ile ingekuwa vyema Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kukiri kuwepo kwa madai ya wazee hao na orodha iliyopo Ofisini kwake kimikoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwaka 2003/2004.

**MHE. JANETH E. MASHELE:** Mheshimiwa Spika, kwanza Vituo vya *Television* na Redio, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na kueleweka. Vile vile ningependa kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuwa na Vituo vingi vya *Television* na Redio mbalimbali. Imesaidia kupeleka huduma kwa kusambaza habari kwa haraka zaidi kwa wananchi maeneo ya Mijini na baadhi ya Vijiji.

Lakini ningependa kuishauri Serikali kuweka utaratibu wa kuvisaidia Vituo hivyo kwa kuvipatia nyenzo na vifaa vya kitaalam vya kisasa vya kufanyia kazi ili kuwawezesha kufanya huduma hizo ziweze kuwafikia wananchi kwa urahisi hususan Vijijini. Kwani ni sehemu nyingi ambazo bado hazijapatiwa huduma hizo. Pamoja na hayo, wafanyakazi wanaofanya kazi katika Vituo hivyo maslahi yao yaboreshwe kwani kuna maeneo mengine wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la ugonjwa sugu wa Ukimwi. Ugonjwa wa Ukimwi umekuwa ni tishio ambao mpaka sasa umesambaa kila sehemu. Napenda kuipongeza Serikali hususan Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jitihada nyingi iliyoonyesha katika kupambana na ugonjwa huo ambao kwa kweli umekuwa sugu. Lakini ningependa kuishauri Serikali kwa sababu na nchi za wenzetu zilizoendelea zimeguswa na gonjwa hili, kuna baadhi ya nchi zimeweza kutufadhili kwa kutumia *NGOs* zetu ambazo tunazo nikiwa na maana Mashirika yaisyo ya kiserikali yameweza kutusaidia kwa hali na mali. Serikali ifuatilie kwa karibu zaidi misaada hiyo kwa kufanya tathmini kwa Mashirika hayo yanayotoa misaada hiyo ili kuona kwamba zinatumika inavyotakiwa na kuhakikisha kwamba misaada hiyo inawafikia wananchi (walengwa na viongozi). Vile vile zitolewe semima mara kwa mara hasa Vijijini zinazohusu gonjwa hili la Ukimwi ili wananchi waweze kuelewa kwani mara nyingi semina na mikutano hiyo huishia Mijini ukizingatia Vijiji ugonjwa huo umekuwa ni tishio na sugu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuzungumzia suala la Makao Makuu kuhamia Dodoma, kwani kwa sasa Serikali imekuwa ikitumia gharama nyingi kwa Miji miwili nikiwa na maana Dar es Salaam na Dodoma. Serikali iwe na mikakati thabiti kufanikisha suala hilo ili kuondoa gharama zinazotumika sasa. Cha kushangaza kila wakati tunapojaribu kugusa au kuzungumzia kuhamia Dodoma, Ofisi ya Wizara Mkuu pamoja na baadhi ya Wizara husema kwamba tayari wamehamia Dodoma. Si kweli kwa sababu Wizara hizo na Watendaji wake huhamia wakati wa Vikao vya Bunge hususan Bajeti lakini mara Vikao vikiisha, Watendaji hao pamoja na Mawaziri hupanda magari na kuhamia Dar es Salaam na kusababisha kuwa na Makao Makuu mbili na kuleta gharama ambazo hazipo katika bajeti ya Serikali.

Baada ya kuzungumza hayo, naishia hapo na ninaipongeza Serikali na ninaomba izingatia yote yatakayoboresha Wizara hii na Serikali kwa ujumla.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, hivi kuna Ofisi yeyote ya Waziri Mkuu upande wa Zanzibar? Kama ipo, Je, yupo Katibu Mkuu Mkazi wa upande wa Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, Wizara inayo habari ya njaa inayotesa Mogororo Vijijini? Ilitokea Mei mwaka huu, wanafunzi wa Shule za Msingi Tarafa ya Ngerengere walishindwa hata kufika mashuleni hadi mimi kama Mbunge niliamua kutumia senti yangu ndogo kuwanunulia unga gunia 90 nikatoa kwa Shule za Msingi 30. Hali ya wananchi ni mbaya, ninaomba msaada wa chakula bila ya aibu uetwe Ngerengere kabla ya Julai mwaka huu 2003 kiwe cha kazi za barabara na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara 10 Jimboni kwangu, ndio siasa ya Jimbo. Kidunda - Ngerengere; Tununguo- Ngerengere; Mdaula - Kidugallo - Visaraka; Lubungo - Msomvizi; Madamu - Kinole - Mzambarauni; Kwaba - hadi Usungura; Mtego wa Simba - Kiwege; Kidugallo - Magera - Lubumu; Mkuyuni - Mkumbuluni - Rudewa na Mkuyuni - Gizigizi - Lung'ala. Kuweka lami eneo la mlima Ng'aro.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zinapapaswa papaswa tu. Ninaomba Waziri Mkuu atume watu waangalie barabara hizo. Mimi nitagharamia kukaa kwao huko Vijijini.

Kutokana na migogoro inayoibuka katika baadhi ya Vyama vya Siasa nchini, iletwe sheria kuwa Vyama vya Siasa viwe na siasa sio virugu. Vyama vyenye vurugu visiwe na nafasi nchini. Ziandaliwe *Form* maalum za tahadhari. *Form I* onyo la kwanza *Form II,* onyo kali, *Form III* karipio na hatua ya nne kufuta Chama.

Mheshimiwa Spika, ninashauri fedha zilizotolewa miaka ya nyuma kujengea Ofisi zetu zipelekwe moja kwa moja *Vote* ya Bunge. Tujulishwe ni kiasi gani kwa kila Mbunge muda wa miaka miwili ya nyuma. Mimi ninajenga Ofisi yangu Mikese; Je, kama Wabunge wakijenga Ofisi, mtalipa gharama? *BoT!*

Mheshimiwa Spika, hivi vazi la Taifa ni lipi nchini Tanzania? Hatujui! Ni kaunda suit, *UK Suit*, kitenge, Bahama, *Track Suit* au pajama? Kweli halijulikani vazi letu la Taifa. Tuandae na tutajiwe vazi la Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Frederick Sumaye, William Lukuvi na Muhammed Seif Khatib timu hii ni nzuri, inavutia kwa Watanzania. Ninaomba mpokee pongezi hizi kwa dhati kwa kazi nzuri sana mliyoifanya kipindi hiki kifupi. Shukrani.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze WaziriMkuu kwa hotuba yake nzuri aliyowasilisha Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara kama ilivyo Mikoa mingine ya pembezoni ya nchi kama Kigoma, Mtwara, Bukoba na mengineyo kwa sababu ya kijiografia ni miongoni mwa maeneo yenye tatizo kubwa kwa mawasiliano kama usikivu wa *RTD.* Mkoani Mara ni hafifu kiasi cha kupeleka wananchi wengi kusikiliza vipindi vya radio za

nchi jirani za Kenya, Rwanda, Burundi na Uganda ambazo redio zake zinasikika vizuri kuliko redio yetu ya Taifa *RTD.* Hali hii inapelekea kuwepo na tatizo la kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya nchi. Kwa vile njia ya redio ndio njia ya pekee nafuu kuwafikia wananchi wengi ambao hawawezi kumudu gharama za *television* na magazeti, ni vyema Serikali ikachukua hatua madhubuti kuhakikisha redio Tanzania inawafikia wananchi wengi kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, mbali na matatizo hayo, bado *RTD* ndio redio kubwa kuliko zote nchini. Ili redio hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na iweze kukabiliana na ushindani uliopo, ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Taasisi hii nyeti nchini. Maslahi yanayotolewa na Vyombo vya Habari binafsi ni makubwa ukilinganisha na maslahi ambayo Serikali inatoa kwa watumishi wa Vyombo vya Habari ikiwemo *RTD.*

Mheshimiwa Spika, ili vyombo vyetu vya habari viweze kutekeleza majukumu yake vyema, wakati umefika kwa Serikali kutoa nafasi za mafunzo kwa watumishi wa vyombo hivi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kufikisha huduma za TVT nchini kote ifikapo mwaka 2004 mwishoni. Muda huu ni mrefu sana ikilinganishwa na umuhimu wa upatikanaji wa habari kwa wananchi wetu. *Information is power.*

Mheshimiwa Spika, panapokosekana taarifa sahihi, wananchi watapotoshwa na walaghai na hatimaye Serikali inaonekana haitimizi wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tulio mipakani taarifa nyingi zinazopatikana ni za nchi jirani kama Kenya. Hali hii ni hatari kwa nchi hasa pale tunapokuwa na utamaduni au taratibu ambazo zinatofautiana kama *KBC* wanaendesha vipindi katika lugha za wenyeji kama vile Kijaluo, Kikurya, Kikikuyu na kadhalika. Kwa vile nchini kwetu wapo watu wa tabaka hizo, basi huendelea kusikiliza vipindi hivyo katika lugha nilizozitaja. Hii itatuletea matatizo ya kudhoofisha lugha yetu ya Taifa, yaani Kiswahili. Sote tunafahamu umuhimu wa lugha yetu ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuleta maani na umoja nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni suala la uwajibikaji. Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikitoa maagizo mbali kwa Watendaji mbalimbali Serikalini.

Hata hivyo nina wasiwasi mkubwa kama kuna hatua zozote ambazo zinachukuliwa kwa wale Watendajiwanaoshindwa kutekeleza maagizo hayo. Ni vyema basi maagizo ya Waziri Mkuu yaendane na ufuatiliaji na hatua za kinidhamu kwa wale wanaokiuka maagizo hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawasilisha.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ibara ya 51 ya Mheshimiwa Waziri imeeleza mafanikio ya kuongeza upatikanaji wa maji Mjini Dodoma na kukamilika kwa mradi wa maji Chalinze kufikia asilimia 80. Mji wa Ifakara Jimboni Kilombero vyanzo vyake vyote vya maji viko kwenye mazingira ya *high water table level.* Kwa hali ya tambarare ya nchi hiyo. Kwa hiyo, Ifaraka ina tatizo sugu la kipindupindu. Kwa kuwa Wilaya imeshafanya uchunguzi wa chanzo cha maji kilicho juu na salama. Je, kwa hali hii ya hatari, ni lini Serikali itaokoa maisha ya wakazi wa Ifakara?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Vijiji vya Taveta na Tanganyika Jimboni Kilombero hapa nchini ndio vinavyotoa machungwa ya hali ya juu sawa na yale ya Florida nchini Marekani, hivyo kutoa tumaini kabisa kwa hapo baadaye kuwezesha usindikaji sambamba na ibara ya 28 ya hotuba yako. Kinachohitajika ni matengenezo ya barabara kwa gharama nafuu. Tatizo ni Mto wa Ruhuji Katiyao, Taveta na Tanganyika (Masagati). Tathmini ya daraja kwa miaka ya themanini ilikaribia shilingi bilioni saba. Lakini Vijiji vya Kipulapula, Jimbo la Njombe Kaskazini na Tanganyika, Masagati la Kilombero la kwa pamoja wamejitolea kwa nguvu kazi kutengeneza barabara kati ya Vijiji vyao. Kinachohitajika ni kujenga madaraja madogo madogo au ma-*drift* kwa gharama nafuu ukilinganisha na ile ya kujenga daraja la Mto Rufiji.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu isingekuwa jambo jema kama madaraja hayo madogo madogo yengepewa kipaumbele ili kuhamasisha ujirani mwema wa Majimbo haya mawili na hapo hapo kusaidia kupunguza umasikini kwa wananchi?

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza hotuba ya Waziri Mkuu, yenye mantiki ndani yake. Pia nawapongeza Watendaji wote walio katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuzungumzia elimu. Napenda kuishukuru Serikali kwa kuzingitia elimu kuipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea kuhusu vijana wanawake. Katika elimu, Shule za Msingi mpaka Sekondari vijana wa kike wengi hushindwa kuendelea na masomo yao ingawa wamo ndani yao ambao wana uwezo mzuri na vipaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wa kike hupata mimba wakiwa bado wanaendelea na masomo na baadhi yao hupewa mimba hizo na walimu na wanafunzi hao hawaendelei tena na masomo. Huyu mwanafunzi wa kike hukosa kuendelea na masomo na matokeo yake mwalimu huhamishwa Shule. Je, Serikali haioni sasa uko umuhimu wa kuleta Muswada wa Sheria ili vijana hawa nao wawe na haki ya kuendelea na elimu?

Kwani vijana hao hukosa elimu na maisha yao kuwa ya taabu sana kwa kukosa kazi na kukosa elimu ambayo haimruhusu kijana huyu kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea ajira kwa vijana wa jinsia zote. Suala hili sitakuwa na mwisho wa kuliongelea maana hotuba ya Waziri iliyopita nililiongelea sana

na sasa ni hivyo hivyo.  Kwa sababu Waziri Mkuu amekiri katika hotuba yake ukurasa wa 29 nanukuu:  "Hata hivyo madini yanayozalishwa nchini yamekuwa yakiuzwa nchi za nje bila kusanifiwa.  Hali hiyo inaikosesha nchi mapato na nafasi za ajira kwa wananchi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hiyo tosha kudhibitisha kuwa wapo wananchi wengi ambao hawana kazi hasa vijana na ni kitu ambacho ni cha hatari sana kwa sababu vijana hawa wanahitaji kuishi kwa matumaini na mahitaji yao kama binadamu yanakamilika. Kwa maana hiyo vijana wanahitaji Serikali iwasaidie kufikiria/kuamua vijana hawa tutakaa nao bila ya ajira mpaka lini nao wanakua na ni watu wazima ambao hawana ajira. Je, Serikali inawasaidiaje vijana?

Vijana ni kundi kubwa ambalo tunashukuru kwa mgawanyiko wao wengine Askari Polisi, JKT na huko waliko ndio vyombo vya ulinzi vya nchi hii. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuandaa chombo kama hicho kwa kila Kata ambao watakuwa na mstaafu mmoja ambaye atashirikiana nao kuwa ni kiongozi wao na kujihusisha na masuala ya miradi ya kufyatua matofali na hata pia kujenga nyumba ambazo ni za bei nafuu na kuziuza kwa wananchi kutokana na msaada wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hotuba hii.

**MHE. JANET B. KAHAMA:**  Mheshimiwa Spika, nami nampongeza Waziri Mkuu pamoja na Ofisi yake katika kuandaa mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya mwaka 2003/2004.

Napenda kutoa hongezi pia kwa Wabunge wapya waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama, jitihada imefanywa kwa kiasi kikubwa lakini bado nguvu ya dola inahitajika katika kutoa nguvu zaidi katika maeneo ya mipakani ili kuzuia wimbi la ujambazi unaoingia humu nchini na hasa kusababisha maisha ya raia wetu kupotea.

Kuhusu ongezeko la madawa ya kulevya, mbinu zaidi zibuniwe za kuzuia upandaji wa bangi na pia uzuiaji wa kuingizwa kwa madawa ya kulevya toka nchi jirani na nchi za ng'ambo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, misaada mingi ya manufaa hapa nchini kwetu inaletwa toka kwa wahisani mbalimbali toka nchi za nje ili kusaidia huduma za afya na huduma mbalimbali.

Huduma hizi za vifaa mbalimbali kama vile mashine za kutumika katika *operations* mahospitalini, madawa, nguo na kadhalika.  Usafiri wa kuvileta vifaa hivyo hapa nchini toka ng'ambo unalipwa na Wahisani wenyewe ambao wamevituma vifaa hivyo.  Cha kushangaza sana, vifaa hivyo ambavyo kwetu sisi ni misaada mikubwa, tunaambiwa kuwa Wahisani hao tena wanatakiwa kulipia ushuru.

Mheshimiwa Spika, kama hivi ni kweli, basi ni bora Serikali ifikirie kurekebisha hali hii kwani tukizidi kuwakandamiza Wahisani, tutaishia kukosa kabisa misaada ya madawa, mashine za hospitali na pia katika mashirika mengine kwa vikundi maalum kama vile watoto yatima.

Mheshimiwa Spika, ni Vituo vichache sana vyenye nafasi na sehemu ya kutunzia watoto wenye mtindio wa ubongo. Madarasa ya kuwafundishia ni machache, *health centers* chini ya *welfare* ni chache. Inashangaza sana kuna baadhi ya Maafisa na viongozi wa Wizara husika zote hawafahamu kuwa kuna baadhi ya wanawake wananchi wamejitolea katika kutafuta mbinu za *fund raising* na kuweza kujenga madarasa 17 huko Dar es Salaam. Vikundi kama hivi vinatakiwa kuhamasishwa na kutambuliwa ili kuwapa motisha wa kazi.

Mheshimiwa Spika, jitihada ya Serikali kuendelea kutambua maeneo mapya ya utalii ni vyema sana. Naomba pia kwa kipindi kijacho Serikali ifikirie pia kulihusisha eneo muhimu la hifadhi ya Tawala za Kale (Machifu wa kale - Abakama), ni sehemu iliyo nzuri yenye mandhari safi ya Ziwa Bwelanyange huko Karagwe.

Eneo hili lilikuwa ndilo sehemu ya kufikia kwa kwanza kwa Wafalme wa kale walipokuwa wakiingia nchini mwetu Tanzania, toka nchi za jirani kama Uganda (Toro, Nyoro). Walifika hapo pamoja na vifaa vyao vya kiutawala vya thamani na maana. Vifaa hivi walivihifadhi hapo, mpaka hivi sasa haijulikani waliishia kupelekwa wapi! Eneo hili basi litengenezwe nyumba za kiasili zijengwe ili kuhifadhi eneo maalum ili kuvutia watalii wa ndani na nje na pia kuhifadhi hitoria yetu. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. COL. FETEH S. MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa pongezi zangu za dhati kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini kwa hotuba nzuri ambayo imepangika, imejaa hekima na mipango mizuri ya maendeleo ya nchi yetu. Naomba kwa heshima kubwa kutamka kuiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na kukubali moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imekamilika, kwa maana hiyo ningeomba kuchangia katika maendeo machache kabisa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba imeelezwa wazi kwamba hali ya mipaka yetu haijaridhisha vya kutosha na inaonekana huenda kukapatikana utulivu hapo baadaye, ninavyoamini mimi kwa vile nchi za jirani zetu zina matatizo makubwa na bado utulivu haupo nchi za jirani, basi na sisi nchini kwetu tusiamini kabisa kwamba tuko katika amani na utulivu. Ninasema maana ya kusema lazima tuchukue juhudi mara mbili zaidi ya ulinzi mkali wa mipaka yetu na ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia ninakiri kwamba kweli uchumi wetu umepanda kidogo lakini naomba kusema kwamba asilimia 6.2 ni nzuri ukilinganisha na asilimia 5.6 kwa mwaka 2001. Ninaomba tuwe wazi kwamba bado tunahitaji bidii katika kupeleka mbele

viwanda, kilimo na tuangalie sana uchumi kwa upande wa baharini na raslimali zilizomo katika maziwa yetu (majini). Uchumi wetu bado uko chini mno kwani bado tuna bajeti tegemezi yaani tukikosa misaada kutoka nchi rafiki tumeanguka vibaya kwani asilimia 45 ya kukamilisha bajeti hatunayo, hivyo ni kuvurugika kwa mipango yetu yote.

Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba Serikali imechukua juhudi kubwa katika huduma za jamii kama afya, elimu na kadhalika. Mafanikio makubwa yamepatikana lakini ninaomba tuangalie sana upande wa kukuza elimu hasa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, sote tunakubali kwamba elimu ndio msingi wa maisha kwa kila kitu ndio mwanga unaong'arisha kila kitu katika ulimwengu wetu huu. Ninaomba tubadilishe mfumo wetu tuondoke katika kuwalea watoto wetu hadi darasa la saba. Mtoto huyo anaacha Shule akiwa mdogo mno hana elimu ya kumsaidia maisha yake.

Mheshimiwa Spika, ninadhani kuna haja ya kuwalea watoto hao hadi Sekondari kwa maana ya *Form Four.* Aidha, Shule zetu ziwe na utaratibu wa kuwafunza kazi mbalimbali za amali yaani kazi za ufundi ili iwasaidie katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo ninaomba kwa mara nyingine tena kusema kwamba ninaunga mkono hotua hii mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Mkuu iko kimya kuhusu suala la kuhamia Dodoma. Tunaomba programu ya Wizara kuhamia Dodoma ichapishwe kuonyesha lengo, mwaka na ni Wizara ipi inahamia.

Mheshimiwa Spika, fungu 64 katika ukurasa wa 55 Sekta ya Habari, naipongeza Serikali kwa kuruhusu vyombo vya habari vingi nchini. Lakini hiyo sheria ya *restriction* ya matangazo kwa Mikoa fulani tu ina umuhimu gani leo 2003! Pale Kongwa kuna *local technology* mtu anaona *TV* ya Msumbij, Uganda, Cameroon na kadhalika, hivi vituo vya hapa nchini vinazuiwa kwa nini? Redio kama za Kidini, Kikristo au kiislamu nazo zinazuiwa nini kutangaza matangazo yake nchi nzima? Wakati sasa umefika kwa wananchi kuelezwa wazi kama bado sheria hiyo ina mantiki ya kubakia.

Mheshimiwa Spika, hongera kwa Serikali kuanzisha kada ya Maafisa Watendaji wa Mitaa kwa Mijini na Miji midogo. Serikali iliishaahidi kuirudisha kada ya Makatibu Tarafa kwenye Halmashauri za Wilaya. Hili halikuongelewa katika hotuba; nini msimamo wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi na kutenga fedha mwaka 2002/2003 za kujenga Mahakama ya Wilaya ya Kongwa. Hakuna kilichofanyika, tunaomba sana mwaka huu jengo hilo lijengwe na pia Hakimu wa Wilaya ahamishiwe Kongwa ili aendelee kufanya kazi katika *facility* zilizopo wakati Serikali ikijiandaa kujenga jengo la Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hongera kwa kazi nzuri sana katika eneo hili hasa MMEM. Wilayani Kongwa tumefanya kazi nzuri sana. Mwaka jana Serikali iliahidi kuwa safari hii itaanzishwa *massive program* iitwayo *Secondary Education Development Program (SEDEP)* . Hotuba ya Waziri Mkuu haikutaja chochote kuhusu ukombozi huu muhimu tuliokuwa tunausubiri kwa hamu sana hasa Wilaya zetu zilizo nyuma sana kielimu. Napendekeza mwakani tuanzie hapo.

Elimu ya Sekondari inakwamishwa sana na ada ya Sh. 40,000/= kwa Shule za Sekondari za Serikali. Hili ni tatizo kubwa sana linakua ari kwa watoto wa masikini, wajane, yatima wa kike na kadhalika. Naiomba sana Serikali kuona uwezekano wa kuondoa kero hiyo pia ili watoto wa Tanzania wasome.

Mheshimiwa Spika, upo upungufu mkubwa sana wa Waalimu wa Sekondari Wilayani Kongwa kwa Shule za Zoissa Sekondari, Kongwa Sekondari na Mlali Sekondari.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Kamati za Halmashauri za Wilaya ziangaliwe upya; kwa maana Kamati ya Mipango, Fedha na Uchumi kwa Halmashauri za Wilaya zibadilishiwe muundo na majukumu ikiwa ni pamoja na kuondolewa uwezo wa kuwa Kamati za Zabuni na pia Wenyeviti wa Halmashauri, Manispaa na Majiji wasiwe Wenyeviti wa Kamati za Zabuni.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi sana zina uhaba mkubwa wa wataalamu, Wahandisi, Madaktari, Wahasibu na kadhalika na vijana wasomi wapo mitaani. Tafadhali sana Serikali itoe nafasi za ajira kwa wataalamu hao ikiwa ni pamoja na kada ya Ukurugenzi.

Katika mpango wa kujenga jengo la Bunge jambo ambalo ni zuri, nakumbushia kuhusu umuhimu wa Wabunge kuwa na Ofisi Dodoma. Si vyema Wabunge kukaa na nyaraka muhimu majumbani, magesti na kadhalika. Suala la majengo maalum ya Ofisi za Wabunge Majimboni pia likumbukwe kwenye Bajeti ya 2004/2005. Bajeti ya huduma kwa Wabunge ikiwa ni pamoja na kuwawezesha ili wafanye kazi ipasavyo. Najua hili linashughulikiwa, tatizo ni *process* ndefu yenye kuchelewa. Nashauri jambo hili lipewe umuhimu wa kipekee.

Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Spika, nimepata faraja kubwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokiri kwamba matokeo ya uchaguzi mdogo uliofanyika Mei mwaka huu yameijengea nchi yetu heshima kubwa ndani na nje ya nchi. Lakini ni lazima tukubali kwamba matokeo hayo hayakuja tu bila sababu. Kwa mfano kule Zanzibar ambako wachunguzi wa ndani na wa nje waliusifu sana uchaguzi huo kuwa ulikuwa wa haki na huru, ni kutokana na matokeo ya utekelezaji wa muafaka uliofikiwa kati ya Vyama vya CCM na *CUF* jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, hatua kadhaa zilizochukuliwa zikiwemo:-

- Kuundwa Tume huru ya Uchaguzi iliyoshirikisha Vyama Vikuu Visiwani humo;

- Katiba ya nchi na Sheria ya Uchaguzi vimefanyiwa marekebisho kukidhi haja ya kuwepo kwa Vyama Vingi vya Siasa;

- Kuanzishwa daftari la kudumu la wapiga kura ambapo wadau wote wameshirikishwa; na

- Elimu ya uraia ilipewa umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo kwa upande wa Tanzania Bara inasikitisha kwani ni muda mrefu ilikwishakubalika kutengenezwa hilo daftari la kudumu. Lakini ndio kwanza linategemewa kuanzishwa mwaka huu.

Hali kadhalika Katiba ya nchi na Sheria ya Uchaguzi bado havifanyiwi marekebisho yanayostahili. La kuvunja moyo zaidi ni kuwa mpaka hii leo Tume ya Uchaguzi ni ya Chama kimoja (Tawala) na baya zaidi ni kuwa imewekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Elimu ya Uraia nayo ni duni, bado haijapewa umuhimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hiyo, kamwe tusitegemee kuwa na chaguzi huru na za haki kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa hiyo, kuanzishwa kwa daftari la kudumu la wapiga kura pekee bila kuzingatia hayo mengine muhimu niliyoyataja itakuwa ni kupoteza imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu aige hatua zilizochukuliwa Zanzibar, kwani kuiga mema si vibaya.

Kwanza ni lazima Tume ya Uchaguzi iundwe upya kwa kushirikishwa wadau wote vikiwemo Vyama vya Siasa. Aidha, Tume hiyo iondolewe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na badala yake ijitegemee na ipokee kasma yake kutoka Hazina moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi na Sheria ya Uchaguzi lazima vifanyiwe marekebisho viendane na hali ya Siasa ya Vyama Vingi. Elimu ya urai ipewe umuhimu wake na hatimaye daftari ya usimamizi wa Tume Huru ya Uchaguzi. Tukifanya hivyo tutaendesha chaguzi zetu katika hali ya utulivu, salama na uhuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nashindwa kuelewa kwa nini chaguzi za Vitongoji na Serikali za Mitaa zinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu hali tukijua kwamba nao ni *interested party* katika chaguzi hizo. Mwenendo huu unatia wasiwasi kwamba umeandaliwa makusudi kuwa ni mkakati wa kukisaidia Chama Tawala kushinda kirahisi chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kichekesho kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo viongozi wake wakuu pia ni viongozi wa Chama Tawala utegemee kuwe na *fair election.* Wala mimi sioni sababu kwa nini chaguzi hizi za Vitongoji na Mitaa zisiwekwe chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyo huru.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama kweli tunataka kuwa wazi na kuaminiana katika shughuli za chaguzi za Vitongoji na Mitaa, basi chaguzi hizo moja kwa moja zihame kutoka Ofisi yako na mara moja zisimamiwe na Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi ambayo itakuwa imeshirikisha wote.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha mazingira ya mashirikiano ya Serikali zetu mbili na kuondoa kero mbalimbali za Muungano.

Aidha, naipongeza hatua iliyofanikiwa ya makubalino kuhusu gawio litokanalo na faida ya Benki Kuu *(BoT)* na misaada kutoka kwa Wahisani. Hii ni pamoja na kuundwa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kumtanabahisha Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hili ni suala mbalo limekuwa linaleta manung'uniko makubwa kutoka pande zote mbili za Jamhuri. Ni vyema basi wananchi waone kuwa gawio hili halibakii kwenye makaratasi tu. Utekelezaji wake upewe umuhimu mkubwa tena katika hali ya uwazi kabisa. Tukifanya hayo, tutaweza kupunguza manung'uniko kwa kutokuaminiana na hatimaye tutaimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, mgao wa faida hiyo uzingatie asilimia ya mtaji ambao kila upande ulichangia katika kuanzisha Benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ilikumbwa na maafa mbalimbali katika mwaka 2002/2003 na inaonekana Serikali imechukua hatua kadhaa kukabiliana na maafa hayo ikiwemo kuwalipa fidia waathirika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ametaja maafa mbalimbali yaliyojitokeza na hatua zilizochuliwa. La kushangaza tu ni kwamba maafa ambayo yametajwa katia hotuba hiyo ni yale yaliyotokea Tanzania Bara tu, kana kwamba kule Tanzania Zanzibar hakutokei maafa.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba ajali kadhaa zimekuwa zikitokea Zanzibar hasa za usafiri wa baharini na maisha ya binadamu mengi hupotea. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haikuona kuwa hayo ni miongoni mwa maafa ambayo yamepoteza roho za Watanzania walio wengi? La kuhuzunisha zaidi ni hii ajali ya mashua iliyoondoka Tanga kuelekea Pemba mnamo mwezi Januari mwaka huu 2003. Mashua hii ilizama na tumeelezwa kwamba taarifa zilipelekwa kwenye Taasisi zinazohusika (forodha, Polisi na kadhalika). Aidha, wananchi baadaye nao baada ya kupata taarifa walijaribu kuomba msaada kutoka Polisi na kikosi cha KMKM pale Wete

Makao Makuu lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa visingizio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, raia hawa walikokotwa na maji kwa muda wa siku tatu na hatimaye kutokana na machofu njaa na kiu wakapoteza maisha wote, isipokuwa watu wawili ambao hatimaye walifika nchi kavu kwa uwezo wa Mungu. Inasadikiwa kuwa kaisi cha watu 30 waliopoteza maisha, ambao kama hatua za dharura zingechukuliwa wangeliweza kuokolewa.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi ni kitendo cha Serikali kushindwa hata kutoa tamko kuhusu kupotea chombo hicho na hatimaye kupoteza roho za Watanzania wenzetu. Aidha, mpaka hii leo Serikali imeshindwa hata kuwafariji sembuse kuwapa fidia wale waliopatwa na maafa hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kupitia kwako ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kuyatambua na kuyaweka katika kumbukumbu zake maafa yanayotokea Tanzania Zanzibar na hali kadhalika nao kupatiwa fidia kama wenzao wa Tanzania Bara (kwa kuanzia na maafa haya ya mashua) ili nao waone wanatendewa haki.

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninawapa pongezi Wabunge wapya wote walioapishwa katika Bunge lako Tukufu hili. Vile vile ninampongeza Waziri Mkuu pamoja na Wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri isiyo na dosari na yenye mwelekeo mzuri wa kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hotuba hii na ninaitakia kila la kheri katika kufanikisha kazi zake. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. ABDALLA KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia.

Pia sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyojumuisha mambo mbalimbali ya maendeleo katika Sekta tofauti kwa lengo la kukuza, kuendeleza, kuimarisha na kubwa zaidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 - 2005.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika upande wa ulinzi na usalama. Juu ya kuwa hali ya uchumi ina matatizo kidogo, ipo haja mambo yafuatayo yazingatiwe:-

(a) Vitendea kazi kwa walinzi hasa Polisi kama *Radio Call* na kadhalika;

(b) Kuboreshwa mishahara ya Polisi, Magereza ili angalau ifanane fanane na kazi zao nzito wanazofanya.

(c) Kuwahamasisha vijana kujifunza zaidi masuala ya Mgambo.

Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya wananchi wanaoishi Vijijini ni maskini. Ukuaji wa pato la Taifa karibu kila mwaka linaongezeka lakini mwananchi huyu wa Kijijini anaposikia kuwa pato la Taifa linaongezeka na yeye bado hali yake kubaki vile vile haelewi. Ipo haja wananchi wakaelimishwa jinsi gani ya ukuaji wa uchumi na pato la Taifa ili waelewe. Vinginevyo itawawia vigumu sana kwao kufahamu jinsi ukuaji na ushukaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye pamoja na Mawaziri wa Nchi walioko Ofisini kwake, Katibu Mkuu na Wataalamu wote kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini makubwa. Hotuba hiyo imeelezea hatua mbalimbali Serikali yetu inatarajia kuchukua huduma za jamii na kuendeleza kwa kasi kubwa zaidi na endelevu uchumi jumla na tariban sekta zote za uchumi na huduma za uchumi kwa mujibu wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, dira ya Taifa ya 2025 na mkakati wa Taifa wa kupambana na umasikini. Hakuna shaka yoyote kwamba yote yakitekelezwa ipasavyo, Tanzania itakua kiuchumi na kiustawi wa jamii kwa kasi kubwa endelevu. Kwa mwelekeo na mtamzamo huu naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ya kuridhisha kwa jumla, ningependa kuchangia kwa maeneo machache kama ifuatavyo:-

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwekea mkazo suala la uimarishaji wa ujenzi wa Ofisi ya Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo ya (mwisho mwa aya ya tisa ukurasa wa saba). Suala hili limeendelea kuwa miongoni mwa kero kuu zinazowasibu Waheshimiwa Wabunge kwa miaka mingi na kupigwa mpira kati ya Ofisi ya Ma-*RC* na Ma-*DC* hata baada ya Waziri Mkuu kuhimiza juu ya utekelezaji bora wa hili.

Mheshimiwa Spika, Jimbo ninaloliwakilisha la Mkinga limekuwa likikabiliwa na kero nyingi kwa muda mrefu bila ufumbuzi ufaao. Baadhi ya kero hizo ni ukosefu wa mawasiliano maalum yaliyopo katika Ofisi ya Uhamiaji mpakani Hororo na JKT Maramba. Jimbo la Mkinga halina mawasiliano ya simu na huduma za Posta ni kama hazipo kabisa. Pamoja na mawasiliano mengi na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na pia Taasisi zake za Posta na Simu na Kampuni binafsi husika, mafanikio hayapatikani na wananchi wanaendelea kukosa huduma hizi muhimu.

Ukosefu wa umeme kwa sehemu kubwa ya Jimbo la Mkinga, Vijiji vingi kama vile Dahuni, Gombero, Kwala, Machimboni, Mayomboni, Mkinga na Zingibari ambavyo vingeweza kuongeza uzalishaji mali na huduma nyingine kwa kutumia umeme vinakosa fursa ya kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu na kupunguza umaskini wa wananchi wake kutokana na ukosefu wa umeme. Pamoja na ahadi nyingi zilizotolewa na viongozi wa Wizara ya Madini na Nishati kutembelea Jmboni Mkinga ili kutafuta uwezekano wa kuondoa kero hii, hilo halijawezekana bado.

Madini na uwezekano wa kuwepo mafuta, zaidi ya madini ambayo tayari wachimbaji wadogo wanayafanyia kazi tayari, nimeripoti dalili za kuwepo madini mengi zaidi na pia dalili za kuwepo mafuta Jimboni Mkinga, Wizara bado haijapeleka wataalam kufuatilia masuala hayo.

Kuhusu Kero ya maji, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na wananchi, Halmashauri ya Wilaya na Wahisani mbalimbali bado ukosefu wa maji safi na salama kwa binadamu na mifugo ni mkubwa sana. Kwa kweli, ni muhimu kero ya maji ya Jimbo la Mkinga likawekwa katika mpango mkuu *(Master Plan)* wa Taifa na maji ili kuweza kupatiwa visima virefu, mabwawa na malambo kutokana na mpango mkuu wa Taifa badala ya kutegemea Halmashauri na Wahisani pekee.

Kuhusu barabara, ni jambo la faraja kubwa na kujivunia kwa jitihada kubwa iliyofanywa na Serikali Kuu, Halmashauri na Wahisani kwamba barabara nyingi zimekarabatiwa. Aidha, ninaipongeza Serikali kwa kujenga upya madaraja sita katika barabara ya Tanga - Hororo. Sasa bado madaraja mawili na kalavati moja tu. pia naipongeza Serikali kwa kuiweka barabara hii katika kipaumbele cha kwanza miongoni mwa barabara ambazo zitajengwa kwa kasi ya lami chini ya ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Barabara hii, katika hali yake ya sasa, inatia aibu sana hasa kwa watalii na wageni wengine wanaotumia barabara kuu hii kwani kwa upande wa Kenya barabara hiyo imetiwa lami hadi mpakani, lakini abiria na mizigo kama vile matunda, mboga na maziwa yanaathirika sana kwa upande wa Tanzania. Ipo haja ya kulipa jambo hili msukumo maalum ili barabara hii iwekewe lami.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkinga wamekuwa wakiomba Wilaya tokea wakati Marehemu Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine alipokuwa Waziri Mkuu. Inasemekana uamuzi wa kuifanya Mkinga iwe Wilaya ilifikiwa tokea wakati huo, lakini utekelezaji wake ulikuwa ukisubiri upatikanaji wa fedha. Hii ndio kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Mkinga. Wamekuwa wakilifuatilia sana karibu kwa kila kiongozi. Nami nimelifuatilia na TAMISEMI kwa mdomo mara nyingi na kwa maandishi tangu mwaka 2001 lakini mpaka leo sijapata jibu hata la kuunda Halmashauri ya Mkinga kama Tanga Vijiji ni kwa kuanzia lakini hakuna jibu rasmi. Wananchi wa Jimbo la Mkinga wanakerwa sana na hali hii kiasi kwamba wamekuwa wakitafuta fursa ya wao wenyewe kupeleka ujumbe kwa Mheshimiwa Rais. Kwa kuzingatia kero na gharama wanayopata kwenda na kurudi Makao Makuu ya Wilaya Muheza, nashauri ama jibu rasmi litolewe au mmoja wa viongozi wa ngazi ya juu atembelee Jimboni Mkinga kufafanua uwezekano au tatizo linalokwamisha ombi lao kukubaliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kuandaa Bajeti hii vizuri. Mimi mchango wangu, nauelekeza katika Wizara ya Kilimo na Chakula. Ili tuweze kuepukana na balaa la njaa, ni vizuri wakulima hasa wakulima wadogo wadogo wapewe utaalam wa kilimo wa kutosha. Kwa mfano, waelekezwe wakati muafaka wa kulima; wafahamishwe namna ya kutumia mbolea za samadi na mboji; Maafisa wa Kilimo wafungue mashamba madogo madogo (vitalu) ili kuonyesha mfano kuhusu faida ya kulima bila utaalam na tofauti ya kulima kwa utaalamu; na wafanyakazi wote wa Wizara wanapolima lazima walime kwa kuzingatia kanuni za kilimo. Hii itawafanya wakulima kuwa na imani kuwa bila kulima kwa kutumia utaalam mafanikio ya mavuno yanakuwa dhaifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirika, wakulima wengi wanapenda kulima kwa ushirika, lakini hawajaelekezwa faida ya ushirika. Napendekeza elimu itolewe zaidi katika vikundi hivyo. Serikali itoe upendeleo maalum kwa wakulima kuwakopesha pembejeo za kilimo pamoja na kuwepo na uhakika wa kununuliwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu asilimia mia moja.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuanza kutoa shukrani kwako mwenyewe kwa kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema moja kwa moja kuwa naunga mkono hoja mia kwa mia. Namshukuru Mheshimiwa Rais anavyojitahidi kukabiliana na kero za wananchi nchi nzima. Kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye mwenyewe na Mawaziri walio chini yake ninawashukuru kwa juhudi wanazoendelea nazo, kupambana na matatizo mengi yanayotukabili kwa ujumla katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kusema yanayohusu Jimbo langu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa jinsi ambavyo Serikali imejitahidi kusaidia au kutekeleza mengi ambayo niliyasema sana katika hotuba yangu katika kipindi cha Bajeti mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na Wizara ya Afya. Wizara hii kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi wametutatulia tatizo la upungufu wa Watumishi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na sasa tunayo *X-Ray, Ultra Sound, OCS* zinaendelea kusaidia mambo mengi ya hapo hospitalini kwetu na utendaji wa kazi umeboreka zaidi katika hospitali yetu ya Wilaya. Gari la wagonjwa, chakula cha wagonjwa, yote haya ni mafanikio ambayo yamepatikana chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nitagusia kwa ufupi sana Wizara zifuatazo:- Wizara ya Ushirika na Masoko, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Utawala Bora, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Elimu na

Utamaduni, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Wizara zote zilizopo hapo juu ukweli zimejitahidi kufikisha huduma mbalimbali katika Jimbo langu, hivyo napenda kwa ujumla wake nikufahamishe kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa nimepata ushirikiano wa karibu sana na Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilichangia kwa kuongea Bungeni, naomba kusema hayo machache yanatosha. Napenda nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu azisukume Wizara nyingine zifanye hivyo kama zilivyofanya hizo hapo juu. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na wataalam wote walioshauri Serikali na hususan Bibi Rose Rugembe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza nianze kuchangia suala la barabara. Barabara ya Tabora - Itigi- Dodoma ipitike kwa mwaka mzima kwa kuanzia na baadaye Kigoma-Tabora- Dodoma ili hali ya uchumi ipande.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji, hasara ya kuchelewa kubinafsisha Mashirika mengi hapa nchini kusababisha kutopata wateja kwa wakati muafaka na pia kutouzwa kwa bei inayolingana na thamani yenyewe.

Kwa mfano, kuchelewa kubinafsisha *Air Tanzania* dhaifu matokeo yake biashara ya usafirishaji ikachukuliwa na Makampuni mengine kwa asilimia 60. Uzuri wa biashara hii ulifanya *Kenya Airways* kununua Shirika binafsi la *Tanzania Precision Air* na kuleta ndege nzuri kubwa katika njia za biashara zilizokuwa chini ya *ATC* kwa mfano, Dar es Salaam-Mwanza-Dar es Salaam - Nairobi, Dar es Salaam - *KIA,* Dar es Salaam - Entebbe - Kigali - Bujumbura.

Hivyo ningeshauri hata Kiwanda cha Nyuzi Tabora kipewe wawekezaji hata kwa bei ya hasara ili tuweze kukinusuru angalau gharama za mitambo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu nitoe shukrani za pekee kwa Serikali kwa kujitolewa kuwasomesha bure Madaktari katika Hospitali za Bugando, *KCMC* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la UKIMWI, vita dhidi ya UKIMWI ningeshauri fedha ziendelee kupelekwa kwenye Serikali za Vijiji, Mitaa, Vitongoji kwa uhamasishaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia machache katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme kuwa naunga mkono hotuba hii ambayo imesheheni shughuli za utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka 2002/2003 na maelezo mazuri ya Bajeti ya mwaka 2003/2004. Naipongeza sana hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Ofisi yake kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu na hatimaye kuleta Bungeni hotuba ya Bajeti inayokidhi matarajio ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilipochangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nilikwisha ipongeza Serikali kwa busara na hekima kubwa ya kusikia kilio cha wananchi juu ya kufutwa kodi zenye kero, itoshe tu kusema kuwa Serikali ya CCM iendelee na juhudi zake za kukusanya mapato kutoka vyanzo vyake ili iweze kufidia pengo la kodi litakalotokana na kufutwa kwa kodi niliyobainisha.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza kwenye maeneo yafuatayo ya sekta binafsi na ubinafsishaji, sekta ya kilimo na Serikali za Mitaa.

Katika sekta binafsi ni kweli kuwa yapo mafanikio katika ubinafsishaji hasa kwamba asilimia 50.4 yamenunuliwa na Watanzania kwa asilimia 100, asilimia 43.6 ya mashirika yamebinafsishwa kwa ubia na asilimia 6.0 yamebinafsishwa kwa wawekezaji wa nje kwa asilimia 100, bado suala kubwa siyo idadi ya mashirika bali thamani ya mashirika hayo. Inawezekana kabisa idadi ya wageni ikawa ndogo, lakini thamani ikawa kubwa na wageni wakawa ndiyo wahimili wa uchumi wetu. Sambamba na thamani ya mashirika yaliyobinafsishwa kwa wageni, itakuwa jambo la busara kama Serikali itakuwa makini zaidi kudhibiti uondoshaji wa raslimali na Pato linalotokana na shughuli za kibiashara za mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni sekta ya kilimo. Ni kweli kuwa katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Serikali iliongeza Bajeti ya kilimo kwa asilimia 32 lakini ongezeko hili bado halionyeshi uwiano wa moja kwa moja na uzalishaji huko Vijijini. Mafunzo pekee hayatoshelezi kuongeza uzalishaji, bado wakulima wanahitaji fedha taslimu na zana ili kukidhi haja ya ongezeko la kazi za shambani zinazoshabihiana na ongezeko la uzalishaji. Bado asasi chache zinazotoa mikopo inayoitwa nafuu bado siyo nafuu kwa kuwa *implied* riba bado inafikia asilimia 30 - 40 kwa mwaka ukiachilia mbali uwezo mdogo wa kilimo kuzalisha ziada inayoweza kubeba riba kubwa kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni juu ya Serikali za Mitaa. Naipongeza Serikali kwa kuanzisha Cheo cha Afisa Mtendaji katika ngazi ya Mtaa, Kijiji na Kata na kuwalipa mishahara. Nilipochangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bajeti ya mwaka 2001/2002 niligusia suala hili kuwa Vijiji na Kata ndiyo chimbuko la maendeleo ya nchi kwa kuwa hili ndilo eneo la utendaji wa wananchi hivyo kuimarisha watendaji katika ngazi hizi ni suluhisho la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, juu ya jambo hili, naishauri Serikali katika mchakato wa kuimarisha utendaji Vijijini na ngazi ya Kata, watendaji wanaoajiriwa wawekewe sifa zinazostahili ili wawe wasimamizi thabiti na kuwa chachu ya maendeleo. Mfano, Mtendaji wa Kata na Kijiji anasimamia wataalam wenye sifa mpaka ngazi ya diploma, hivyo ni dhahiri kwamba kuwa na Watendaji wa sifa ya chini sana kutaleta athari.

Mheshimiwa Spika, vile vile hivi sasa Watendaji na wataalam hawana Ofisi, hivyo kuwa vigumu kuwa na mahali pa kutayarisha mambo yanayohusu utendaji. Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia Ofisi zenye hadhi Maafisa wa ngazi hii tendaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa hazina budi kutazama upya hali ya ajira katika ngazi ya Halmashauri na kuainisha sifa stahili kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara ili wawiane na mabadiliko ya sasa ambayo Serikali Kuu itapeleka fedha nyingi zinazohitaji kuwafikia wananchi kuleta maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo narudia tena kukushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuletea hotuba iliyogusa kila eneo la maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa katika nchi yetu inaendelea kuwa nzuri lakini sikubaliani na maelezo ya hotuba hii yanayosifia, Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwamba imefanya kazi nzuri wakati wa kipindi cha uchaguzi mdogo Kisiwani Pemba. Baadhi ya Watendaji wa Tume hiyo walikuwa wanawapendelea Upinzani, *CUF.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono maelezo yanayosema kuhusiana na Tume ya Uchaguzi ya Taifa kuwa imeendesha kazi nzuri kwa upande wa Ubunge yaani *NEC,* lakini kwa upande wa *ZEC* mambo yalifanyika kwa upendeleo na kupinga Sheria na hata Katiba yetu ya Tanzania kuhusiana na suala la uraia.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza kuwa wananchi mbalimbali wa CCM hawakuruhusiwa kujiandikisha wala kupiga kura eti kwa kuwa wana asilia ya Bara. Ni ushahidi kamili kuwa kulitokea tatizo la kuwatesa na kuwanyanyasa wananchi juu ya haki yao wenyewe, walinyimwa haki yao ya kupiga kura kwa kuwachagua wawakilishi wao. Je, huu ni uungwana?

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo lilipelekwa kwenye Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, lakini lilidharauliwa na kusababisha raia wengi wa Zanzibar asili ya Bara wasipige kura hata kama raia amezaliwa na kukulia Zanzibar (Pemba), lakini kama asili ya Bara hakuruhusiwa kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri daftari la kuandikisha wapiga kura lisianzie kwa mfano wa daftari hili lililopita la uchaguzi mdogo kwa sababu halitakuwa na haki kwa raia wengine. Mfano mzuri ni ule wa kukoseshwa kuandishwa na kupiga kura hasa kwa Askari wetu wenye asili ya Bara katika Majimbo tofauti ya Pemba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema *point* hiyo moja muhimu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika vifungu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5. Naipongeza Serikali kwa kufikiria kuanzisha daftari la wapiga kura kwa upande wa Tanzania Bara. Naomba Serikali iandae utaratibu mzuri kwa watu watakaotumiwa katika kutekeleza zoezi hili ili Watanzania wote watakaokuwa na sifa za kufanikisha zoezi hili washirikishwe. Ni vyema Serikali ikatoa tangazo la hawa watumishi ili kila mtu anayetaka aweze kuomba. Baadaye orodha yote ya walioomba ipachikwe ili vyama vyote vya siasa waweze kutoa maoni yao kwa hao walioomba. Baadaye wafanyiwe usajili *(interview)* na atakayebahatika bila ya kuangalia itikadi ya kisiasa aajiriwe. Usajili huu ufanywe na kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi na si mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7, tunaomba ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo yao hasa kwa upande wa Zanzibar usimamiwe na Ofisi ya Waziri Mkuu na si Ofisi ya Waziri Kiongozi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 55, afisa mtendaji wa mtaa katika Miji si suala baya ila tu ni vyema Watendaji hawa wakapatikana kwa njia ya kuchaguliwa na si kwa kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 58, ni vyema Mahakama hasa za Zanzibar zikafanyiwa marekebisho makubwa kama ilivyokubaliwa katika muafaka ili zifanane kama Mahakama za nchi nyingine za Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 64, utendaji wa vyombo vya habari bado umeelekea zaidi upande wa Chama Tawala. Ni vyema vyombo vya habari vya Serikali vikafanya kazi zao kwa usawa kwa vyama vyote vya siasa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 69, naishukuru Serikali kwa kutoa msaada kwa walioathirika kwenye ajili ya treni. Basi pia ni vyema Serikali isibague katika kutoa misaada katika mambo ya maafa. Watanzania 36 walikufa katika ajali ya boti kutoka

Tanga kwenda Pemba lakini Serikali haikufikiria kuwapa fidia watu hawa. Pia suala la walioathirika katika maandamano ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001 bado ni kitendawili. Nilimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, suala hili lakini nasikitika alilikwepa na hakunijibu inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu twende Pemba akajionee mwenyewe hali ya yatima, vilema na vizuka naamini atawahurumia tu.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri ya mapitio ya kazi za Serikali yetu. Nampongeza pia kwa juhudi zake zote anazoweka akiwa Waziri Mkuu, kwa usimamizi mzuri wa kazi za Serikali. Pamoja na pongezi hizi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atupie macho maeneo yafuatayo ili kuboresha zaidi mafanikio yaliyopatikana sasa.

Kwanza, utangazaji kwa *Television.* Halmashauri nyingi hazijafaulu kuwa na *station* za *Operator* wa *Television.* Iwapo tatizo ni uwezo wa Halmashauri hizo, nashauri sekta binafsi iruhusiwe ikiwa ni pamoja na kurekebisha Sheria ili ilegeze yale masharti ya sekta binafsi au asasi zisizo za Serikali. Hii itawawezesha wananchi kupata habari kwa njia ya *Television* nchi nzima.

Pili, kilimo cha maeneo kame. Serikali na Watendaji wake wasiishie kuhimiza kilimo hiki katika majukwaa na kutunga Sheria za kuwabana wakulima kwa kuwawekea masharti ya kilimo hiki. Nashauri Serikali itumie uzoefu na Tafiti za Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)* ambao wamefanya tafiti za kilimo cha kuvuna maji ya mvua katika maeneo kame ya Wilaya ya Same na Mwanga. Naamini kwa kutumia matokeo ya wataalam hao wa Kilimo wa *SUA,* kilimo kitafanikiwa katika maeneo hayo kame. Nashauri pia Serikali ivune maji kwa kutumia *wind-power mills* katika maeneo ya Same ambapo upo upepo mwingi sana.

Tatu, kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Serikali itumie wataalam wake au wale wa *SUA* kufanya tafiti za kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya mito na vijito,chemchem katika Kanda za milimani. Kule katika Wilaya ya Same lipo bonde la umwagiliaji la Mto Nakombo, Pangani, Hingilili, Nyongoma na Sasini. Pia zipo ndiva nyingi za kilimo cha umwagiliaji katika milima ya Same. Serikali itumie uzoefu na matokeo ya tafiti za asasi zisizo za Serikali za *SAIPRO* na *TIP* kule Same. Wilaya hii inakumbwa na baa la njaa na kuhesabika ni Wilaya kame kwa sababu raslimali hizi za kilimo cha umwagiliaji zimepuuzwa. Naiomba Serikali sasa ilifanyie kazi eneo hili la kilimo na kutoa majibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama wa raia, naipongeza Serikali kwa hatua inayochukua kuhusu ujambazi nchini. Juhudi hizi hazijaridhisha kutokana na ongezeko la Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2002/2003 na mwaka 2003/2004. Jeshi hili linatakiwa nidhamu ya askari na viongozi wake kuangaliwa. Naamini kikwazo kikubwa cha Jeshi hili ni nidhamu. Ili nidhamu iwepo lazima viongozi wake wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya. Tume hii nayo inahitaji pongezi katika kudhibiti ulimaji wa bangi nchini. Kinachohitajika sasa ni kuwatangaza kwa uwazi wahalifu na idadi ya watu waliovunja sheria ikiwa ni pamoja na adhabu zao. Zipo dawa nyingine za kulevya za Kihindi kama *Kuber* ambazo inaelekea Serikali imeziachia ziingizwe nchini. Hizi ni dawa za kulevya, nazo zidhibitiwe kama mirungi ilivyodhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maafa iwe na uwiano na vigezo vilivyo wazi vya kutoa misaada kwa waathirika wa maafa. Kule katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Same yalitokea mafuriko ya mvua katika Kata ya Gonja na upepo ulioezua nyumba Kata ya Saweni. Taarifa zilipelekwa kwa viongozi wa Wilaya, Mkoa na Wizara husika chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini wananchi hao hawakupata msaada wowote mpaka leo. Matukio yote yalitokea mwanzoni mwa mwaka huu kati ya mwezi Januari na Mei. Naomba Serikali sasa iangalie uwezekano wa kuwafariji wananchi hao. Kwa kufanya hivi wananchi wetu watajenga imani kubwa na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja na kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweke ushauri wangu katika kumbukumbu zake za kufanyia kazi.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kuelekeza mchango wangu kwenye janga la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, Ukimwi limekuwa ni tatizo kubwa la kutuachia wajane na yatima wengi. Wajane hawa huwa tayari wameshaambukizwa Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, wajane hawa hupata taabu sana wanapodai urithi unaotokana na waume zao. Wanapofika Mahakamani hupandishwa kizimbani kama mhalifu, hivi Serikali haioni kuwa inawazalilisha wajane?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge Fungu la fedha la makusudi ili kuwapatia mikopo yenye riba nafuu wanawake hao kwani wanapofariki waume zao huchanganyikiwa. Huwa hawana miradi yoyote ya kuwaendeshea maisha yao na watoto wao ndiyo hapo anapoamua kuhama Mkoa huu na kwenda Mkoa mwingine au Wilaya nyingine na akipata mume au mwanaume anaishi naye na anaanza kueneza Ukimwi kwani anakuwa bado ni mzuri na wala watu hawamjui anakotoka kwani watu hawachunguzi mtu anakotoka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majambazi wengi wanaokamatwa nchini mwetu ni wa kutoka nchi za jirani, kwa hiyo, Serikali ni lazima ijitahidi kuwaangalia askari wetu ipasavyo. Ni kweli askari hasa wa Jeshi la Polisi wanapambana na mambo mazito sana na majambazi sugu kutoka nchi jirani, askari wanaowekwa mipakani wawe ni wazalendo hasa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, askari wetu tuwaangalie tena kwa upande wa mshahara kwani wana kazi nyingi za usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ilione hili suala la Muungano kwani ni jambo kubwa na ni zuri. Ninasema hivyo kwa sababu kuna viwanja ambavyo vimetolewa au viko tayari kujengwa Ofisi za Muungano lakini mpaka sasa hivi hakuna kiwanja hata kimoja ambacho kinategemea kujengwa angalau kukawa na jina la Ofisi ya Muungano. Naiomba Serikali ianze kujenga majengo hayo mwaka 2003 ili wananchi walio wengi waweze kufurahia suala hili la kuwa kuna Ofisi za Muungano, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akipata nafasi aje kututembelea Mkoani kwetu, wananchi wanamwomba aje ili aweze kuonana nao.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Watendaji, kwa kuandaa hotuba yenye mtazamo makini. Hongera sana.

Aidha, pamoja na pongezi hizi, napenda tu kuchangia katika baadhi ya mambo ambayo yanahitaji tafakari kubwa sana ya Serikali ili yale yaliyokuwa yanasemwa na Serikali yatekelezeke badala ya kuendelea kuwa maneno matamu yasiyotimilika.

Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la kuhamia Dodoma ni muhimu sana Serikali ikaweka jitihada za kuhakikisha kuwa maamuzi kama haya na mazito kwa Serikali yanatekelezeka badala ya kugeuzwa kama hadithi za mara kwa mara. Ni vema basi wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anahitimisha hotuba yake, akalizingatia kwa karibu suala hili kwa kuonyesha ni kwa namna gani Serikali kweli inadhamira ya dhati ya kuhamia hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pili, majukumu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa huyu ni Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali bado kuna haja ya kumshauri Mheshimiwa Rais, ili aweze kumpatia fursa sahihi ya kutekeleza vema majukumu yake. Serikali ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iweje sasa kauli nyingi za Mheshimiwa Waziri Mkuu zisituelekeze na badala yake yanabaki maagizo tu yasiyokuwa na meno?

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa kuwa *Television* ya Taifa imekuwa ni hadithi na hasa kwa kuendelea kuonekana katika Mikoa michache sana na hasa Dar es Salaam na Pwani tofauti na matarajio ya Watanzania wengi, inakuwaje sasa vyombo vya watu binafsi kama *ITV, STAR TV* na *Channel Ten* zinao uwezo mkubwa wa kuonyesha matangazo wakati *Television* ya Taifa haina uwezo huo? Hivi ni nani mwenye uwezo mkubwa kati ya Serikali na watu binafsi? Ni vema Serikali ikatekeleza jukumu lake la kuharakisha kuwa *TVT* ionekane nchi nzima na kwa ufanisi sana.

Mheshimiwa Spika, ni vema Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anahitimisha hotuba yake, aweke bayana ni kwa namna gani na lini *TVT* sasa itaonekana nchi nzima ikiwa ni pamoja na kuboresha vipindi vyake kwa manufaa ya Watanzania wote.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, katika mojawapo ya miradi itakayotekelezwa mwaka huu wa fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu ni kuendeleza Programu ya Masoko ya Kilimo *(Project 4456),* shilingi bilioni 2.048. Mradi huu uliandaliwa na Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, je, Ofisi ya Waziri Mkuu ina nyenzo, taaluma na uwezo wa kutekeleza mradi huu?

Je, ni Wilaya zipi zitafaidika na mradi huu na kila Wilaya husika itatengewa shilingi ngapi mwaka huu?

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyogusa karibu maeneo yote muhimu. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu apokee salaam za pekee toka kwa wananchi wa Wilaya ya Ulanga kwa ziara yake aliyoifanya hivi karibuni. Wananchi wamepata nguvu mpya kwa hotuba zake za kusisimua alizozitoa katika ziara hiyo, hasa kitendo cha kuulizana maswali hadharani na kumkabidhi Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira, kushughulikia baadhi ya matatizo ya wananchi. Nakuthibitishia nimeyashughulikia yote kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya chakula, katika ukurasa wa 63, ni kweli kabisa kwamba mwaka 2003 kutakuwa na upungufu mkubwa wa chakula. Ni vyema yawepo maandalizi makubwa ya Serikali hasa kwa kununua chakula cha akiba kwa wingi. Pili, kwa ukubwa wa nchi yetu nashauri chakula cha akiba kisogezwe kwenye Mikoa na kuhifadhiwa kwenye maghala ya Makao ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri ya kilimo lakini katika Taifa letu tuna tatizo la usimamiaji, tunapanga vizuri, maneno mazuri lakini hakuna utendaji hasa ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kaya kwa Kaya, kuna mambo mengi lakini yanaishia Wizarani, mbolea itapelekwa wakati sio wake na pesa zitakwenda wakati sio muafaka kwa kilimo na utendaji wetu sio mzuri. Mfano mzuri ni pesa za kujenga madarasa zilizotoka Wizarani zikapelekwa Wilayani moja kwa moja, madarasa yamejengwa vizuri nchi nzima na kwa wakati mmoja. Huo ndio utendaji mzuri wa kimaendeleo, leo tunazungumzia mafanikio ya madarasa hayo nchi nzima kwa ufanisi wa kazi nzuri iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja iliyoko mbele yetu mimi nitajielekeza katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Ni dhahiri kuwa tokeo awali Serikali haikuwa na dhamira ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu. Ninasema hivyo kwa sababu tokea awali jambo hili limekuwa likitamkwa na kukaririwa tu lakini hatujawahi kuona maandalizi ya maana ya kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli maneno ya kuifanya Dodoma Makao Makuu ni ya kisiasa labda ya kuwafurahisha wananchi wa Dodoma waone kuwa Serikali inayoongozwa na CCM inawajali sana kwa kuupa Mkoa wao na Mji wao hadhi ya kuwa Makao Makuu ya Serikali na kumbe inabaki kuwa ni danganya toto.

Mheshimiwa Spika, siku zote huku iking'ang'ania kuwa na azma ya kuustawisha Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu, hapaonekani hatua ya kuthibitisha azma yao hiyo. Kinachojitokeza kwa kweli ni Serikali kujikita na kujichimbia zaidi na zaidi katika Jiji la Dar es Salaam. Mfano mzuri ni azma ya Serikali ya kujenga uwanja wa kisasa na mkubwa wa ghali sana wa michezo huko Dar es Salaam, ukarabati wenye kuendelea wa Ikulu ya Dar es Salaam, nyumba ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi nyingine muhimu sana kama vile Mabenki, Ofisi za Kibalozi, hospitali kubwa na ujenzi na utanuzi wa Mji, yote hayo hayaonekani kufanyika katika Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, jambo pekee lililofanyika ni kulihamisha Bunge kutoka Dar es Salaam hadi hapa kwa nia ya kulificha ili likose kutoa msisimko wa hali ya juu kwa wananchi wa Jiji la Dar sa Salaam wenye mwamko mkubwa wa kisiasa na shauku kubwa ya kutaka kujua jinsi Bunge lao linavyosimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kujitetea kwake kuhusu kusua sua kukubwa kwa Serikali katika kukamilisha azma yake ya kuhamia Dodoma, suala la ufinyu wa Bajeti limekuwa ndio kisingizio kikubwa. Lakini tatizo sio hilo bali kukosekana kwa nia ya kweli, Waswahili wanasema, "Penye nia pana njia." Mbona shilingi bilioni tano za kujenga ukumbi mpya wa Bunge zimepatikana mara moja baada ya Serikali kuamua kwa dhati kufanya hivyo. Tusijidanganye wenyewe, bado hatuna nia ya kuhamia Dodoma kama Makao ya Serikali na hatutafanya hivyo. Ni vyema tukalifanya jambo hilo kama ndoto za alinacha.

Mheshimiwa Spika, pili, utekelezaji wa muafaka kati ya CCM na *CUF*. Muafaka ulifikiwa kwa msingi wa kuondosha uhasama uliojikita katika vyama na miongoni mwa wananchi kwani yaliyotokea yaliathiri maslahi ya vyama hivyo lakini pia tena vibaya sana yaliathiri maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ahadi kubwa zilizotolewa na viongozi wakuu wa nchi yetu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kutekeleza muafaka huo, bado hadi sasa mambo kadhaa na muhimu hayajatekelezwa. Kwa mfano hadi leo Mheshimiwa Rais wa Zanzibar bado hajawateua

Wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi kutoka Chama cha *CUF.* Na kwa kweli suala hili ni kielelezo kikubwa kinachoonyesha kuwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume, hana nia njema na muafaka wetu na kama alivyofanya mwenzake Dr. Salmin Amour Juma na yeye haitazamiwi tena kuwa atamaliza kipindi chake bila ya kuwateua Wajumbe hao.

Mheshimiwa Spika, ikiwa wenzetu wa Burundi wamekubali kutekeleza mambo makubwa na mazito ya kukabidhiana madaraka ambapo Mheshimiwa Rais Pierre Buyoya, amemkabidhi madaraka yule aliyekuwa Makamu wake ambaye ni wa chama tofauti na chake, lakini sisi tunashindwa hata kuteua wawakilishi wawili ambao sio wa chama chake. Inatia aibu kubwa kwa Tanzania ambayo ina mchango mkubwa katika kupatikana kwa amani ya Burundi.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kuunda Tume mbalimbali za kuchunguza yale maeneo yaliyowaathiri wananchi moja kwa moja. Tume hizo ziliundwa, zikafanya uchunguzi na hatimaye kutoa ripoti lakini kazi za Tume hizo zimeishia hapo. Hakuna Tume hata moja iliyozaa matunda ya manufaa kwa wananchi ambao ndio walengwa pale Tume hizo zilipoundwa na kwamba yale madhumuni ya kuponya makovu na kusahau yaliyofutwa hadi leo hayakufikiwa na hivyo kuibakisha jamii ikifukuta chuki na malalamiko yale yale.

Mheshimiwa Spika, muafaka ulitiwa saini kwa lengo la kuhifadhi umoja, udugu, upendo na mshikamano wa nchi yetu na watu wake, kwa kifupi kwa maslahi ya Taifa. Sasa wale wanaoubeza wasitekeleze yale wanayopaswa kuyatekeleza wanafanya hivyo kwa maslahi ya nani?

Mheshimiwa Spika, mimi ninashauri sote tuwe waungwana maana waswahili wanasema: "Ada ya mja kunena uungwana ni vitendo." Kiongozi wa juu kabisa akikosa kuwa mkweli na muungwana akatekeleza aliyokubaliana na wenzake sio tu kuwa ni aibu kwake bali hata kwa Taifa hususan katika uso wa ulimwengu. Kwa hiyo, yote tunayoyahofu ili yasitokee kila mmoja anapaswa kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waheshimiwa Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Uwakilishi huu una matatizo yafuatayo:-

(i) Uteuzi wao hauzingatii uwakilishi wa vyama vilivyomo katika Baraza. Ninapendekeza uzingatie jambo hili kuanzia mwaka 2005.

(ii) Imegunduliwa kuwa Waheshimiwa Wabunge hao hawawajibiki hata sehemu ya 1/4 katika majukumu yao, muda mrefu sana huwa hawaonekani Bungeni kwani Bunge na Baraza la Wawakilishi hufanya vikao vyao kwa wakati mmoja kama tunavyoona hivi sasa na zaidi ya hayo inakuwaje mtu anakuwa Waziri au Naibu Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakati huo huo anakuwa Mbunge, mtu huyo anajigawa vipi katika kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna maneno yanayozagaa kuwa Waheshimiwa Wabunge hao wanafaidi tu mishahara miwili, viinua mgongo viwili lakini kazi wanafanya upande mmoja peke yake. Kuna wanaodai kuwa Waheshimiwa Wabunge hawa huonekana hapa Bungeni kwa kutia saini fomu ya posho tu na wakishapokea posho hizo hupanda magari wakarudi Zanzibar. Hii ni aibu kwetu sote kama viongozi.

Nashauri suala hili lichunguzwe kwa busara na kupatiwa ufumbuzi wa maana. Itafutwe njia nyingine ya kuwapata Waheshimiwa Wabunge hao watano.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda sikuweza kufikia kilio kikubwa cha Mikoa ipewayo fedha kidogo ambayo ni Rukwa, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Singida.

Kama nilivyodokeza jana, kasoro hii nimeibaini kwa miaka mingi sana na majibu makuu uliyonipa kama vile Mikoa mingine kuwa na wafadhili, wakazi wa Mikoa mingine kama Arusha wako nyuma (Wasonyo walitajwa) na mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amesema atateua Tume ya wataalam wa fedha ili kutafiti chanzo cha kasoro hii.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kuwa majibu yote niliyopewa hayaniridhishi kamwe kwa sababu, kwanza, Mikoa isiyopata ufadhili wa nje ingefadhiliwa kwa fedha za ndani.

Pili, kutoendelea kwa kabila au makabila kadhaa kutokana na mila na utamaduni wao siyo sababu halali ya Mkoa waishio kupewa fedha lukuki zaidi ya Mikoa niliyoitaja. Tatu, kuteua Tume ya wataalam ni matumizi mabaya tu ya fedha za Serikali kwa kuwa Hazina ndiyo hutupa *ceiling* mwaka hadi mwaka kwa mtindo mbaya sana wa *rolling planning* ambao huongeza asilimia fulani kila mwaka kwa kila Mkoa kitu ambacho huendana na sera ya Biblia ya kumpa zaidi aliyenacho na kuzidi kumpunja aliye na kidogo na hivyo kuliongeza pengo lilipo kati ya Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anipe maelezo sahihi vigezo vilivyotumika mwaka 1998/99 kwa Mkoa wa Tabora pamoja na ukubwa wake kutengewa shilingi 106,000,000/= tu ambayo ni asilimia 1.7 tu ya zilizotengwa kwa Mkoa wa Kagera, Kigoma ilitengewa shilingi 76,000,000/= tu sawa na asilimia 1.2 tu ya Kagera, Rukwa ilitengewa shilingi 241,000,000/= sawa na asilimia 3.9 tu. Mtiririko huu unaendelea mpaka mwaka 2002/2003. Rukwa imepata asilimia 5, Tabora asilimia 6.8 na Kigoma asilimia 6.5. Hii ndiyo *Western Province* za zamani, je, Mikoa hii itakwenda?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie jedwali nililofungasha ili kuona ukweli unaotupa uchungu mkubwa na utupatie majibu ya kuridhisha ili tusiendelee kunyong'onyea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba nami niungane na wenzangu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri. Pia napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili walioko katika Ofisi yake yaani Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuondoa kodi ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi na hasa wanawake na vijana. Pia, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutoa ruzuku kwenye mbolea na pembejeo za kilimo kwa Mikoa ya upande wa Nyanda za juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu kuhusu maafa. Naipongeza Serikali kwa kushughulikia matatizo ya maafa yanapotokea, lakini napenda kuishauri Serikali hasa kwa kuangalia upya vigezo au aina za maafa badala ya kuangalia njaa, mafuriko na matetemeko. Sasa tuangalie pia milipuko ya magonjwa, tuangalie Wilaya zilizoathirika na hasa na ugonjwa wa Ukimwi kwa mfano Wilaya ya Makete ambayo hata Umoja wa Mataifa umetangaza kwamba ni Wilaya ya maafa ambapo watoto hawana chakula cha kutosha na hali ya hewa ni baridi sana, lakini hawana mablanketi na shuka za kujifunika. Je, Serikali haioni sasa kwamba Idara ya Maafa inahitaji kuwasaidia watoto hawa na kuwanusuru na lishe duni na magonjwa yatokanayo na mfumo wa hewa?

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kuendesha vizuri zoezi la sensa ya watu na makazi ambayo imetuelezea hali halisi na idadi ya watu nchini. Hii itasaidia katika kupanga mipango ya maendeleo. Napenda kuishauri Serikali kuangalia kwa undani Wilaya ambazo idadi ya watu imepungua ili kupata taarifa sahihi za kupungua kwa watu au kama ni uhamiaji au ni vifo ili mikakati maalum iweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba mikakati mizuri iwekwe ili kuhakikisha pembejeo za kilimo ziweze kuwafikia wanawake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri sana na kamilifu. Ni hotuba iliyojaa ukweli na ukiisoma hukosi kuona dhamira nzuri ya Serikali ya kuleta maendeleo kwa Watanzania wote katika nyanja zote hasa katika maeneo ya uchumi, elimu, kilimo, mawasiliano na ustawi wa jamii kwa jumla

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyobaki sasa ni sisi sote kwa pamoja kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wetu ili waelewe ukweli kwamba maendeleo yao kimsingi yataletwa na wao wenyewe na kazi kubwa ya Serikali ni kuhakikisha kuwa nchi ina amani na utulivu kwa mujibu wa Sheria za nchi. Tufike mahali tuwe wakweli kwa wananchi na kuwaambia kwamba uvivu ni adui mkubwa. Jamii ambazo sehemu kubwa ya maisha yao ni kucheza bao au kucheza ngoma haziwezi kuendelea bila kubadilisha tabia na kufanya kazi kwa bidii. Mila potofu ambazo zimetapakaa katika jamii mbalimbali nchini kote lazima zipigwe marufuku ili kufungua milango ya maendeleo kwa mujibu wa matakwa ya sayansi na teknolojia ya ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, elimu ndiyo njia pekee ya kuleta maendeleo yanayoendana na ulimwengu wa leo. Juhudi za Serikali katika eneo hili zinaonekana, lakini bado tuko nyuma sana kama Taifa. Ni lazima tuendelee kuboresha elimu katika ngazi zote yaani Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu. Ni lazima tuhakikishe kwamba Elimu ya Sekondari inatolewa kwa watoto wote bure na pia Elimu ya Juu ipanuliwe na itolewe kwa watoto wote wenye uwezo. Hakuna njia ya mkato.

Mheshimiwa Spika, suala la umaskini ni suala nyeti. Suala hili tulitazame katika ngazi *(levels)* mbili yaani Ngazi ya Kitaifa na Ngazi ya Kijamii. Juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukuza Pato la Taifa na kujenga utulivu katika uchumi wa nchi hatimaye zitasaidia kupunguza umaskini kwa wote kwani huduma za jamii zitaboreka na umaskini utapungua.

Katika ngazi ya jamii, umaskini utatoweka tu kama sambamba na juhudi za Serikali za kukuza Pato la Taifa, jamii husika itafanya kazi kwa bidii na maarifa. Mila potofu zipigwe vita, uchawi utokomezwe na Serikali iwe tayari kusaidia kuondoa matatizo ya kimazingira ya kila jamii ambayo yanadhihirika kuwa kizingiti katika maendeleo ya jamii hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kyela, kizingiti kikubwa katika maendeleo ya jamii ni umbile la Jimbo. Jimbo zima ni tambalake, lina mito minne mikubwa katika eneo la kilometa za mraba 1,350. Mafuriko ni tatizo la kila mwaka kwa sababu hiyo, barabara za Wilaya huharibika sana wakati wa mvua za masika na kusababisha hasara kubwa, juhudi za wananchi kujenga nyumba bora na za kisasa zinaathirika na mawasiliano ndani ya Jimbo ni magumu kutokana na sababu za mafuriko.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, barabara za Mkoa hivi sasa ziko katika hali mbaya sana, tunaomba Serikali izikarabati. Hasa barabara ya kutoka Kikusya hadi Matema kupitia Ipinda, hii ni barabara muhimu sana kwa maendeleo ya Kyela na Serikali ichunguze uwezo wa kudhibiti Mito ya Mbaka na Lufilyo ili kupunguza athari za mafuriko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wenzangu katika kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo itakuwa dira ya maendeleo katika mipango ya maendeleo kwa Serikali kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nawapa pongezi Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa William Lukuvi, pamoja na Makatibu Wakuu na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza kuchangia hotuba hii, kutokana na kitendo cha utekekezaji wa ahadi za Serikali Bungeni wa mwaka 2002/2003 ambayo Serikali iliahidi kutoa kwa Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano huu wa 2003/2004 juu ya ujenzi wa ukumbi mpya wa kisasa kwa ajili ya Mikutano ya Bunge hapa Mjini Dodoma na ujenzi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar utaanza. Kitendo cha ujenzi wa Ofisi hizi kutaharakisha shughuli za Bunge kwa sababu majengo hayo yatakuwa ni ya kisasa na yatakayokuwa yanakwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, ingawa suala la *TRA* linazungumzwa mara nyingi katika Bunge lako Tukufu, suala hili litaendelea kuzungumzwa kutokana na matatizo wanayoyapata wafanyabiashara ndogo ndogo kutoka Zanzibar wakati wanapoleta bidhaa Dar es Salaam. Wafanyabiashara hao wakifika Dar es Salaam hutozwa ushuru kwa bidhaa hizo ambazo tayari zimekwishalipiwa wakati zikiingizwa nchini. Kitendo hicho cha kufanya bidhaa kutozwa ushuru mara mbili kinawafanya wananchi watupigie kelele sisi Wabunge wao na ndiyo maana Wabunge kutoka Zanzibar wanakipigia kelele kitendo hiki. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, akitupie macho kitendo hiki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na chimbuko la wimbi la ujambazi, ninaipongeza hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikisha Jeshi la Mgambo kwa vile wanamgambo wapo kila sehemu katika nchi yetu, sera hiyo itasaidia kuongeza nguvu za ulinzi na kuweka sawa usimamizi wa mgambo kiutawala wakati wa amani na usio wa amani.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi na hasa Wilaya ya Mjini inamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aitembelee Wilaya hiyo. Tunaomba aje kutembelea Majimboni kwetu maana wapiga kura wetu wanahamu ya kumwona.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo langu la Mwembe-Makumbi wametuma salaam za pongezi kupitia kwangu, Mbunge wao, wanasema kuwa wanazipongeza hotuba zote kuanzia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyobeba maeneo ya vipengele vyote ili kukidhi haja ya kupambana na umaskini na kuendeleza demokrasia nchini. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ninaanzia moja kwa moja kwenye mada ya hali ya siasa katika kitabu cha hotuba kwenye ukurasa wa nne, mistari ya minne ya mwisho na mistari minne ya mwanzo kwenye ukurasa wa 5 nanukuu: "Kazi kubwa tuliyonayo hivi sasa sisi

viongozi wa kisiasa ni kuendelea kuwaelimisha wananchi watambue umuhimu wa uchaguzi kama nguzo ya demokrasia na wawe tayari kushiriki kikamilifu katika kuwachagua viongozi wanaowataka kwa hiari yao wenyewe.”

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuliona hili katika kukidhi haja ya demokrasia ya mfumo wa vyama vingi kwani utekelezaji wa hili unahitaji mpango madhubuti na mkakati wa aina yake ya Serikali ya kutaka kufanya mageuzi ya kweli ya kuendeleza demokrasia itakayowashirikisha viongozi wa ngazi mbalimbali wa vyama vyote, hivyo ninaomba Serikali kutoa taaluma kwa walengwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile semina, warsha, kongamano na kadhalika ili walengwa kupata elimu ya kutosha ili chaguzi zetu ziwe za amani, utulivu na mshikamano wa kweli katika demokrasia.

Mheshimiwa Spika, pia kutengwa kwa fedha kwa ajili ya kuanzisha daftari la wapiga kura ni jambo zuri la kupitolewa mfano kuelekea kwenye uchaguzi wa kweli, huru na wa haki. Lakini hata hivyo suala la maandalizi ni lazima hao wadau waliotajwa wajumuishwe kikamilifu katika hatua zote za uanzishwaji wa daftari hili, ikiwashirikisha viongozi wa vyama vyote, Taasisi mbalimbali na *NGO's* mbalimbali kwani Tume imeridhika kufuata mfumo wa demokrasia ya vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, daftari la wapiga kura kuanzishwa kwake ni mwanzo mzuri hata hivyo suala la msingi zaidi sambamba na daftari ni kuundwa kwa Tume Huru ya Taifa ya uchaguzi angalau yenye sura kama ile ya Zanzibar *(ZEC)* ili angalau kukidhi haja ya chaguzi za kweli haki na huru katika kuwapata viongozi wanaotakiwa na wananchi wenyewe bila mizengwe, nguvu au udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, bado Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliopo hivi sasa haikidhi haja ya mfumo wa vyama vingi. Ni Tume ya Serikali na Chama Tawala hivyo ni vyema suala la Tume Huru likatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie vita dhidi ya Ukimwi ambapo imezinduliwa Tume ya Kudhibiti Ukimwi tarehe 10 Mei, 2003. Kwa kweli ni jambo la faraja katika kupambana na janga hili kubwa na la hatari ambapo linapoteza maisha ya nguvu kazi zetu. Pia ni faraja ya aina yake Tume hii kuzijengea mamlaka na Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia na kudhibiti kuenea kwa Ukimwi katika maeneo yao.

Maambukizo ya Ukimwi yaangaliwe kwa namna ya pekee hivi sasa kwani semina, warsha na makongomano mbalimbali yamefanyika na fedha nyingi zimetumika lakini bado maambukizo ya virusi vya Ukimwi yanaongezeka kwa kasi kubwa na waathirika wanaongezeka pia. Sasa ni vyema tukapime na kutathmini juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, inaonekana elimu ya Ukimwi Vijijini imefika kama vile Mijini lakini tahadhari kwa jamii ni ndogo na bado jamii haijataka kubadilisha tabia. Hii inatokana na kwamba Serikali bado haijadhamiria kikamilifu kupambana na janga hili kwani vyanzo vya maambukizo bado Serikali inavifumbia macho, kama vile nyumba maalum za ngono, kuachiwa uhuru mkubwa zaidi vilabu vya pombe, pia Serikali bado

inafumbia macho baadhi ya mila na tamaduni za makabila yanayochangia maambukizo ya virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwasaidia waathirika wa Ukimwi lipewe umuhimu mkubwa na ionekane kwamba lishe bora na madawa yawafikie walengwa hao zaidi kuliko fedha nyingi kuzipoteza kwenye semina, kongamano au warsha.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, fedha zitumike kwa kuwasaidia watoto wa marehemu na watoto wa waathirika kwa kupata huduma bora, kama vile kupatiwa elimu kuanzia ya msingi hadi sekondari na kuchunguzwa afya zao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kwamba Tume hiyo iliyozinduliwa ikaongezewe meno ya kuwapima kwa hiari yao Watanzania wote sambamba na kufanyika kwa sensa hii itapelekea kujua takwimu halisi ya waathirika na hatimaye kupata njia muafaka wa kudhibiti janga hili.

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu ni kwamba ushauri wangu utachambuliwa kwa kina na hatimaye Serikali kutekeleza ikiwezekana.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ndefu na iliyoandaliwa kwa umakini sana. Mimi napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, hali ya uchumi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamekuwa na majigambo mengi yanayoelezea ukuaji wa uchumi katika nchi yetu lakini mbona hatuoni maendeleo ambayo yanaenda sambamba na ukuaji huo wa uchumi?

Hali ya umaskini wa wananchi bado iko pale pale, vijana ambao hawana kazi idadi yao inaongezeka kila leo, kinachoendelea ni uchumi au ni umaskini? Maana dalili ya ukuaji wa uchumi ni kuondokana na hali duni ya maisha ya wananchi na kuona kwamba katika nchi hapana matatizo ya uajiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pili, Tume Huru ya Uchaguzi. Nchi yetu tayari imeingia katika mfumo wa vyama vingi karibu mwaka wa kumi na moja sasa, lakini bahati mbaya mpaka sasa hivi bado Tume haijawa huru. Kwa hiyo basi, Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa ni vyema hufanywe mpango wa kuifanya Tume ya Uchaguzi ya Taifa kuwa huru angalau kama vile Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nakusudia kwamba Tume iundwe kwa kujumuisha katika Wajumbe wale wa vyama vyote ambavyo vimepata usajili wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, tatu, daftari la wapiga kura. Muungwana ni yule ambaye anafuata mipango yake mwenyewe aliyojipangia. Katiba katika kifungu cha 5(3) imeeleza wazi kwamba pawepo na daftari la kudumu la wapiga kura. Kwa kuwa haya tayari yameshaelezwa katika Katiba, hapana budi yatekelezwe maana haya ndiyo makubaliano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Bajeti kifungu hiki kimetengewa fedha kidogo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni vyema basi fedha kwa ajili hii ziongezwe ili kazi ifanyike kabla ya uchaguzi ujao wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nne, nchi yetu imekumbwa na wimbi kubwa sana la ujambazi kiasi kwamba wananchi wengi wamefadhaika sana. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo ufumbuzi wake hauwezi kupatikana kwa kufumba na kufumbua macho bali panahitajika mbinu, utaalam na mikakati maalum ili papatikane ufumbuzi. Hapana budi pafanyike uchunguzi wa kina kujua nini chanzo cha ujambazi huu wa aina yake hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wengine wanadhani ni kukithiri kwa umaskini katika jamii hivyo mtu hana budi ila afanye vitendo vya ujambazi ndio apate mahitaji yake. Baadhi ya watu wanadhani ni kutokana na ukosefu wa ajira kwa kuwa vijana wengi hawana kazi ya kujiingiza mapato basi kuamua kufanya vitendo vya uhalifu ili ajipatie chochote. Ili tuondokane na balaa hili la ujambazi, lazima Serikali ichukue hatua za makusudi katika kulitokomeza balaa hili.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hatua wanazochukua hasa baada ya kupata kipigo cha kuuwawa askari wake. Hiyo juhudi iendelezwe isije ikawa ni zimamoto.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaunga mkono kama utatoa maelezo kuhusu hayo niliyoyaeleza. Ahsante sana.

**MHE. OMAR JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa kwa kweli ni nzuri hasa ukilinganisha wakati wa uchaguzi mdogo wa Majimbo 17 kule Zanzibar ulikuwa wa huru na wa haki na hii imetokana na kuheshimiwa muafaka uliotiwa saini kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha *CUF.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu daftari la wapiga kura la kudumu ndiyo kitu pekee ambacho kinaweza kuweka mazingira mazuri ya utulivu pamoja na kuaminiana wakati wa uchaguzi ujao wa mwaka 2005. Lakini pia haitoshi kuweka daftari la wapiga kura tu bali pia ni lazima kuwe na Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itavishirikisha vyama vyote vya siasa ambavyo vimepata usajili wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali kushauriwa kuondoa kodi ya maendeleo hasa ukizingatia kwamba kodi hiyo ilikuwa haileti hasa hayo maendeleo yenyewe bali ilikuwa ni udhalilishaji wa wananchi tu, pia mwananchi kumlipisha kodi ya kichwa ilikuwa ni sera za kikoloni.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuhusu suala la Ukimwi, sasa limekuwa ni janga la Taifa kwa hiyo Serikali ni lazima itafute suala la kupambana na Ukimwi kwani mila zetu za mavazi tumeziacha bali tunafuata mila za nchi za Magharibi na watu wanatembea wakiwa ni kishawishi mbele za wanaume.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme, limekuwa ni kero kwa nchi nzima, kila Wilaya wanadai umeme kwa hivyo Serikali isikie kilio cha wananchi ili waondoshewe kero hii hasa ukizingatia umeme ndiyo kichocheo cha kuleta maendeleo.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Bajeti yenye mwelekeo wa kutoa kero za wananchi kwa mwaka 2003/2004. Ni tegemeo langu kwamba Bajeti hii itatekelezeka na kuonyesha kweli kwamba Serikali inapunguza kero za wananchi. Pamoja na pongezi hiyo naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika Bajeti imeainisha dhamira ya Serikali ya kuanzisha Benki kwa ajili ya wakulima. Nashauri Serikali isijiingize katika uanzishaji wa Benki nyingine wakati tuna Benki zenye mitandao. Kuanzisha Benki huwa gharama kubwa ya mahitaji ya majengo, vifaa na mtaji. Tunayo Benki ya *NMB* ambayo ina mtandao nchi nzima hivi kwa nini tupange mbinu ya kuanzisha Benki nyingine? Tuanzishe Benki halafu kesho tulazimishwe kuibinafsisha?

Mheshimiwa Spika, ninakataa kata kata kuunga hoja ya kuanzisha Benki mpya, tuitumie Benki yetu ya *NMB* yenye mtandao nchi nzima. *NBC* imeuzwa wanunuzi wamepewa majengo *at 0 value,* hivi kweli Serikali iko makini? Leo Serikali ikaombe kuchukua majengo ya Matawi yaliyoachwa na *NBC* tuone kama hatuambiwa mamilioni. Hivyo sikubaliani kuanzishwa kwa Benki mpya.

Mheshimiwa Spika, pili, ubinafsishaji. Katika hotuba yake ukurasa wa 18 Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumzia ubinafsishaji na kuonyesha kuwa kumekuwa na ufanisi mkubwa. Naipongeza sana Serikali. Lakini dhana hii ya ubinafsishaji tunahitaji kuipitia upya na kuona kama kweli tumepata ufanisi au kama kuna matatizo sehemu nyingine. Inawezekana tumefanikiwa *TBL, TCC* na Saruji Tanga lakini ubinafsishaji wa *NBC* una maswali mengi. Je, Serikali inajua matatizo yalipo pale? Je, Serikali inajua jinsi *Absa* wanavyochota fedha zetu kwa mbinu?

Mheshimiwa Spika, tusiridhike na hundi tunazopewa, hebu tuwasikilize Watanzania wanaopigania haki zao na mali ya Watanzania. Kwa nini Serikali imekaa kimya na haitaki kuwasikiliza wala kuwasaidia watumishi wazalendo waliopo *NBC?* Msitake tuamini kwamba wakubwa wote mmenunuliwa. Ofisi ya Waziri Mkuu kama msimamiaji Mkuu wa Serikali, isitumia mabavu iwasaidie wafanyakazi wale tusije kugeuzwa watumwa ndani ya nchi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tatu, ukurasa wa 20 - 21 Mheshimiwa Waziri Mkuu, anazungumzia ushuru wa forodha katika nchi za Afrika Mashariki. Nampongeza kwa hatua hiyo ya kuwahimiza Watanzania waingie kwa bidii katika biashara. Je, Serikali imewaandalia Watanzania mazingira mazuri? Wakati wenzetu Kenya wamepunguza *tariff* ya umeme sisi Tanzania bado gharama ya umeme ni kubwa, je, viwanda vyetu vitakuwa na uwezo wa kushindana na vya Kenya? Kwa nini tunaingia kwenye makubaliano bila kuandaa mazingira yatakayowawezesha wananchi kuingia kwenye ushindani? Angalia *exchange rate* kati ya *Tanzania shilling* na *Kenya shilling* inatisha,

ushindani wa kibiashara tutauweza? Naomba tuwe makini katika kutafakari na kuweka mikakati ya utekelezaji maana wenzetu ni wajanja na sisi ni wajumbe ndio.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Gesi ya Songosongo. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema watu wa Lindi na Mtwara watafaidika na gesi hiyo, hivi gesi hiyo tutaitumia vipi? Majiko ya gesi ni ghali, ni mazingira yapi yameandaliwa ili kuwawezesha wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara waitumie gesi hiyo? Hadi leo sielewi mantiki ya kuondoa gesi pale hadi mitambo ya umeme Ubungo, Dar es Salaam na kuunganisha katika gridi ya Taifa wakati Mikoa ya Lindi na Mtwara haina umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wananchi wa Lindi na Mtwara tuendelee kubaki bila umeme wakati raslimali ambayo ingetukomboa inakuwa *pumped out, why?* Kweli Kusini tunadharauliwa kiasi hicho. Mwekezaji gani atakuja Kusini kama hakuna umeme wa uhakika? Au ndiyo *Magnetic South* kila kinachowafaa kinanasa na hakiwezi kutumika Kusini? Mbona korosho zetu ndiyo moja ya zao kuu linaloleta fedha za kigeni. Jamani tupatieni umeme kwa gesi yetu tumechoka kusahauliwa kila siku.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima kubwa na kwa fahari, naomba nitoe mchango wangu mdogo katika kuiunga mkono hotuba hii ambayo imewasilishwa katika Bunge hili kwa kiwango cha juu na kwa hakika imetayarishwa kitaalam kabisa na walioitayarisha wameonyesha kuwa ni wataalam wanaolingana na wakati wenyewe wa kuielezea kwa wananchi ambao wanajua mahitaji yao na wanafahamu mambo na wala siyo mbumbumbu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani zangu ambazo kwa kweli hazina mpaka, nathubutu kusema kuwa hotuba hii imetolewa ili kukidhi kiu zetu sote pamoja na hata hao watani wetu wa upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika msema kweli ni mpenzi wa Mungu na mtenda haki malipo yake atayakuta kesho mbele ya haki na kwa tabia inayoelezwa kila siku na Viongozi kulingana na Chama cha Mapinduzi yanahimiza kuwa nyamaza usiropoke ukikosa la kusema na *wallah* hotuba hii haikubakisha kuyaeleza kwa wananchi kuielewa Serikali yao na maana inavyofanya kazi zake kama ambavyo chama kilivyoagiza kulingana na sera yake ama kwa hotuba hii kwa sababu imeandaliwa na wanadamu ni budi tu tuongeze baadhi ya mawazo ambayo kila mtu ataona aongeze kwa kuongeza ladha kama tabia ya mwanadamu na ninakubaliana na *constructive suggestions.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ofisi hii ndiyo inayohusika na uhai wa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ingawa chini yake zipo Wizara nyingi zinazoendeshwa na Serikali hii nimeshawishika sana kuelezea yale ambayo naona niyaseme kwako.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuwa Ofisi zetu zote za Muungano na zisizokuwa za Muungano hiki ndicho kitovu na napenda sana kupongeza ushirikiano uliopo baina ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna ambavyo mnafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Hata hivyo,

bado tunalazimika kutanabaisha kuwa maingiliano ya Ofisi hii na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Zanzibar hayajafikia kiwango ambacho naridhika nacho.

Mheshimiwa Spika, hakuna hata mmoja mwenye umri unaopita miaka 45 asiyetambua makusudi ya kuasisiwa Muungano wa Tanzania na maagizo ya Serikali zetu mbili ambazo zinafanya kazi hapa Tanzania. Nadhani madhumuni ya Muungano si kuelekea kwenye Serikali tatu, bali ni yenye mfumo wa kuelekea kwenye uimara wa Serikali inayomudu kutoa huduma nzuri za Serikali imara zaidi kwa watu wake ambao wako wa asili moja na damu moja. Ndiyo maana nikasema kuwa sasa wakati umefika kwa Serikali zetu zote mbili kupanua wigo zaidi kwa kuweza kufanya mambo muhimu yanayoleta nguvu za Muungano ambapo hapo awali kulikuwa na kisingizio cha kusema kuwa si mambo ya Muungano. Nadhani wasia wake Sheikh Alhaji Ali Hassan Mwinyi , aliotuambia twende na vitabu vyake kulingana na karne tuliyopo, kweli umesibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika ninaridhika sana na namna ambavyo Tanzania Bara inafanya kazi yake kwa nidhamu ya hali ya juu, lakini ninaumia sana kuona kuwa kuna dalili ya ndugu wawili kuwa wanafanya mambo yao kila mmoja na lake tofauti na mfumo wa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba ni tuwe wamoja na wala hatuna sababu ya kufanya mambo kwa kudharauliana na kuepuka kabisa tabia ambayo inaweza kuleta hisia ya kuwa nani bora na nani mjinga. Sidhani kama hatujui kuwa Tanzania ni Muungano wa Jamhuri mbili ambazo zina haki sawa, lakini lazima tujenge tabia ambayo imekwisha asisiwa tokea Aprili, 1964 ambayo imeeleza bayana namna ndugu wawili, baba mmoja na mama mmoja waende vipi kwa kunufaishana.

Mheshimiwa Spika, katika jambo ambalo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kufanya juhudi ya ziada ya kutanua uhuru wa Watanzania wa nchi hizi mbili kuona tunajuana zaidi na wala tusiwe na hisia za kutiliana mashaka miongoni mwetu. Kwetu sisi ni kufufua zaidi hisia za wazee wetu ambao sasa hatunao tena, wao wako mbele ya haki, lakini nina hakika iwapo nchi hii itakuwa na fadhaa huko tunakokwenda, wallahi tutakuja kuwa Masuuli kwa Mungu kesho mbele yake.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kurejea maneno yangu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba isituache Zanzibar tufanye mambo yetu peke yetu na ninaitakia kheri, baraka na fanaka kwa yale yote waliyopanga kuyafanya. Jimbo la Kitope na watu wote tunaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Mungu ataendelea kukusaidia katika kazi yako nzito.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kupitia maandishi haya nichangie machache katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake hapa Bungeni iliyojaa maelezo mazuri na takwimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala zima la Ofisi za Wabunge. Ni lini Ofisi hizi zitajengwa katika Majimbo ya Uchaguzi? Je, kwa hivi sasa ambapo Waheshimiwa Wabunge hujitafutia mahali pa kufanyia kazi, ni utaratibu gani uliopo wa kuwawezesha kuendesha Ofisi hizo wakati wanasubiri kujengewa Ofisi hizo?

Mheshimiwa Spika, pili, Waheshimiwa Wabunge wanatarajia kufanya kazi nzuri ya kuwakilisha Majimbo yao na hata Vyama vyao vya Siasa, lakini wasaidizi wao wanalipwa fedha ndogo ambayo haiwezeshi kupatikana msaidizi mwenye uwezo wa kufanya utafiti, kuandika michanganuo ya miradi na hata kufanya mawasiliano muhimu kama Mbunge hayupo. Suala hili liangaliwe, Msaidizi wa Mbunge awe mwenye sifa ya taaluma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia alizungumzia ongezeko la wakimbizi, majambazi na silaha zinazomilikiwa kinyume cha Sheria. Hali hii imetia hofu maisha ya Watanzania na mali zao, wao wenyewe wako mashakani. Pamoja na wito wa kujilinda sisi wenyewe na mali zetu, Serikali haioni kuwa ulinzi wa Sungusungu kama ilivyo sera ya CCM, ungetiliwa maanani na ukasimamiwa ili uweze kuanza nchini kote kwa nguvu zote? Ulinzi huu ukirejea nina imani majambazi yataogopa na ujambazi unaweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia uanzishwe utaratibu wa kuwaripoti wageni kwa uongozi wa mitaa na vitongoji ili kila mgeni ajulikane alikotokea, yuko kwa nani na ana shughuli gani. Aidha, pawepo vitambulisho vya wakazi ili kila mmoja awe nacho. Ikiwezekana pia iwepo *movement order* inayotolewa na kiongozi wa mtaa au kitongoji kwenda kwa uongozi wa mtaa au kitongoji kule aendako mhusika.

Mheshimiwa Spika, nne, napongeza utaratibu wa Serikali wa kutenga fedha za kusaidia kielimu kwa watoto wanaofaulu kuendelea na masomo. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali iweke utaratibu mzuri, uwe wazi na historia ya kila mtoto ijulikane, iwapo ni yatima au familia ina uwezo mdogo iwe wazi. Aidha, jinsia izingatiwe, watoto wa kike na wa kiume wasaidiwe sawa sawa, pasiwepo na upendeleo wa jinsia moja. Ilitokea wakati fulani watoto wa kiume wakawa hawana msaada, sasa isije kuwa zamu ya watoto wa kike. Watoto wote ni sawa.

Mheshimiwa Spika, tano, napenda Halmashauri ziangaliwe kwa karibu ili kuondokana na tatizo la kifedha ambapo hati chafu zinakuwa nyingi sana. Katika kipindi hiki ambapo Serikali Kuu itazipa fedha nyingi Halmashauri, fedha zifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, napenda sasa kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Rais, Makamu wake na hasa Mtendaji Mkuu wa Serikali hii, Mheshimiwa Frederick Sumaye na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kazi anazozifanya ndizo zinazoifanya Serikali hii angalau kuanza kukidhi maeneo mengi ya matatizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema mengi ya mambo Serikali yetu iliyoyafanya, lakini kama nilivyoanza sifa zote zingeelekezwa kwa Mtendaji Mkuu, mambo yangekuwa mabaya basi yeye ndiye angelaumiwa. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitatoa maoni na maombi hasa yale yanayogusa Jimbo langu la Songwe. Kwa maoni, kwanza, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, awahimize tena viongozi wa Wilaya kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge, kutekeleza amri yake ya kukamilisha majengo ya shule za msingi na uboreshaji wa madawati.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la chakula kila Kijiji, Kata, Tarafa na Wilaya watoe taarifa mara moja kwake juu ya hali ya chakula na kusiwepo na uuzaji holela. Hali sio nzuri hata katika Jimbo la Songwe ambako chakula sisi tunapata vizuri karibu kila mwaka, mvua zimenyesha kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mheshimiwa Waziri Mkuu apewe taarifa rasmi ya watoto waliofaulu na hawakupata nafasi ya kuendelea na shule za sekondari kutokana na uhaba wa shule.

Mheshimiwa Spika, nne, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aangalie uwezekano wa mwaka kesho kuongezwa kwa watoto walipiwao na Serikali kuingia Vyuo Vikuu, idadi ya sasa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, tano, kuwepo na utaratibu rasmi wa kuangalia utendaji kazi wa Makatibu Tarafa na pia uwepo uwezekano wa kuwabadilisha wale waliokaa kwa muda mrefu, kwani hawawezi kutekeleza maelekezo yake na ya Serikali kwa sababu ya kuwa wazito na kutojua wajibu wao. Vile vile kwa Ma-*WEO* na Ma-*VEO*.

Mheshimiwa Spika, sita, kuwepo na uhamisho kwa Ma-*RAS* (Makatibu Tawala wa Mikoa) nao wamekaa sana kwenye Mikoa waliyopo. Hebu Mheshimiwa Waziri Mkuu nao wahamishe, mambo mengi yatajitokeza.

Mheshimiwa Spika, saba, Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie uwezekano wa kulipa mishahara au posho inayofanana kote nchini kwa Halmashauri zetu, ni vyema wapewe Madiwani haki hii kwa sababu muda wote wanakuwepo kutekeleza na kusimamia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu njia ya umeme ya Galula, Kanga, Mkwajuni ambapo umeme upo, ikamilishwe kwani ni muda wa miaka minne hivi nguzo zimewekwa bado kusimamishwa na kufunga nyaya. Hii ni mbaya kwa wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, naomba kufikiriwa kuhusu barabara ya kutoka Galula - Namkukwe. Barabara hii ni ya Mkoa na sio kweli kwamba inagharimu makisio ya shilingi bilioni 16 ambayo ni kilomita 57 tu, nalo ni tatizo na majibu ya kila siku hapa. Jimboni haieleweki kwa wapiga kura wangu angalau ingetengenezwa kwa awamu toka mwaka 1995 nilipoingia Bungeni ingekuwa imekwisha.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba itengenezwe kwa awamu toka Galula - Magamba na baada ya Magamba - Namkukwe na halafu iendelee kwenda Mbozi na Sumbawanga na ndio barabara fupi sana kwenda Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, wananchi bado wanashangaa kwa nini barabara ya Saza - Kapalalai haitengenezwi walau kwa kiwango cha changarawe. Naomba msaada wako juu ya barabara hii, ni ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, wananchi hata utakapokuja wanaomba Wilaya, majengo yapo na yameanza kuchakaa, wanahoji ni lini watapata Wilaya ili kukamilisha utekelezaji wa Serikali Kiwilaya. Naiomba Serikali kutoa fedha ya kukarabati ni muda mrefu umepita pasipo kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri ambayo imegusa karibu kila sekta na yenye kutia matumaini. Hii inaonyesha kazi ya usimamizi wa utaratibu ilivyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini Bajeti au hotuba nzuri haitakuwa na maana mpaka pawe na nidhamu katika utekelezaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu lazima ajenge nidhamu kuanzia kwa Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili kila mmoja atimize wajibu wake na asiyewajibika ipasavyo awajibishwe. Nidhamu imeshuka sana Serikalini, hata kujibu barua hawajibu. Hata wakati baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanachangia hotuba hii jana tarehe 24 Juni, 2003 huku wakiwataja baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri, kulikuwa na Waheshimiwa Mawaziri wanne tu Bungeni, wawili wakiwa Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi. Hii si nidhamu nzuri hata kidogo hasa ukizingatia Bajeti iliyokuwa inajadiliwa ni ya *boss* wao.

Mheshimiwa Spika, sasa ni zaidi ya miaka 28 tangu Serikali iamue kuhamia Dodoma, lakini hakuna cha kujivunia sana. Viwanja vilivyokuwa vimetengwa kwa ajili ya Balozi na Mashirika ya Kimataifa wamegawana wakubwa, hata maeneo ya *Marina Five Star Hotel.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya kudhibiti ujenzi wa nyumba za Serikali na Mabalozi Dar es Salaam imevunjika, bodi sasa si ya Makatibu Wakuu kama zamani

ilivyokuwa ili kuharakisha utekelezaji wa maamuzi. Watu waliokuwa wamewekeza vitega uchumi Dodoma kwa kuamini Serikali itahamia Dodoma, wanadaiwa na wengine wamefilisiwa kwa kosa ambalo si lao bali la Serikali.

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 71 zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ni ndogo mno na haionyeshi *seriousness* ya Serikali kuhamia Dodoma. Hivi shilingi milioni 629 za mishahara, hawa watumishi kweli wanahitajika?

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali itoe ratiba thabiti ya kuhamia Dodoma na iizingatie. Ianze na Wizara nyeti kama Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Waziri Mkuu atekeleze ahadi yake ya kuhamia Dodoma na akae Dodoma.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ufanyike ili shughuli nyingine za *CDA* zihamie *DOWASA,* Manispaa na *NHC*. *CDA* ibaki na miradi ya maendeleo na ipewe fedha za kutosha.

Kuwe na dhamira au utashi wa kisiasa kuhamia Dodoma. Nachelea kukubali kuwa Serikali inapata kigugumizi kuhusu baadhi ya Mikoa ukiwamo Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, miaka 42 baada ya Uhuru, Mkoa wa Kigoma hauna umeme wa uhakika wakati Sera ya *TANESCO* ni kupeleka umeme vijijini. Kwa nini wengine wapate umeme vijijini wakati hata makao makuu ya Mkoa wa Kigoma hakuna umeme wa kuaminika? Huwezi kuzungumzia *EPZ* inayolenga kupelekwa Kigoma bila umeme. Tunahitaji umeme wa uhakika toka maporomoko ya Igamba na si kuhemea umeme toka nchi jirani ambayo usalama wake ni wa mashaka. Tunahitaji barabara ya kutoka Kigoma hadi Tabora kuwezesha hata wakulima wa nyanya wa Kazulamba kupata soko la uhakika.

Ukimwi ni janga la Taifa lakini haichukuliwi kwa umakini unaostahili. Hata hotuba ina paragraph mbili tu katika aya 87! Janga likabiliwe kwa nguvu zote. Naipongeza *TACAIDS* kwa elimu inayotoa kwa jamii kuhusu maambukizi ya Ukimwi hasa maeneo ya Mjini. Sasa ni wakati wa kuelekeza nguvu vijijini ambako elimu na ufahamu kuhusu Ukimwi bado ndogo mno.

Kwa kuwa *TACAIDS* haiwezi kufika kote, iteuwe mawakala ambao watafanya kazi hiyo badala yao kama ilivyofanyika Bima ya Afya. Mafunzo zaidi yatolewe kwa Kamati za Ukimwi za Kata.

Ni muhimu kuanzisha Ofisi ya Msemaji wa Serikali ambayo itazungumza mambo yote yanayohusu Serikali badala ya mtindo wa sasa ambao kila mtumishi wa Serikali anakuwa msemaji wa Serikali. Maelezo si msemaji wa Serikali kwa mapana yake. Ni vema taarifa za Serikali zikatoka chanzo kimoja baada ya kuchujwa ipasavyo. Ni muhimu zaidi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambapo wanamsemaji wa Jeshi la Polisi.

Katika safu ya utendaji wa kazi za kila siku, *RPC* huwajibika moja kwa moja kwa *IGP* na si kwa Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Hii inaweza kuleta tatizo kama *RPC* atakuwa jeuri na asiyemheshimu *RC*.

Serikali imefanya kazi nzuri kudhibiti dawa za kulevya. Ni vema ikatafuta vigogo wa biashara hii na si kuwafunga tu vijana wadogo wanaotumiwa tu. Taifa lingependa kujua nini kinaendelea kuhusu sakata la kiwanda cha Dawa za Kulevya kilichofichuliwa Dar es Salaam na kwa nini kesi za wazito kama hawa zinacheleweshwa sana na kuishia kufutwa.

Nashauri pia Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ihamishiwe Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwenye utaalamu wa upelelezi badala ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Naipongeza Serikali kwa hatua thabiti ilizoandaa kukabiliana na njaa, lakini tuwe makini kutopandikizwa vyakula vilivyoongezwa virutubisho ambavyo vinaweza kuwa hatari kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Kufuta kodi ya maendeleo kutasaidia sana kuondoa kero zilizokuwa zinawakera wananchi wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, viongozi tuwe mfano katika kuendeleza kilimo. Hivyo iwepo mikakati maalum ya kuwezeshwa sisi kwanza ili tunaowasimamia waweze kujifunza na kuiga.

Mheshimiwa Spika, kasi ya kupiga vita madawa ya kulevya iendelee.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu nami kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwashukuru Vyama vyote vya Upinzani hasa Chama changu cha *UDP* kilichopita kikizungumzia kero ya wananchi na kuulizwa faida ya utoaji wa kodi ya maendeleo na hata mimi ukiangalia kwenye *Hansard* ya mwaka 1996 na 1997 utaona nilizungumzia sana jinsi wananchi wanavyopata shida kwa ajili ya kushindwa kulipa kodi na jinsi akina *Village Executive Officers(VEO)* wanavyochukua kuku, ng'ombe, vyombo vya nyumbani na kadhalika hadi nikasema kuku wamewatambua Ma-*VEO/WEO* huwa wakikamatwa na *VEO* hulia *VEO, VEO* na wakifikishwa kwa *WEO* hulia *WEO, WEO, WEO.*

Mheshimiwa Spika, ningepata nafasi ya kuchangia kwa kusema ningeimba au kulia *VEO,* kama kuku anavyolia. Sasa kwa kifupi wananchi hasa wa Kanda ya Ziwa

hasa Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza wamefurahi ajabu. Hii inaonyesha jinsi ilivyo vizuri kuwa na Upinzani yaani kioo cha Chama kinachotuongoza, inaonyesha Upinzani yaani sisi tunajali. Sisi tulisema kero ya wananchi nanyi mliona madaraka, mnajali pia, mmesikia kilio chetu. Kwa misingi hiyo basi, tupongezane wote, kwani wote ni *Victory.* Hongera sana na tuendelee kufanya kazi kwa kushirikiana hivyo kama Taifa kwa maendeleo yetu wote Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, nataka kuzungumzia kitu kidogo lakini kikubwa sana kwa mchango wake. Majuzi 17 Juni, 22003 mimi nilikuwa narudi toka Johannesburg, Afrika Kusini pale Kiwanja chetu cha Kimataifa Dar es Salaam tulipokelewa na wimbo wa Kihindi, kama tunaingia *Bombay.* Sababu kwa kweli sikuelewa. Mimi nafikiri hapo tunatakiwa kupokelewa na nyimbo za kiswahili au za makabila ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, tuna nyimbo nyingi ajabu na nzuri za Kinyamwezi, Kisukuma, Kindamba/Kipogoro, Kigogo, taarabu toka Mikoa ya Pwani/Zanzibar na kadhalika. Kwa nini tusiwe *proud* na nyimbo zetu na kuwaweka wageni wetu kwamba sasa wanaingia Tanzania na kujua utamaduni wetu tofauti na wanakotokea. Naomba suala hili lishughulikiwe ipasavyo. Ni lazima tulingie utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala huwa linanitatanisha sana na huwa sielewi hasa kwa nini inakuwa hivyo hasa nikizingatia kuna jicho la Serikali. Vijana wetu wanaathirika sana na madawa ya kulevya. Hawa vijana sio source kwani wao wananunua tu. Sasa wahusika wanaoingiza madawa ya kulevya wanayaingizaje pale *DIA* bila kukamatwa? Hii ni dhahiri kuna mwanya wa rushwa

Mheshimiwa Spika, mimi naamini *PCB* itafanya kazi vizuri bila kuona aibu, sababu ni vigogo wanaofanya biashara hii, vijana wanatumiwa kwa sababu ya njaa na kukosa ajira na wengine utajiri wa haraka haraka. Kama kweli tuko *serious* tunaweza kuzuia hii biashara katika njia zetu za kuingilia hata kama njia ni za panya, askari kanzu wakienda huko watawakamata kwani inajulikana.

Mimi naamini kama alivyosema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kwamba: *"It can be done, play your part."* Kila mtu akitimiza wajibu wake ipasavyo mambo yatafanikiwa. Naomba basi wale wote wahusika wafuate ushauri wa Baba wa Taifa ili kuwaokoa vijana wetu. Kinondoni ndiyo moja ya eneo la vijana wavutaji wa madawa haya, kazi kwenu.

Mheshimiwa Spika, kule Igunga kuna sehemu zinazojulikana hata kwa askari kwamba kuna majambazi yapo hapo yananyang'anya mali za watu hasa magari, askari wanasema hawana silaha kama za hayo majambazi. Naona hili ni tatizo la Taifa.

Naomba Serikali iwaongezee Bajeti Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili wapate nyenzo, wafanye kazi ya kutulinda ipasavyo, kushindana na majambazi ya ndani na yanayotoka nje. Pia naomba wakimbizi wote wawekewe kambi nchini mwao. Tusiruhusu wakimbizi na tuwe makini sana na wageni wanaoingia nchini na wakiingia

tuwafuatilie kujua wanachofanya. Narudia tena yale aliyoyasema Baba yangu Mwalimu Nyerere: *"It can be done, play your part."*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwisho wa uchaguzi ni mwanzo wa uchaguzi unaofuata, kweli wakati huu ndiyo wa maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2005. Vyama vya Siasa na Tume vina kazi kubwa ambayo vinatakiwa kufanya, Vyama vya Siasa kuelimisha wananchi ili wajue haki zao na hasa haki ya kupiga na kupigiwa kura kwa uhuru kabisa bila woga. Vyama vya Siasa lazima vikubaline kwa vitendo kuwa na Tume ya Uchaguzi Huru na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba kwa Serikali ya Zanzibar kutokana na muafaka wamekubaliana kuwa na Tume ya Uchaguzi mseto yaani huru. Kila mshika dau ana mjumbe mfano *CUF* wajumbe wawili, CCM wajumbe wawili na uteuzi wa Rais wajumbe watatu. Hii angalau wamefikia mahali, maana ni lazima tuanze mahali. Sasa wenzetu wamefikia muafaka kwa kupitia historia ambayo imetia dosari nchi yetu. Lakini nchi hii ni moja na kuna Wabunge kutoka Zanzibar wanaingia Bunge la Tanzania. Kwa misingi hiyo naomba kama Watanzania wote, tusibaguane, tuwe wote na Tume Huru ya Uchaguzi kama Zanzibar na mambo mengi ambayo yanadaiwa kila mara toka Tume ya Uchaguzi/Vyama vya Siasa, naomba yatekelezwe ili tuwe na uchaguzi mwaka 2005 wa haki na huru.

Mheshimiwa Spika, naona nimalizia kwa kumpa pongezi mwanamke mwenzangu, mdogo wangu, Betty Mkwasa, kwa ushindi alioupata hapa majuzi. Kweli kama mwanamke ametupa changamoto sana hasa wanaume ambao bado wanakasumba kwamba watoto wa kike hawawezi. Hivyo kwa kuona Betty Mkwasa ametutoa na kutufanya turinge kama wanawake, turinge. Nawaomba wazazi watoe nafasi kwa kujali vipaji vya watoto wote sawa wa kike na wa kiume. Kwa Taifa ameiwezesha Tanzania kujulikana.

Kwa hiyo, kwa kupitia Wizara hii namba afikishiwe pongezi zangu binafsi. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, niliona niache kuchangia kwa sababu ya kuona karatasi ya kwanza ya kuchangia kwa maandishi imejaa lakini dhamira yangu inaona sijatimiza wajibu wangu ndio maana nimechukua karatasi ya kuchangia kwa maandishi mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, naamini hutajali sana hivyo kuniruhusu tena kuchangia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia suala la Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Enzi za mfumo wa chama kimoja, Waheshimiwa Wabunge hawa watano toka Zanzibar walikuwa wanahitajika ili ku-*balance,* Tanganyika na Zanzibar ili wakati wa kupiga kura wasimezwe sana kwa namba au uwingi wa kura za Bara na Kisiwani. Lakini sasa tuko kwenye Mfumo wa Vyama vingi na kila Jimbo la Uchaguzi la Bara na Kisiwani, kwa misingi hiyo tuna wawakilishi

wa wananchi yaani Waheshimiwa Wabunge kwa nchi nzima Tanzania. Kama ndivyo basi ya nini kuwa na watu wengine wa ziada hasa ukizingatia nchi yetu ni maskini tena uliokithiri. Kuwalipia watu hawa kila kitu kama haki za Wabunge, kwenye vikao na kadhalika ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuwa nao kiubabe hakutusaidii kitu na wala sio busara kwani kama nilivyosema hapo awali tuna wawakilishi na Wabunge kwa kila Jimbo la Uchaguzi Bara na Kisiwani. Hivyo basi, sasa ndio wakati muafaka wa kutoa kipengele hiki kwenye Katiba yetu na hivyo kupunguza Wabunge wasio wa lazima na gharama zisizo za lazima, kwani Wabunge wapo wahusika na Majimbo yote. Kama tunapunguza wafanyakazi katika mashirika ya umma kwa ufanisi zaidi na uzalishaji na huduma bora zaidi basi ni wakati muafaka sasa kuwatoa Wabunge hawa na kusema kweli wanahudhuria kwa manati.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie Waheshimiwa Wabunge kumi walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Hawa kama unakumbuka walikuwa wateuliwa na Mheshimiwa Rais kutoka kwa makundi maalum mfano wazee kama Mzee *Chief* Abdallah Fundikira hapo safi, vijana nako kidogo safi, ila mgongano unakuja umri wa kijana unaishia wapi? Wengine waliotakiwa kuteuliwa ni walemavu.

Sasa unajiuliza nani kaingia Bungeni kwa niaba ya walemavu kupitia kiti hiki kwani kuna wengine wametuliwa si vijana na wala si walemavu.

Mheshimiwa Spika, pia nilifikiria lengo la kuwateua hawa Waheshimiwa Wabunge kumi lilikuwa labda kujihami kwamba huenda CCM ingekuwa ina Wabunge wachache, hivyo Mheshimiwa Rais apewe madaraka ya kuteua Wabunge kumi. Lakini ilivyotokea ni kwamba Wabunge wengi waliopita ni wa CCM, kimantiki, ilikuwa haina haja ya kuongeza Wabunge kumi ambao wote wanatoka CCM. Ingekuwa safi kama Mheshimiwa Rais angeteua toka Upinzani ili kutoa changamoto kwa upande wa pili wa shilingi kwani kinyozi hajinyoi ni lazima aweke kichwa chake anyolewe hata kama ni kionyozi stadi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hii ni tumaini langu hasa tukizingatia uwingi wa Wabunge kupitia CCM, naomba nafasi zilizobakia ziteuliwa toka *CUF* licha ya ile moja toka *CUF* kutokana na muafaka. Nasema hivyo kwa sababu baada ya kuchaguliwa Rais anakuwa Rais wetu wote Watanzania. Naye kama baba anatakiwa na inampasa haswa kuangalia, kulea wote bila ubaguzi si wa Chama tena ni wajibu wake kutusikiliza wote, kutuongoza wote kwa manufaa ya Taifa. Tukimpata Rais mbaya, atatuongoza na kutunyanyasa na akiwa Rais mzuri mambo *bie* kwa wote si wana CCM tu ila sisi wote kama Watanzania.

Kwa kuwa mimi naamini Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ni mwema, naamini ataona au amekwishaona na atafanya hivyo ku-*balance* uteuzi huu. Kwa kweli tunaukosa mchango wao humu Bungeni na Taifa zima kwa ujumla wake, watu hawa maarufu.

Mheshimiwa Spika, kwa hapo baadaye mwaka 2005 na kuendelea, Marais watakofuatia kama Chama kitakachotuongoza kitakuwa na Wabunge wengi basi nafasi hizi ziende kwa wapinzani wa wakati huo hasa viongozi maarufu, wazee wenye busara, walemavu, wanawake na vijana ambao wana *interest* ya kuwa Wabunge ila wamebwagwa kwenye chaguzi kwa sababu moja au nyingine. Tusiwapoteze watu hawa kama siyo hivyo basi hakuna lazima ya kuchagua Wabunge ilimradi kujaza nafasi hizo. Naomba nimeeleweka vizuri tu tena kwa nia nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri ya Bajeti. Inatia moyo na matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nimepewa nafasi ya kuzungumza, naomba nikumbushe kwa maandishi, ukurasa wa 31 na 32 umezungumzia madini na umuhimu wake kwa Taifa.

Kwa upande wa Wilaya ya Geita maeneo ya madini bado hayajaonyesha *direct impact* kwa wakazi wa pale hususan suala la fidia ni tatizo na linabomoa Chama Tawala. Tafadhali ingilia kati wananchi walipwe fidia zao na waliohusika kuvuruga au kuiba pesa hizo wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, pili, ili kurudisha imani kwa wananchi wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo hayo, wapewe mikopo na wapelekewe umeme kwani watachangia sehemu kubwa ya pato la Taifa. Meremeta ianze kazi katika machimbo ya Rwangasa, Bukoli, Nyamgusu, Kaseme na Nyakagwe.

Mheshimiwa Spika, naomba mashirika ya reli yasaidiwe na Serikali hususan Reli ya *TAZARA.* Reli ya *TAZARA* ilijengwa na China ikiwa ni kwa uhusiano uliokuwepo kati ya Tanzania na Zambia. Ni aibu reli hii kufa wakati inatoa huduma katika nchi mbili. Naomba tuone aibu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la kusikitisha sana kwani China imekuwa ikiendelea kusaidia reli hiyo. Kinachosikitisha kwa pesa hizo za msaada kutoka China ni kwamba hutozwa kodi, kwa mfano wanaponunua mafuta ya *train* au vipuri. China haifurahishwi kutoa msaada huo ambao ahutimizi makusudio yao. Kweli haiwafurahishi wao hata mimi sifurahishwi na hili. Mwakilishi wa China aliwahi kuonyesha kutoridhishwa na suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa asikilize matatizo ya *TAZARA,* bado tunaihitaji reli hiyo kwani inatoa huduma. Ni aibu kushindwa kusimamia kitu tulichokipata kwa mkopo na hatujaanza kulipa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ila fuatilia hayo.

Mheshimiwa Spika, ya pili, ni ile tu ambayo inasema ilimradi amekanyaga mnada unamlipia kodi, hiyo nayo haitakuwepo. Zile zingine nitawaachia hao wataalam wa Wizara hizi kwa maana kama amenunuliwa. Kwa kweli kama amenunuliwa ni sawa sawa na mtu aliyeuza kahawa au mahindi ambaye analipa fedha. Ile *Livestock Permit* ya kutembea, nayo ni nzuri kwa maana ya kudhibiti uenezaji wa magonjwa na kujua ng'ombe wanakwenda wapi, ile nadhani haina tatizo. Kwa kweli hili la kusema tu ili mradi ng'ombe eti anapumua tu, basi analipa kodi hiyo hapana na ile ya kwamba amekwenda mnadani. Mtu alikuwa na shida zake amempeleka ng'ombe mnadani hakupata mtu wa kumnunua anamrudisha ng'ombe wake nyumbani unasema alipe kodi, hiyo nayo tumesema hapana. Kwa hiyo, nilipenda tu nitoe ufafanuzi katika hiyo, lakini ziko kodi zingine ambazo wanazifanyia kazi. Nina hakika kabla ya tarehe 1 Julai, 2003 watakuwa wamepeleka taarifa rasmi katika Mikoa na Wilaya ili watu wajue ni nini la kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kodi hizi za maendeleo. Tumesema Kodi ya Maendeleo imefutwa na ni kweli imefutwa. Sasa ninajua watu watapata utata wa kwamba kwa sababu mwaka wa Halmashauri unaanza Januari mpaka Desemba na kwamba hivi tunavyoongea kuna watu watakuwa wameshalipa kodi na wako ambao hawajalipa kodi. Sasa ukweli ni kwamba, wale ambao hawajalipa kodi kwa sababu tumeifuta hatuwezi kwenda kuwadai. Lakini wale ambao wamelipa nao hatuwezi kuwarudishia. Kwa hiyo, nilipenda niseme hili nalo lieleweke tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linahusu utendaji wa Serikali. Wako watu waliozungumzia sana utendaji wa Serikali. Imezungumzwa kana kwamba, Serikali haitekelezi majukumu yake. Jamani! Serikali ingelikuwa haitekelezi majukumu yake ingelionekana wazi. Lakini kama ni ule utekelezaji anaoutaka Mheshimiwa Halinga, uwezo wa kutekeleza namna hiyo tunao, lakini ndio tunaoutaka kweli? Kwamba Serikali lazima itishe, iogopwe na kadhalika. Hiyo itakuwa si Serikali ya watu. Kama ni ya kutisha tu na kuogopwa kila mahali watu wakimwona Kiongozi wa Serikali wanakimbilia vichakani, mimi nadhani hiyo itakuwa si sahihi. Mimi nafikiri la msingi ni Serikali itekeleze majukumu yake, lakini kwa kweli lazima iwe Serikali ya watu. Hatutaki kuleta Serikali ya kidikteta. Lakini Serikali lazima itekeleze majukumu yake. Hilo nami nakubali na mimi naamini kwa sehemu kubwa sana Serikali inajitahidi kwa kweli. Ndiyo maana huko tunakotoka tunaona mabadiliko makubwa. Shule zinajengwa, zahanati zinajengwa, miradi ya maji na kadha wa kadha. Sasa inawezekana kuna matatizo madogo ya hapa na pale lakini hayo ni sehemu ya utawala wa kawaida na ni lazima yashughulikiwe tu. *(Makofi)*

Baadhi ya Wabunge wamezungumza kwamba, fedha za Halmashauri zinaliwa tu kila mahali. Mimi nadhani katika Halmashauri zetu na sisi tuko mle mle. Baraza la Madiwani ndiyo linatakiwa lisimamie mambo haya. Sasa tusimamie basi maana sisi tuko humo. Tena Waheshimiwa Wabunge tuliomba tuwemo kwenye Kamati nyingi tu ili tudhibiti haya mambo. Sasa tudhibiti. Eeeh !!!. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye suala la madini. Nadhani hili la madini limejibiwa vizuri sana asubuhi ya leo. Inaonekana ni tatizo ambalo bado linatupa shida. Sasa mimi nataka niseme tu kwamba, Serikali imesikia *concern* ambayo imekuwa *raised* hapo. Tunalo tatizo kwamba tuna mikataba na hao watu, lakini tumesikia tuachieni tuone nini tunaloweza kufanya katika kuliangalia eneo hilo hata kwa baadaye kwa sababu uwekezaji katika eneo la madini bado unaendelea. Lakini kusema kwamba uwekezaji wetu haufanani, kwa sababu mimi nakumbuka taarifa ambazo tulikuwa tumeletewa kwamba, uwekezaji wetu haufanani na nchi zingine, si kweli unafanana. Inawezekana kuna tofauti za hapa na pale, lakini unafanana sana. Kama mnavyokumbuka huko mwanzo Tanzania haikuwa na uwekezaji katika madini. Kwa hiyo, tulikuwa na kazi kubwa pia ya kuweza kuwavutia watu waweze kuja kuwekeza katika madini. Kama hayo Makampuni hayakuja nina hakika mpaka leo hakuna mtu ambaye angeliwekeza kwenye madini. Sasa hayo Makampuni yamekuja Tanzania imeanza kufahamika. Sasa hivi tunafahamika katika dunia kwamba tuna madini. Mimi nafikiri sasa ni jambo jema tunaweza tukasema sasa unaweza ukazungumza na mtu kwa kuweza kutaka kupata kile unachokitaka. Lakini wakati ule ilikuwa ni vigumu sana.

Kwa hiyo, mimi nafikiri kuna maeneo mengi sana katika madini ambayo yanahitaji kuboreshwa. Hiyo ni kweli na tunaendelea. Mengine ni tatizo la utaalam hatukuwa nao mkubwa, mengine ni *resources* na mengine yanatakiwa yafanyike na hao hao wanaochimba. Kwa mfano hili tunaita la kusanifu. Sasa yale hayawezi kujengwa na Serikali yanaweza kujengwa na Makampuni yenyewe na wanaweza wakafanya hivyo kama wanaona kuna madini ya kutosha kufanya kazi kama hiyo. Lakini tunaendelea kushauriana. Mengine ni ya wachimba madini wetu wadogo, maana tusidhani tatizo liko tu kwa wachimba madini wakubwa hata kwa hao wadogo. Kuna maeneo ambayo yanahitaji yaboreshwe tunashauriana nao, tunazungumza nao na tunadhani baada ya muda maeneo yote haya yataboreshwa ili kupunguza huku kutokuridhika. Kwa hiyo, napenda tu kusema tumesikia *concern* ambayo Waheshimiwa Wabunge, mmeitoa hapa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Daftari la Wapiga Kura. Hili wamesema sana watu wa Upinzani wanafikiri kwamba, Chama cha Mapinduzi ndiyo hakitaki daftari. Sasa mimi nawaambieni nataka kuwahakikishieni kwamba, kama kuna mtu ambaye anataka daftari hilo liwepo ni Chama cha Mapinduzi. Nasema hivyo kwa sababu Chama cha Mapinduzi ni Chama Tawala na Chama Tawala mara nyingi hakichezi mchezo wa *foul.* Hili daftari litatusaidia sana sisi na mimi nataka kuwahakikishieni, tutahakikisha daftari linakuwepo na matokeo yake mtayaona. Kwa hiyo, tumetenga fedha kidogo za kuanzia lakini sasa hivi kuna Kamati ya Wataalam inaangalia njia nzuri na rahisi zaidi ya kuweza kufikia lengo hilo. Tuko pamoja kabisa na Tume ya Uchaguzi na ndiyo kazi ambayo tunafanya. Kwa hiyo, hili jambo linashughulikiwa na nataka kuwahakikishieni kabisa tutahakikisha linafanikiwa kabla ya Uchaguzi wa 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la vitambulisho nalo tunalishughulikia, bado tunalizungumza katika Serikali namna rahisi ya kuweza kufanikisha jambo hili. Mimi nina hakika na lenyewe pia lengo letu ni kuwa na vitambulisho katika muda mfupi kadri inavyowezekana. Tungelipenda sana angalau kabla ya kufika mwaka 2005 tuwe na vitambulisho, hili litatusaidia pia kwa upande wa kujua raia wetu, lakini pia itatusaidia

sana kudhibiti hali hii ya uhalifu ya watu kuingia nchini bila utaratibu. Tunajua tuna tatizo la Wakimbizi lakini tukiwa na vitambulisho bila shaka jambo hili litapunguza sana matatizo haya kama ya ujambazi na watu kuishi nchini bila utaratibu na kadhalika. Kwa hiyo, hili nalo tunalishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ukuaji wa uchumi ukilinganisha na huduma zetu za jamii na ongezeko la watu, hili alilizungumza Mheshimiwa Kimiti namshukuru sana. Ukweli ni kwamba, tunapozungumzia ukuaji wa uchumi ni lazima pia tuangalie vigezo vingine ambavyo vinaathiri uchumi huo. Sasa kigezo kimojawapo ni ongezeko la watu. Huduma za jamii yenyewe ni kama mlaji, kwa hiyo unapozalisha zaidi basi unazipeleka kwenye huduma za jamii na huduma za jamii mara nyingi hazina uzalishaji wa moja kwa moja unaoonekana, lakini baada ya muda utaonekana kwa sababu utakuwa na watu walio na elimu na wenye afya, utakuwa na watu wanakunywa maji safi, utakuwa na barabara nzuri, haya yote yatasaidia uchumi huko mbele ya safari.

Lakini nilitaka nizungumzie hasa hili la ongezeko la watu. Tatizo la ongezeko la watu ni kubwa katika nchi yetu. Wenzetu wa *UNFPA* walikuwa wamekadiria kwamba, Tanzania tutakuwa tunaongezeka kwa wastani wa asilimia 2.3 ambayo na yenyewe ni ya juu sana. Katika ulimwengu wa leo ongezeko lolote ambalo linakwenda zaidi ya asilimia 2 ni kubwa mno. Ni vigumu sana kuweza kupata uchumi wa kuweza kubeba ongezeko la namna hiyo. Unapokuwa na ongezeko kubwa maana yake pia watoto ni wengi. Sasa unapokuwa na idadi kubwa ya watoto maana yake una idadi kubwa pia ya watu ambao hawazalishi, wanakula. Wanahitaji chakula, kuvaa, wanahitaji kwenda shule, hospitali, kunywa maji na kadhalika. Kwa hiyo, unakuwa na idadi kubwa ya namna hiyo. Kwa hiyo, ni lazima suala hili la idadi ya watu au ukuaji wa idadi ya watu tuliangalie sana kama tunataka ukuaji wa uchumi uende vizuri. Kwa hiyo, ile mikoa kama Kigoma ambayo kiwango cha uzalishaji ni kikubwa mno, kwa kweli lazima tukafanye bidii kupunguza. *(Makofi)*

Mkoa wa Rukwa ...

**MBUNGE FULANI:** Hamna umeme

**WAZIRI MKUU:** Inawezekana pamoja na jinsi alivyosema Mheshimiwa Mayonga kwamba, anadhani giza ndilo linaloleta matatizo hayo. Mimi nadhani hata pamoja na kutokuwa na umeme tunaweza bado tukapunguza viwango hivi vya uzazi. Kwa kweli viwango vikubwa vya uzazi ni tatizo katika uchumi, hasa uchumi mchanga wa aina hii. Hili jambo watu wengi hawalielewi na Waheshimiwa Wabunge wengi hawalisemi kwenye vikao vyao kule vijijini. Lazima tulisemee hili. Tulizungumze wazi wazi tusione haya. Kwa hiyo, mimi ningelipenda sana kuona ongezeko la watu katika hii miaka kumi inayokuja kama tungeliweza tukafikia kiwango tuseme cha asilimia 1.5 angalau tusiwe zaidi ya asilimia 2 tungelikuwa na matumaini mazuri sana ya kukuza uchumi wetu. Lakini najua ni kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie jambo moja kwa kifupi tu, hili suala ambalo limezungumzwa na Wabunge wa Mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Rukwa na

Singida. Kwamba katika vitabu inaonekana mikoa hii haipati fedha. Sasa nilikuwa nataka tu nieleze kwamba, kwanza nataka niwahakikishieni hakuna upendeleo au uonevu katika mgao wa keki ya Taifa. Ila ni kweli kwamba, ni vigumu sana kulingana wote moja kwa moja. Ni vigumu kwa sababu tu wengine wana miradi ya miaka mingi. Kwa mfano, ukisema *UNICEF* iliingia lini Iringa mimi nadhani hata wote tuliokaa Bungeni miaka mingi tulikuta tu *UNICEF* iko Iringa miaka yote. *IFAD* wana mikoa fulani na kadhalika.

Lakini niseme tu kwamba, tatizo ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliona limekuzwa zaidi na utaratibu wetu wa namna ya kuandika mahesabu katika vitabu hivi vya Bajeti. Kwa hiyo, si kweli kabisa kwamba, mikoa hiyo hali yake ni mbaya kama ilivyosemwa. Nitatoa ufafanuzi kidogo, lakini tumekwishaiambia Wizara ya Fedha irekebishe kasoro hii. Kwa sababu kuna fedha ambazo zinakuwepo katika mikoa hiyo katika miradi fulani fulani, zile fedha zinaonekana tu kwenye maeneo yale yanayofanya hiyo shughuli. Kwa mfano, unaweza kukuta kama ni mradi wa maji, fedha zile zinakuwa kwenye maji. Sasa ukiangalia pale kwenye Bajeti kubwa huwezi ukaiona, lakini kumbe ipo. Kwa mfano, nikitoa tu mifano tukisema Shinyanga ambapo anatoka Mheshimiwa Derefa na Mheshimiwa Makolo. Wote tunajua kwamba, tuna miradi Shinyanga, tuna Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga ni mradi mkubwa tu, lakini haikuonekana hapa.

Mheshimiwa Spika, labda niitaje michache tu kwa mfano, kwa Shinyanga. Leo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi amewakaribisheni kwenye kusaini Mradi wa Barabara ambao pia Mheshimiwa Derefa alikuwa anauulizia sana. Leo mmesaini. Mwanza/*Shinyanga Border* kwenda Itinde shilingi 28 bilioni, Nzega - Tinde - Isaka, shilingi 20 bilioni, hizi zote zinatoka *European Union*. Kwa hiyo, utaona miradi ipo, lakini niseme tu kwa mfano, *Aforestation* Malya na Bariadi, hii ni midogo midogo shilingi 35 milioni. Lakini tuna *Sustainable Rural Water Supply* wa kama shilingi 17 bilioni, unaofadhiliwa na Netherlands, Tuna *Tanzania Netherlands Programme on HIV Control* shilingi bilioni 3, ambao pia ni wa Netherlands unajumuisha pia *Mwanza Reproductive and Child Health Initiative* shilingi 1.7 bilioni, *USAID*, *Natural Resources and Competent Center of Forestation, Agro Forestry Management and District Development* shilingi 552 milioni, *Participatory Irrigation Development Programme* ambao uko Shinyanga na Tabora *US Dollar* 17 milioni ambayo ni shilingi 17 bilioni, *Shinyanga Urban Water Supply* shilingi 77 milioni na *of course* na miradi mingine ya *TASAF* na iko mingine midogo midogo.

Kwa hiyo, inawezekana jinsi ambavyo miradi imekuwa inaripotiwa katika vitabu vyetu inaleta sura kana kwamba kuna watu wamesahaulika lakini kwa kweli hapana. Hata ukienda Kigoma sura ni hiyo hiyo. Ukienda Tabora ni hivyo hivyo. Kwa mfano, Kigoma kuna Mwandiga/Manyovu ambao aliisema Mheshimiwa Mbunge shilingi 478 milioni. Nataja tu ile mikubwa mikubwa, *Co-ordination and Micro Projects* ambao ulikuwepo tangu mwaka 1997 mpaka mwaka huu upo shilingi 1.7 bilioni, Kagera/*Kigoma Game Reserve Rehabilitation* shilingi 487 milioni mradi unaoendelea, *Kigoma Micro Project Component* shilingi 116 milioni unaendelea, *Lake Tanganyika Attachment Reforestation and Education* shilingi 323 milioni ambao ni mradi wa *SPRAA*.

*District Development Programme* mradi unaoendelea *Euro* 300 milioni ambao ni zaidi ya shilingi bilioni 3. Miradi ya *TASAF, Roads Rehabilitation and Upgrading Project* shilingi 9 bilioni, ambao unajumuisha pia Mikoa ya Shinyanga na Tabora.

*Improvement of Banana Croping in Kagera Region and Kibondo District* shilingi 463 milioni. *Rehabilitation of Kagera/Kigoma Game Reserve* shilingi 654 milioni. Mradi wa *EU* na kadhalika. Kwa hiyo, ninachotaka kusema tu ni kwamba, katika namna ambavyo vitabu vyetu vimekuwa vikiripoti kweli vinatoa picha kana kwamba kuna maeneo ambayo yameachwa. Lakini napenda tu kusema kwamba, tutafanya pale ambapo kweli inaonekana hakuna fedha nyingi za nje, tutafanya juhudi kuelekeza zaidi fedha katika maeneo hayo. Nataka kuwahakikishieni kwamba, haitusaidii kama Taifa, kama tutaweka maendeleo sehemu fulani na sehemu fulani ikabaki nyuma. Ni lazima wote twende mbele pamoja ndiyo tunakuwa na Taifa ambalo linaheshimika na watu wote wanafurahia shughuli zozote katika Taifa lao. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishieni tu pale ambapo pana upungufu tutajitahidi kurekebisha kadri inavyowezekana. Lakini kwa kweli ile sura iliyokuwa inatoka ni tofauti na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu la jumla, mambo mengi sana yamezungumzwa hapa kwa upande wa mahitaji ya barabara. Barabara za lami na zingine ambazo hazipitiki angalau zipitike, barabara ni tatizo kubwa. Mimi nimetembea sana nchi hii na najua hali za barabara na sehemu kubwa nimetembea sana kwa barabara. Nilipokuwa Rukwa nilitembea kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga kwenda na kurudi. Nilipokuwa Ruvuma nilitembea kutoka Songea mpaka Tunduru kwenda na kurudi na barabara hizo zote ni barabara ambazo tunazijua hali zake, pamoja na kwamba kuna juhudi mbalimbali kwa kweli ambazo zinafanywa sasa hivi za kuzikarabati, lakini tungelipenda ziwe za lami. Nina hakika Sumbawanga kwenda Tunduma hali ni hiyo hiyo, ingawa tunafanya juhudi sasa hivi kujenga madaraja na kadhalika.

Kutoka hapa kwenda Singida sasa hivi kuna juhudi zinazoendelea kwa mradi wa kutumia fedha zetu ili barabara hiyo iweze kutengenezwa. Kwa hiyo, lengo letu hasa ni kujitahidi zile barabara kuu kama nilivyosema kwenye hotuba. Tungelipenda sana barabara kutoka Dar es Salaam/Mwanza iwe ya lami, Dar es Salaam/Mtwara iwe ya lami, halafu tuunganishe na hizi za katikati Iringa/Arusha, Singida/Arusha na zile za Sumbawanga kule mpaka kwenda Kigoma na Tabora. Tabora wana tatizo kubwa sana la barabara. Kwa hiyo, bado mahitaji ni makubwa lakini tunafanya kila juhudi kadri tunavyoweza. Umeme ni tatizo kubwa. Najua Kigoma wana tatizo kubwa la umeme, Songea wana tatizo kubwa la umeme. Lindi/Mtwara wana tatizo kubwa la umeme, kwa maana ya miji mikuu ya mikoa. Kwa hiyo, bado tunayo kazi kubwa lakini tunaamini kabisa tunakwenda vizuri.

Maeneo ya utawala kuna watu wangelipenda Wilaya mpya zianzishwe kama Bukene kule. Mimi karibu sehemu nyingi nikipita naambiwa Rais aliahidi Wilaya hapa, sasa tunakutuma ukamkumbushe. Sasa mimi nasema, Rais hawezi kuanzisha Wilaya kila mahali. Kuna mambo ambayo lazima kwanza yakamilike. Tuwe na uwezo wa kuziendesha hizo Wilaya. Wale walioanzishiwa Wilaya sasa hivi unaona wanayozungumza ni kwamba, mnaanzishaje Wilaya bila ya kuweka kila kitu

kinachotakiwa. Lakini wakati wakiomba Wilaya wanasema sisi tunajitosheleza. Lakini mimi nina hakika kadri itakavyowezekana kwa jinsi ambavyo tungependa utawala uwe karibu na wananchi haya yote yatafanyika jinsi muda utakavyoweza kutupa nafasi. *(Makofi)*

Gesi ya Songosongo huu ni mradi wa miaka mingi sana jamani tusisahau. Huu mradi ulikuwa umekwama sasa umekwamuka na ni mradi ambao kimsingi ni wa binafsi. Gesi hii kwa jinsi ambavyo walifanya tathmini ikija Dar es Salaam ndiyo inaweza ikatoa manufaa zaidi kwa maana ya wale wenye Kampuni, lakini na gesi ikapata matumizi ya kutosha. Sasa kuna maneno mengine ambayo sitaki kuyarudia lakini vituo vya njiani kwa makubaliano yaliyokuwepo, wenzetu wa Nishati watakuja kuthibitisha vituo vile vya njiani watapata huduma za gesi. Kuna matoleo ya gesi hiyo na umeme. Kwa hiyo, si kwamba wengine wanasema Kusini tunadharauliwa tu, hapana sio kweli. Hii gesi imekuwepo miaka yote kama hao wasingelikuja ingelikuwa bado ipo mle mle Songosongo. Lakini mimi nina hakika kabisa kwamba, kwa juhudi ambazo sasa hivi zimeelekezwa Kusini, miradi hiyo itakapofanikiwa, suala halitakuwa umeme, ni mambo mengi sana yatazaliwa kule Kusini. *(Makofi)*

Suala la ajira kwa vijana nakubaliana kabisa ni jambo la kushughulikiwa. Lakini mimi nataka tuelezane vizuri zaidi. Tunapozungumza ajira ya vijana hivi hasa tunazungumza nini. Tunazungumza tutengeneze viwanda mjini ili vijana waajiriwe liko wapi. Kwa hiyo, mimi nadhani ajira nzuri na ninafikiri ndio lengo hili ambalo tunalitekeleza sasa la kuboresha kilimo. Kama tunaweza kuboresha kilimo vijana watavutika kubaki vijijini ili wafanye kazi za kilimo.

Sasa mimi nafikiri tunapozungumza ajira ya vijana, tuanze kujenga dhana ndani ya vichwa vya vijana kwamba ajira kwa kweli ni kwenye mashamba. Sasa iwe ni jukumu la Serikali na sisi wote kuhakikisha tunaboresha kilimo. Hilo ndilo jawabu la tatizo hili. Lakini tukijenga hisia kwamba kimbieni mjini mtapata ajira, hakuna kitu na uchumi utazidi kupata matatizo. Kwa hiyo, lazima tuboreshe kilimo. Mimi naamini kabisa tukiboresha kilimo tutakuwa tumetatua matatizo mengi sana na ndiyo lengo la Bajeti hii tangu mwaka 2002. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie mambo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, mojawapo ni kuhusu Tume Huru. Suala hili limezungumzwa sana na wenzetu wa Upinzani, wakasema haifai uchaguzi wa wananchi wote kuamuliwa na Tume iliyochaguliwa na Chama kimoja, kwa hiyo, tunataka Tume Huru.

Mheshimiwa Spika, nadhani yule aliyesema maneno hayo hakuwepo enzi hizo, lakini nina hakika alishiriki katika *White Paper*. Jambo hili lilikuwepo katika *White Paper*, tulilipeleka kwa wananchi, tukawaulizwa mnataka Tume ya Uchaguzi ya namna gani?

Mheshimiwa Spika, napenda niulize kwamba, Tume Huru maana yake nini? Hivi ukiwa na Tume ambayo Katibu Mkuu wa CCM yumo mle ndani, Katibu Mkuu wa *CUF* yumo mle ndani, wa CHADEMA naye yumo, hivi hiyo ni Tume Huru? Hiyo ndiyo

Tume ambayo siyo huru, kwa sababu kila mtu atakuwa anapambana kupigania upande wake. Haiwezi kuwa Tume Huru kwa sababu utakuwa unaweka Tume ambayo ina watu na kila mtu ana *interest* zake. Utakuwa huna Tume ya Uchaguzi, bali una genge tu ambalo linatetea maslahi yao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ripoti ya Jaji Kisanga, waliosema kwamba Tume iwe na wawakilishi kutoka Vyama vya Siasa, kutoka Zanzibar walikuwa asilimia 16.73 na kutoka Bara ni asilimia 11.01. Waliosema Tume iendelee kama ilivyo sasa, Zanzibar asilimia 83.24 na Bara asilimia 88.30, wastani ni asilimia 86.96 na wale waliotaka Vyama asilimia 12.52. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kinachonishangaza ni kwamba, Majaji wa Mahakama hawahusiki na Chama chochote, hawana Chama na Tume yetu inaongozwa na Jaji wa Mahakama ya Rufaa, lakini bado watu wanasema, tunataka Tume Huru. Kwa hiyo, kama tunataka Tume ambayo kwa kweli itatenda haki bila kutazama upande wowote ni Tume ambayo itateuliwa na ni ya watu ambao hawahusiki na Chama chochote. Sidhani kama kuna mtu ana wasiwasi na *integrity* ya wale watu. Ndiyo, wala hakuna mtu ambaye amewahi kusema hapa Tume imefanya kitu fulani ambacho si sahihi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI MKUU:** Hakuna! Labda kama kuna tafsiri ya uhuru ambayo siijui, lakini kama ni hiyo ninayoijua, nadhani haina tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu Katiba mpya. Sisi tunasema kwamba, Katiba tuliyonayo ni halali na Wataalam wa Mambo ya Katiba walilichunguza jambo hili na wakasema kwamba, Katiba yetu ni halali. Lakini wakati wa *White Paper* tulisema pia kwamba, Katiba siyo msahafu, inabadilika kadri mazingira yanavyobadilika kwa kufanya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali tunajiandaa kuleta marekebisho ya Katiba. Ninyi wa Upinzani mnaosema mnataka Katiba mpya, hayo maeneo mnayotaka kubadilisha leteni, nani amekataa? Tutaangalia kama tunaona yanafaa tutayabadilisha, lakini kama tunaona hayafai tutawaambia ni kwa nini hayafai. Maana naona tu watu wanazungumza kwamba, wanataka Katiba mpya, ukimuweka chini ukamwambia hebu niambie katika Katiba hii ni sehemu gani huipendi? Ataanza kusema, aah Bwana hii ni ya Chama kimoja, tunataka Katiba mpya. Nani kasema? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ina-*accommodate* huu utaratibu wa Vyama Vingi, lakini endapo kuna mahali ambapo Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba panamkera, alete hoja hapa Bungeni, tutaiangalia na tutaibadilisha kama tunaona ina maslahi, lakini kama haina maslahi tutamwambia bwana haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni hili la Serikali tatu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, alilieleza vizuri sana na kwa ufundi mkubwa kabisa. Nilimsikia Mheshimiwa sijui anaitwa nani?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Karim.

**WAZIRI MKUU:** Ndiyo, Mheshimiwa Karim Said Othman, alisema Muungano una matatizo na dawa yake hamtaki tu, lakini ni Serikali tatu. Hakueleza hiyo dawa inaponyesha nini katika huu Muungano na wala hakusema sasa hivi anakosa nini kwa kuwa na Serikali mbili na Mheshimiwa huyo ameelezea zile tarakimu, lakini sitaki kuzirudia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wa pande zote mbili walioanzisha Muungano, waliona mbali zaidi. Leo Tanzania ina watu 34.6 milioni, Zanzibar ina watu 984,000, Bara ina kama watu 33.6 milioni, kwa idadi ya Watanzania wote, Zanzibar ina asilimia 2.8, Bara ina asilimia 97.2 na ukienda kwenye raslimali bila shaka ni hivyo hivyo. Sasa, ukisema Serikali tatu, maana yake ni kwamba, uwe na Serikali tatu, uwe na Marais watatu, Rais wa Bara, ambaye atakuwa Rais wa watu 33.6 milioni na *resources* zote. Utakuwa na Rais wa pili ambaye ni wa Zanzibar, atakuwa Rais wa watu 900,000 na *resources* za Zanzibar, halafu utakuwa na Rais wa Muungano, ambaye kwa kweli atakuwa hana watu hasa. Kwa hiyo, atakuwa Rais anayeelea elea tu hapa na atakuwa na Baraza la Mawaziri.

**WABUNGE FULANI:** Atakuwa na Maruhani! *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Kwa hiyo, napenda tuwashukuru sana Waasisi wetu pamoja na kwamba sasa hivi wao ni Marehemu, lakini walifanya jambo la busara sana. Binafsi nimeliangalia sana hili jambo, hizi Serikali tatu ambazo watu wanadai ni kutokuangalia mbali, unaangalia tu hapa, yaani akimaanisha karibu. Ukiangalia mbali Serikali tatu katika mfumo huu haiwezekani, utaleta tu fujo ndani ya nchi. Unawezaje kuwa na Rais anayesema yeye ni Rais wa *federation,* lakini kati ya wale wawili wanaotakiwa wawe wadogo zake, mmoja ni *so powerful,* ana watu karibu sawa tu wa eneo lote, haiwezekani! Kwa hiyo, acha hii ndoto ya Serikali tatu, haifai na wala haina maslahi! Serikali mbili tutaendelea nazo.

**WABUNGE FULANI:** Moja! *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Napenda kusema kwamba, Ilani cha Chama cha Mapinduzi, pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema mfumo wa Serikali...

**WABUNGE FULANI:** Mbili!

**WAZIRI MKUU:** Lakini hiyo ya tatu, yaani haifai! Kwa hiyo, napenda niwaeleweshe hivyo tu, acheni hiyo ndoto ya Serikali tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilieleze hapa ni lile ambalo niliigusia huko mwanzo, dhana ya Utawala katika Mfumo wa Siasa ya Vyama vingi. Inawezekana wengine hawaielewi sawa sawa dhana hiyo. Leo tuna Vyama 16 katika nchi yetu na Vyama hivyo ni tofauti kwa sababu kila kimoja kina Itikadi yake, kila

kimoja kina Sera zake na kama ni wakati wa uchaguzi bila shaka kila kimoja kitakuwa na Ilani yake. Kuna dhana inajengeka kwamba, mfumo wa Vyama Vingi ni CCM dhidi ya Vyama vingine au Vyama vingine vyote na vyenyewe ni Chama. Kama Vyama vingine vyote ni Chama, basi jiungeni kwenye Chama kimoja, inakuwa rahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu ukirudi kwenye hili suala la kodi, jambo ambalo kwa bahati mbaya sana watu wamelirukia tu, siyo lao, siyo la Upinzani. Sasa katika hiyo kodi wanasema hiyo ni Sera ya Upinzani. Binafsi ninajiuliza, hivi ninyi Wapinzani yaani kwenye kodi tu ndiyo wote mna Sera moja? Kwenye kodi zingine zote hamkuwa na Sera moja, ni kwenye hii kodi ya maendeleo tu ndiyo mmekuwa na Sera moja? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwaulize hao Wapinzani, siyo kwamba nataka wanijibu, lakini nataka tu wanipate. Kama mnasema hii ni Sera yenu, ninaamini haikuzaliwa leo na kama ndiyo Sera yenu, ni kwa nini basi hamkuchaguliwa mwaka 2000, kwa maana ya Chama chenu kuwa Chama Tawala? Kwa hiyo, si Sera yenu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hawa jamaa wanasema ni Sera yao, ziko Halmashauri ambazo wao wanaziongoza, nataka niambiwe kama hiyo ni Sera yao, maana kama ni Sera yako unaitekeleza, ni kwa nini Karatu hawakuondoa kodi kama ni Sera yao? Kwa nini Kigoma hawakuondoa kodi kama ni Sera yao? Kwa nini Hai hawakuondoa kama ni Sera yao na kwa nini Bariadi hawakuondoa kama ni Sera yao? Leo CCM imeondoa kodi wanasema ni Sera yao, hivi vitakuwa ni vituko vya ajabu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema inawezekana watu hawaelewi dhana ya Vyama Vingi. Kila Chama kina Sera zake na Itikadi yake, haiwezekani kukawa na Itikadi na Sera ya jumla ya Vyama vyote vya Upinzani! Hakuna kitu cha namna hiyo, vinginevyo Ndugu Tendwa, angevifuta hivyo Vyama akaandikisha Chama kimoja tu halafu wote mkajiunga humo.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati fulani timu za mpira zilicheza, timu moja ikawa hoi sana, ikawa inafungwa magoli, walipoona sasa hakuna ujanja, hakuna namna ya kuifunga ile timu nyingine wao wanafungwa tu, wakaanza kufunga magoli kwenye lile goli lao. Mpira ulipoisha nao wakashangilia kwamba na wao wameshinda maana wamefunga magoli kwenye goli lao. Sasa, usikute wenzetu wamezidiwa wanataka kufunga magoli kwenye goli lao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda nizungumzie kwa kifupi sana juu ya umuhimu wa Umoja wa Taifa letu. Jambo moja kubwa kabisa katika Umoja wa Taifa letu ni Muungano wetu. Kwa hiyo, ni lazima tukubaliane kwamba, hakuna mtu kuchezea Muungano wetu, tutaulinda Muungano wetu kwa uwezo wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere wakati alipokuwa hai alituambia, tuache mambo ya kubaguana, siku mtakapoanza kubaguana hayataishia hapo tu, mtaanza kuona kati yenu kuna Watanganyika na Wazanzibari, Wazanzibari na Wazanzibara na kati ya

Wazanzibari mtaanza kuona Waunguja na Wapemba, baadaye Waarabu na kadhalika. Ni lazima umoja wetu tuuangalie sana na kama kuna kitu cha thamani katika nchi hii ni umoja wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amani yote hii tunayoizungumzia ni kwa sababu Watanzania tuko kitu kimoja na tunaheshimiana. Ninaogopa sana tukianza kwa mfano, kutengeneza Sera za kusema kuna Watanzania weupe, Watanzania weusi, Watanzania wa njano na kadhalika. Hiyo haitusaidii hata kidogo. Nakubaliana na Sera tunayoitengeneza na Sheria tuliyonayo hapa Bungeni ya kusema tuwaangalie Watanzania, lakini tusiweke rangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo ambao wamebahatika tu kuwa weupe kama Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Mwapachu. Ukitembea Vijijini wapo Waarabu wengi sana, lakini ni wa miaka nenda rudi hata hawajui kwao kwingine ni wapi zaidi ya Tanzania. Sasa, watu kama hao huwezi kusema unapotaka kuzungumzia masuala ya kuwaangalia Watanzania unawaondoa, haiwezekani. *(Kicheko/Makofi)*

Wale Wahindi mnaowaona Dar es Salaam, siyo kwamba wote wana hali nzuri, wako wenye hali hoi kweli kweli. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, tusianze kuangalia hili suala la kutaka kujigawa kwa rangi zetu. Nakubali kuna watu wenye hali nzuri na kuna wale wenye hali za chini, sasa tuangalie wale wa hali ya chini, awe mweupe, awe wa kijani au awe mweusi ili mradi yuko katika hali ya chini ni Mtanzania, kwa hapo sina ugomvi hata kidogo, napenda tuelewane hivyo. *(Makofi)*

Tusije kuwafanya watu wengine wakajisikia wana hali mbaya sana na wasijisikie raha ya kutembea katika nchi yao. Kuna watu wana rangi nyeupe, lakini ukifuatilia katika nchi hii wameishi kwa muda gani, utashangaa kuona wamekaa muda mrefu kuliko sisi wengine ambao ni weusi! Kwa hiyo, tusianze kubaguana kwa misingi ya rangi. Napenda suala hilo lieleweke hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo alilizungumza Mheshimiwa Mutungurehi, lakini nadhani tatizo lake ni Kiswahili. Alisema, kwanza niwaombe radhi Watanzania, eti kwa kuwasababishia kero ya ulipaji kodi, lakini lingine alilirukia, ambalo si la kwake, la kusema watu waliofungwa kwa kutolipa kodi wasamehewe. Suala hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, wakati wa Hoja ya Waziri wa Fedha. Rafiki yangu huyo aliidandia, haina neno! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, tulipokuwa tunalipa kodi ya maendeleo halikuwa kosa, ndiyo maana nasema, labda tatizo la Mheshimiwa Mutungirehi ni Kiswahili, maana yeye alifikiri kwamba kulikuwa na kosa na sasa tumelirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapakuwa na kosa, ilikuwa ni halali, kodi ilikuwa inalipwa kwa ajili ya maendeleo. Katika makusanyo yetu tumefikia kiwango kizuri tukaona sasa tunaweza kusamehe hii kodi na shughuli zetu zikaendelea vizuri. Ndiyo maana nilieleza kwamba, jambo hili lilianza kufanyiwa kazi tangu enzi za Mzee Ngombale-Mwiru akiwa

Waziri wa *Local Government*, kwa sababu ilikuwa ni lazima tufanye uchambuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haiwezi ikaamka tu asubuhi ikasema tunafuta kodi! Ni lazima iangalie ikifuta hiyo kodi itajazaje hilo pengo, kodi gani ifutwe, iende wapi na tufanyeje. Kazi hiyo ilichukua muda kidogo na sasa tumeshafikia tamati yake, ndiyo maana tumefuta hiyo kodi. Nakubaliana na Mheshimiwa Profesa Sarungi, anasema nikusamehe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kusema kwamba, nimeweza kusimama hapa kwa saa 1.25, kwa sababu ya misaada ambayo nimepewa na timu yangu ambayo iko pale ya Mheshimiwa William V. Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. Pia, napenda nimshukuru sana Katibu Mkuu na timu yake, kwa misaada yote ambayo wametupa ili kuweza kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuwahakikishia kwamba, *material* waliyotupa ni mengi sana, nimeshindwa kuyasema yote hapa, ndiyo maana nimesema tutakwenda kuyaweka katika sura ya kitabu ili tuweze kuyafanyia kazi. Napenda kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika hoja zile tulizozizoea mtoa hoja akishakamilisha hoja yake huwa tunawahoji ili mtoe uamuzi. Katika hoja hizi za Bajeti haiwi hivyo, hatua ya kuwahoji bado haijafika. Hoja ilikuwa ni kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na tutapitisha makadirio yenyewe kwenye Kamati. Kwa hiyo, tutakapomaliza Kamati, Mheshimiwa Waziri Mkuu au mmojawapo wa Mawaziri wake wa Nchi, atatoa Bungeni taarifa ya kazi iliyofanywa na Kamati kwamba, Bunge sasa liikubali taarifa hiyo. Nitakapowahoji, ndiyo tutapitisha makadirio ya ofisi hii. Kwa hiyo, sasa tunakwenda kwenye hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

## FUNGU 25 - OFISI YA WAZIRI MKUU

Fungu 25 - Waziri Mkuu .... ..... ....... ..... Sh.1,127,602,200/=

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii *Subvote 1001 - Administration and General*, nipate maelezo tu kwamba, ni hatua gani zinazochukuliwa kuhusu suala la umeme? Naomba nipate maelezo ya Serikali kwa sababu Viongozi wote wamekuwa wakija pale wanaelezwa, lakini wanatoa ahadi hizo. Sasa maelezo ni yapi?

**MWENYEKITI:** Aah, maelezo yameshatolewa wakati wa *winding up,* wewe ulikuwa nje? *(Kicheko)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa ..... ... Sh.8,677,364,100/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu ...... ....... ... Sh.12,418,696,800/=

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 37 Subvote 1001,* kifungu namba 250100 - *Basic Salaries,* nilitaka tu ufafanuzi kwamba mwaka 2002, tulikuwa tumepatwa na janga la maafa katika Kijiji cha Chihanga kulitokea mafuriko, lakini hatukupata msaada wowote. Sasa nilikuwa nataka maelezo yake niweze kujua kwa nini hatukupata msaada kutoka katika Mfuko wa Maafa?

**MWENYEKITI:** Hicho kifungu ulichokitaja ni *Basic Salaries*. Sasa utapata msaada kutoka katika mishahara ya watu? *(Kicheko)*

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Naweza kushika mshahara wake kwa sababu katika kitabu hiki ukiangalia kuhusu suala la maafa halipo kabisa, ndiyo maana nimekuja katika kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Fungu la maafa hatujalifikia.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halipo.

**MWENYEKITI:** Tuna utaratibu wa *programs* kwa mfano *program 10* nakadhalika. Sasa ngoja niwe na hakika, Mheshimiwa Waziri, maafa ni program gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na hilo alilozungumza Mheshimiwa Mbunge, utaratibu niliusema mchana wa kupewa taarifa juu ya maafa yanayotokea katika ngazi mbalimbali. *Program* ni ya 20 ukurasa wa 89 lakini kwa bahati mbaya sana hilo analolisema Mheshimiwa Mbunge ndiyo kwanza nalisikia hapa. Inawezekana lilielezwa katika ngazi inayohusika na maafa hayo na likashughulikiwa katika ngazi ile ile. Si kila jambo lazima lifike katika ngazi ya Taifa. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sisi *procedure* zote tulizifuata Kiwilaya, tuliandika tukapaleka Mkoani na nilipofuatilia Mkoani nako nikaambiwa kwamba imepelekwa kwenye ngazi ya Taifa. Hali halisi si nzuri hata ya kisiasa kwa sababu hata pale kijiji kizima watu walirudisha kadi pia. Sasa sijui mtanisaidiaje hilo?

**MWENYEKITI:** Lakini hii ni bajeti ya mwaka ujao wa fedha wa 2003/2004, hayo maafa yalitokea katika bajeti ya mwaka huu wa 2002/2003, kwa hiyo hapa si mahali pake.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima niliuliza kama wengine walivyokuwa wanachangia na kwa kuwa hiki kifungu 250100 kinahusu mshahara katika Ofisi ya Waziri Mkuu, nikiuliza katika utendeji na ku-*suggest* kwamba, kama tulivyowasamehe wale ambao hawakulipa kodi, basi wale waliofungwa waweze kutafutiwa namna ya kusamehewa. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati anajibu alisema badala ya kuwasamehe hao wamenisamehe mimi! Sikasiriki kwa lugha aliyosema kwamba sielewi kiswahili, nadhani ilikuwa ni utani kwa sababu nina shahada katika *linguistics* na lugha mbili za Kimataifa. Sasa nilipenda kujua kama bado wazo hili analichukua kwamba Serikali inatafuta utaratibu wa kuwasamehe au bado anaendelea kusema kwamba amenisamehe mimi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati akitoa maelezo Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema, kama kuna adhabu ilitolewa, ilitolewa kihalali kwa sababu ukusanyaji wa kodi wakati ule ulikuwa unafanywa kihalali. Ndiyo alivyosema na nafikiri inajibu swali lake. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Subvote 2001 - Civil Affairs and Contingencies,* katika majibu ambayo yalikuwa yametolewa asubuhi na Waziri anayehusika, tulizungumzia juu suala la njaa na maelezo yalikuwa ni kwamba, wananchi chakula walichonacho wakitunze na pia wale wenye mifugo wauze mifugo ili waweze kununua chakula. Swali ni kwamba, yale maeneo ambayo hawana chakula, lilikuwa ni tegemeo letu kwamba Serikali ituambie kwamba, Serikali ina chakula kiasi gani *in stock,* kiasi gani kimeagizwa na kiasi gani kitapelekwa katika yale maeneo, ili wananchi wakiuza ng'ombe wao na mifugo yao wapate fedha waweze kununua chakula *at spot.* Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba, asubuhi Mheshimiwa Semindu Pawa, aliuliza swali hilo hilo wakati wa maswali asubuhi na nilijibu vizuri na Waheshimiwa Wabunge walinielewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huna sababu ya kurudia majibu hayo.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia *program 50 Subvote* 5001 kifungu kidogo cha 280500 - *Transfer and Subsidy-Institutions at the same level of Government.* Katika kifungu hiki kwenye maelezo ya vitabu vya Wizara, ambavyo hapa havipo, walituonyesha kwamba kifungu hicho kinakwenda *CDA*. Ukikilinganisha kifungu hicho na kifungu kingine katika kitabu ambacho hatujakifikia lakini kinaonyesha katika *program* ya 4451 *CDA* imepewa shilingi milioni 71. Katika kuchangia kwa maandishi, niliomba maelezo ya kina kwamba, ni muda wa zaidi ya

miaka 31 tangu tumeweka Sera ya Kuhamia Dodoma. Kwa bahati mbaya tangu tumeweka hiyo sera haijafanyiwa tathmini katika utekelezaji na manufaa yapi na athari zake ni zipi. Isitoshe baada ya kuweka hivyo, hatujaangalia vile vile ni gharama kiasi gani ambayo Taifa limeingia. Sasa najua ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, lakini sera ni kwa manufaa ya Taifa. Nilipendekeza kwamba, ingelifaa sasa tuweke Kamati Maalum ya kutathmini sera hiyo kama Bunge, ili kuona fedha ambazo tunazitumia ziweze kutumika vizuri zaidi katika namna nyingine au ziendelee kutumika kwa njia hii. Ukitazama katika kifungu hiki nilichokitaji, imetolewa kwa *CDA* kwa matumizi ya kawaida shilingi 639.8 milioni. Lakini kazi wanayofanya ni ya shilingi milioni 71, maana yake matumizi ya kawaida ni zaidi ya mara 9 kuliko fedha ambazo wanapewa kwa ajili ya kazi ya maendeleo.

Sasa kazi wanayopewa wangeweza kupewa vile vile Manispaa ya Dodoma wakaifanya kama ilivyo kwa watu wengine. Shilingi milioni 71 ni kwa ajili ya maua, kwa ajili ya mitaro kwa ajili ya nini? Sasa haya ni matumizi ambayo si mazuri kwa kweli ukiangalia. Aidha, nikapendekeza tathmini hiyo ifanyike au kuwe na utaratibu makusudi wa kisheria ambao tunahakikisha kwamba tunaweka *Action Plan* ya kuhamia Dodoma. Sasa sikupata maelezo yoyote katika majibu, ningependa nipate maelezo ya ufafanuzi na ninategemea kutumia kifungu cha 81 baadaye kama sitapata maelezo ya kina. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kifungu alichokitaja hapa kinasomeka kiasi cha fedha shilingi milioni 639,846,700, hiki ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya *CDA* na Dakawa. Lakini ni kweli vile vile kwenye kitabu namba nne kuna fedha shilingi milioni 71, ambazo ni kwa ajili ya maendeleo ya shughuli mbalimbali za maendeleo ya *CDA*.

Lakini ni ukweli ulio wazi kwamba, si yeye pekee, Waheshimiwa Wabunge pia, wamezungumzia juu ya *CDA* leo na majibu yangu yalikuwa wazi. Si leo tu, miaka yote tumekuwa tunasema kwamba, lengo la *CDA* tangu ilipoanzishwa mpaka sasa ni kuhakikisha na kusimamia uhamishaji wa Makao Makuu kuja Dodoma.

Mwaka huu tumeweza kuwapa hizo fedha kidogo, japo anasema kidogo lakini si kweli kwamba watu wa *CDA* wanategemea fedha hizi pekee katika shughuli za maendeleo. Serikali imewapa uwezo kwenye vyanzo vyake, wanavyo vyanzo vya ndani ambavyo wanakusanya *CDA* vinavyowezesha kufanya shughuli nyingine za maendeleo zaidi ya fedha hizi zinazoonekana hapa. Fedha hizo huwa zinakusanywa na *CDA* na zinaamuliwa na Bodi, siyo na Bunge hili.

Kwa hiyo, ukichukua hizi shilingi milioni 71 na ukichukua vyanzo mbalimbali walivyonavyo *CDA* idadi yake ni kubwa zaidi ya hizi shilingi milioni 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu maelezo kwamba, nyumba zote mnazoziona hapa Dodoma, ambazo kwa miji mingine tumezoea kuita Msajili wa Majumba na National Housing, hizi ni nyumba zinazomilikiwa na *CDA.*

Pango lake linapelekwa *CDA*. Mpaka mwishoni mwa mwaka 2002, miundombinu ya maji machafu hapa Dodoma ilikuwa inamilikiwa na *CDA*, kodi zote zilikuwa zinalipwa kwa *CDA,* kodi za Viwanja. Kwa hiyo, wana mapato mengine zaidi ya haya. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hizi shilingi milioni 71 zimetolewa tu kwa Mradi Maalum.

Lakini bado *CDA* inasaidia Serikali katika jukumu lake la msingi ku-*facilitate* uhamishaji wa Serikali kuja Dodoma kama kazi yake ya msingi. Kazi hii inatekelezwa, tumeshuhudia katika miaka hii mitatu tangu 2000 Wizara kadhaa zimehamia hapa kwa msaada mkubwa sana wa kutafuta maeneo na majengo mbalimbali uliofanywa na *CDA*. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, yamefafanua matumizi tu ya mafungu niliyoyataja, lakini hayajaeleza kama anakubaliana au hakubaliani na pendekezo la kwamba sasa tufanye tathmini na kwamba sasa imefika wakati tuweke *Action Plan*.

Ninakumbuka toka mwaka 1996 nikiwa katika Bunge hili majibu ni kwamba tutahamia Dodoma na baadhi ya Wizara zimehamishiwa kweli hapa, lakini ukiangalia katika hali halisi wengi utakuta safari mara nyingi ni kwenda Dar es Salaam kwa hiyo gharama zinazidi kuwa kubwa kwa Taifa. Sasa kutokana na hilo, mimi ninaomba kwa kuwa siridhiki nitumie kifungu cha 81(2) (c) kutoa shilingi moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, sasa ngoja niwasomee kifungu chote hicho kwa wale ambao hawana kanuni. Kinasema: “Mbunge yeyote aweza kutoa hoja isiyokuwa na mjadala ya kupunguza shilingi moja katika kifungu chochote, ndiyo hoja aliyoitoa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. Madhumuni halisi ya hoja hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyeitoa aweze kueleza kutoridhika kwake na yeye Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ameeleza kutokuridhika kwake. Sasa linalofuata hoja hiyo itaamuliwa bila mjadala wowote.

Lakini Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu yake kwa hoja ikiwa atakuwa hajayatoa. Sasa kama Waziri unataka kutoa majibu zaidi ya hayo uliyoyatoa unapewa nafasi la sivyo sasa tuiamue hoja hiyo. Wanaokubaliana na Mheshimiwa Dr. Slaa, kwamba, fungu hili lipunguzwe shilingi moja, wanaokubaliana waseme "Ndiyo".

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Wasiokubaliana waseme "Siyo".

**WABUNGE FULANI:** Siyo.

**SPIKA:** Sijatoa uamuzi sasa wewe unafanya fujo. *Sergeant-at-arms* kaa tayari tayari. *(Kicheko/Makofi)*

Wasioafiki wameshinda kwa hiyo fungu linabaki hivyo hivyo. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 42 - Ofisi ya Bunge ...... ...... ..... Sh. 11,339,395,600/=
Fungu 54 - Redio Tanzania .... ...... ..... Sh. 3,892,859,300/=
Fungu 61 - Tume ya Uchaguzi ... .... Sh. 1,829,714,700/=
Fungu 91 - Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya .... .... ..... Sh. 665,261,600/=
Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti Ukimwi ... ... Sh. 4,294,982,000/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu ... ... ... .... Sh. 4, 067,610,100/=
Fungu 42 - Ofisi ya Bunge ... ... ... .... ... ..... Sh. 5,300,000,000/=
Fungu 54 - Redio Tanzania ... ... ... .... . ....... Sh. 300,000,000/=
Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti Ukimwi ..... ...... Sh. 10,427,184,900/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2003/2004, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyalikubali makisio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Bunge limepitisha Makadirio ya Ofisi Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa kazi zilizopangwa kwa ajili ya siku ya leo. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi, tutakapojadili hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

*(Saa 12.48 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 26 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*